

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 22 Aprili, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Tobacco Board for the year ended 30<sup>th</sup> June, 2007*).

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2006/2007 (*The Annual Report and Accounts of the Higher Education Students Loans Board (HESLB) for the year 2006/2007*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2006/2007 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Education Authority for the year 2006/2007*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 132

## **Hali mbaya ya Walimu na Shule za Msingi**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. BENITO W. MALANGALILA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa Serikali imetenga fedha nyingi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini pamoja na fedha hizo kutengwa bado hali siyo nzuri katika elimu ya msingi nchini:-

- (a) Je, Serikali inaelewa kuwa bado wapo walimu katika shule za msingi wanaoishi katika nyumba za nyasi?
- (b) Je, Serikali inaelewa kuwa wapo wanafunzi wanaosomea chini ya miti katika baadhi ya shule za msingi nchini?
- (c) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kutatua matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu haina taarifa rasmi kuhusu walimu wanaoishi katika nyumba za nyasi pamoja na kwamba tunaelewa kuwa kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu hapa nchini. Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2001 hadi 2007 jumla ya nyumba za walimu 10,968 zilijengwa nchi nzima kwa lengo la kuwapa walimu nyumba na hasa shule za vijijini ambapo upatikanaji wa nyumba za kupanga huwa ni haba.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kuwa upo upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule nyingi za msingi. Hata hivyo, mkakati wa muda unaotumika ili kupunguza tatizo hili ni kuwapanga wanafunzi kwa zamu (*double shift*) katika vyumba vilivyopo. Aidha, katika utekelezaji wa MMEM mwaka 2001 mpaka 2007 jumla ya vyumba vya madarasa 42,542 vilijengwa kote nchini. Kutokana na idadi kubwa ya watoto wanaoandikishwa darasa la kwanza kwa kila mwaka inawezekana kabisa yapo maeneo ambayo madarasa hayatoshelezi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua matatizo ya upungufu wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa, kulitokana na ongezeko la uandikishaji wanafunzi na ajira ya walimu, imeanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (MMEM) II kuanzia 2007-2011). Kupitia mpango huu jumla ya vyumba vya madarasa 45,012 na nyumba za walimu 89,744 vinatarajiwa kujengwa ifikapo mwaka 2011 kwa lengo la kupunguza upungufu huo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2008/2009; nyumba

za walimu 21,936 na vyumba vya madarasa 10,753 vinatarajiwa kujengwa kote nchini kulingana na ratiba ya mpango huu wa maendeleo ya elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliopo wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa utaendelea kupungua kadri fedha zinavyopatikana na wananchi kuendelea kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa majengo hayo. Aidha, Halmashauri zote nchini zinashauriwa kuelekeza fedha za ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu kwenye maeneo ambayo yana upungufu mkubwa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika vikao vya Halmashauri kuhimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchangia ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi kutokana na mapato yake yenyewe, fedha za miradi mbalimbali kama vile *TASAF*, *LGCDG Local Government Capital Grants* pia kuwahamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi zao, ili kuvutia mazingira mazuri ya kuwaweka walimu wasiondoke katika maeneo ya pembezoni,

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na juhudi za Serikali na naipongeza kwa kufanya bidii na kwa kuwashirikisha wananchi kuongeza madarasa na nyumba za walimu. Lakini bado inaonekana kwamba kasi ya ujenzi wa nyumba za walimu na madarasa hakuna uwiano kati ya majimbo na majimbo au wilaya na wilaya, ziko nyingine ziko mbele, ziko zingine ziko nyuma. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wale walioko nyuma ili tuweze kuwapa nguvu zaidi ili waweze kufanya uwiano na wenzao katika suala hili?

Mheshimiwa Spika, la pili, niliuliza swali hapa kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina ziada ya walimu karibu 2,000 na wanatakiwa waajiriwe na sisi tuna uhaba wa walimu. Je Serikali imefikia wapi uamuzi wa kuwaajiri walimu walioko Zanzibar? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mpango wa elimu ya msingi katika programu ya kwanza kuna Wilaya ambazo ziko nyuma na wilaya ambazo ziko mbele. Tukiangalia ni sababu gani ambazo zinafanya Wilaya nyingine ziwe nyuma na Wilaya nyingine ziwe mbele, ziko sababu nyingi. Lakini sababu kubwa ni kwamba kuna sehemu ambazo wananchi wamejitolea kwa dhati na wameelewa mpango wa MEM. Kwa hiyo, wao wako mbele. Lakini kuna sehemu ambazo wananchi naweza kusema kwamba ni wavivu hawataki mambo ya kujitolea. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga. Lakini ukiangalia Mikoa mingine wananchi wameelewa mpango wa MEM na wanajitolea vizuri sana. (*Makofi*)

Mimi niwaombe tu ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuwahimiza wananchi katika kujitolea. Serikali peke yake haiwezi ikatoa mchango mkubwa. Sababu nyingine ni vipaumbele vya Halmashauri. Kuna Halmashauri nyingine hawatoi kipaumbele katika suala la elimu. Kwa hiyo, masuala ya elimu utakuta mara nyingi yanarudi kwa sababu hawaweki vipaumbele katika suala la elimu.

Swali la pili, kuhusu walimu walioko Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Maongezi yanaendelea kati ya Wizara ya Elimu, Wizara yangu pamoja na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona uwezekano ambao utatuwezesha kuwaajiri au kufanya njia yoyote ya kusaidia upungufu wa walimu katika Tanzania Bara. Hata hivyo, Wizara ya Elimu ya inazidi kuwasomesha walimu wengi zaidi ili kuweza kukabiliana na tatizo hili. Tatizo hili litapungua jinsi walimu wanavyotolewa katika vyuo vyetu mbalimbali.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna mpango kabambe wa MEM II. Katika MEM I, Wilaya ya Geita walijitolea sana wananchi kwa kufuata kauli ya Serikali kwamba wajenge maboma na Serikali itaezeka. Wakafanya hivyo, wakajitahidi kwa nyumba za walimu na madarasa.

Sasa tatizo likaja Serikali ikashindwa kuezeka. Sasa katika MEM II, inasemaje Serikali sasa kuanza na Geita ikaondoa hiyo aibu ya maboma ambayo hayajaezekwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana wenzetu wananchi wa Geita kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Ni mfano ambao ni wa kuigwa kwa Watanzania wengine kwa juhudi zao za kujitolea katika juhudi za maendeleo. Katika MEM II, kitu kikubwa kitakachoangaliwa ni vile viporo ambavyo vilikuwa havijamalizwa katika mpango wa elimu ya msingi MEM I. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wa MEM II suala la maboma ambayo yamejengwa kule Geita litapewa kipaumbele na niwaombe wenzetu wa Halmashauri kwa kutumia fedha za *Local Government Capital Development Grants* kutumia fedha hizo kupeleka kwenye madarasa ili kutodhoofisha nguvu za wananchi ili waendee kujitolea katika miradi mingine. (*Makofi*)

Na. 133

### **Mpango wa kupunguza msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshaahidi kuwa ina mikakati ya kupambana na tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam:-

Je, mipango hiyo iko kwenye hatua gain?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika Jiji la Dar es Salaam kuna tatizo kubwa sana la msongamano wa magari na Serikali inalitambua tatizo hili. Serikali imechukua hatua za muda mfupi na muda mrefu kwa jitihada za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Hatua za muda mfupi, wakati tukiingoa zile muda mrefu ni kama zifuatazo:-

(i) Kuongezwa kwa ufanisi wa matumizi ya njia tatu: Serikali imeanzisha matumizi ya njia tatu kwa barabara za Morogoro na Ali Hassan Mwinyi nyakati za asubuhi kuanzia (saa 12:00 hadi saa 3:00) na jioni kuanzia (saa 10:00 hadi saa 2:00 za usiku). Aidha, Wakala wa Barabara *TANROADS* imefanya maboresho ya barabara ya Bagamoyo kuanzia makutano ya Ali Hassan Mwinyi na barabara ya Kawawa kuelekea Mwenge kwa kuongeza njia moja ili kuwezesha njia tatu kuanzia eneo la Makumbusho hadi barabara ya Morocco.

(ii) Njia ya pili, kuendelea kwa Maboresho ya Barabara za Kiungo (*Ring roads*); *TANROADS* na Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam zinaendelea na juhudi za kuboresha barabara za pete (*ring roads*) katika barabara kuu za jiji kama vile Barabara ya Sam Nujoma inayoshughulikiwa na (*TANROADS*), Barabara ya Goba (Kinondoni) na Barabara ya Kinyerezi (Ilala).

(iii) Ukarabati wa taa za kuongozea magari, *TEMESA* na *TANROADS* wamekwishafanya matengenezo kwa taa za barabara kuu.

(iv) Kuzuia magari makubwa kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam, malori yamezuiwa kuingia katikati ya jiji la Dar es Salaam wakati wa asubuhi ambapo watu wanaelekea kazini na wakati wa jioni wakati wanaporudi. Ili kutekeleza azma hii Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imefuta Kituo cha malori eneo la Jangwani na kukihamishia eneo la kugesha malori sehemu za Mbezi.

(v) Kuhamasisha uwekezaji wa shughuli mbalimbali pembezoni mwa jiji (*satellite cities*) kama vile ujenzi wa Ofisi, Maduka makubwa (*super markets*), shule na kadhalika badala ya kuendelea kujenga katikati ya jiji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mkakati ya muda mrefu utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendeleo haraka (*Dar Rapid Transit-DART*) umeendelea kuongezewa kasi ili kuwezesha kujengwa kwa miundombinu inayokidhi watumiaji wote wa barabara na matumizi ya mabasi yenye ujazo mkubwa wa kupakia abiria yaweze kutumika.

Aidha, fidia ya mali zilizoathiriwa na ujenzi wa miundombinu ya *DART* zimelipwa na zoezi hili litakamilika mwezi Juni, mwaka 2008. Mchakato wa ujenzi wa miundombinu umepangwa kuanza mwezi Julai, mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, sanjari na ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa *DART* maandalizi ya mpango kamambe wa usafirishaji wa Jiji la Dar es Salaam (*Transport Policy and Systems Development Master Plan*) unaandaliwa kwa kushirikiana na timu ya

wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*) utakaokamilika mwezi Juni mwaka 2008. Mpango huu utainisha kwa kina mikakati ya kuondoa kero ya msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam, kwa mpango wa muda wa kati na mpango wa muda mrefu.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza pamoja na mikakati yote hiyo lukuki ya Serikali katika kupambana na tatizo hili, je Serikali inafahamu kwamba bado tatizo la msongamano wa magari ni kubwa na kama hivyo ndivyo Serikali itakubaliana nami inahitaji mikakati zaidi?

Swali la pili, kwa kuwa bado msongamano kama nilivyosema kwamba bado upo, je Serikali haioni kwamba ni vema ikachukua juhudi ya kutengeneza barabara za kwenye mitaa hasa kati ya Kariakoo na Ilala ili baadhi ya magari kuweza kutumia barabara hizo badala ya kutumia barabara kubwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba tunalifahamu tatizo hili bado ni kubwa ndiyo maana tunaweka mikakati mbalimbali ili kupunguza tatizo hili. Mikakati hiyo ya muda mrefu pamoja na ya muda mfupi. Kwa kweli mimi ningemwomba Mheshimiwa Mbunge awe mvumilivu tutekeleze kwanza mikakati hii ambayo iliyopo ndipo tuanze mikakati mingine ambayo tunaona kwamba inaweza ikatekelezeka. Si vema kupanga mikakati mingi halafu utekelezaji ukashindikana. Naomba tu tutekeleza kwanza mikakati ambayo nimeitaja ili tuone kwamba tatizo hili litapungua kwa kiasi gani.

Kuhusu barabara za mitaa kwa kushirikiana na Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam yaani Manispaa ya Ilala, Temeke pamoja na Kinondoni, barabara za mitaa zimeanza kutengenezwa kwa mradi maalum wa *safer cities* katika mitaa mbalimbali. Kama unavyoona mwenyewe kwa watu ambao kama barabara ya Manzese zimeanza kutengenezwa na barabara zote ambazo ziko katika mitaa zimeanza kutengenezwa ili kuweka mji wetu katika hali nzuri na pia kupunguza adha hii ya msongamano katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kuniona. Nina swali moja zuri. Kwa kuwa njia tatu zinazotumika Dar es Salaam na Morogoro zinavunja kabisa Sheria za barabara kwa maana kwamba kama mnakwenda kushoto, ni kushoto tu lakini magari mengine inapaswa kutembea upande huo huo wa kushoto kwa kukutana huko ni kuvunja sheria ya wazi wazi na sijawahi kuona mahali popote duniani. Je, endapo magari yatakuwa yamepata ajali mbaya, ni nani atakayeonekana kwamba amevunja sheria?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwanza tulivyoanza kutekeleza mpango wa njia tatu, tulianza kutoa elimu kwa watumiaji wote wa njia hizo.

Pili tuliweka mkakati wa kuhakikisha kwamba wapo askari ambao wanaongoza hayo magari. Kwa hiyo, elimu ile baada ya muda ajali zimeanza kupungua na kwa sasa kama Halmashauri kama Jiji la Dar es Salaam inaongeza nguvu kwa kuomba ajira kwa askari wa barabarani ili kuongeza nguvu ili isitokee madhara kama hayo.

Katika kutatua matatizo njia mbalimbali zinatumika. Kwa hiyo, hii tuliona kwamba ni njia mojawapo ambayo inaweza kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Tusingeweza kungoja kwa njia za muda mrefu. Hii ni njia ya muda mfupi. Hapo tutakapopata ufumbuzi wa muda mrefu tutaweza kuacha njia hiyo na kutumia njia nyingine ambazo sisi tunaona kwamba zitapunguza msongamano katika Jiji letu la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Jamani kwa kweli sina budi kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri huyu kwa kweli, unajua kwa dakika kama 20 amehimili maswali mazito kabisa na hiyo TAMISEMI inakusanya Sekta zote, barabara za Dar es Salaam, masuala ya shule vijijini, walimu kukaa nyumba za nyasi, hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

Na. 134

### **Pensheni za Wanajeshi Wastaafu**

**MHE. USSI AME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa wanajeshi wastaafu hulipwa pensheni zao kila baada ya miezi sita, hali inayosababisha ukali wa maisha ambao umekuwa ni tatizo kwa wastaafu hao:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu kwa makini swali la Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wastaafu wanaolipwa na Wizara ya Fedha na Uchumi ikiwa ni pamoja na wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania hulipwa penseheni zao kila baada ya miezi sita. Aidha, Wizara ya Fedha imekuwa ikipokea malalamiko mengi juu ya utaratibu uliopo wa kuwalipa wastaafu kila baada ya miezi sita. Kufuatia malalamiko hayo, Serikali imefanya uamuzi wa kuhamishia pensheni za wastaafu kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Spika, pili kuanzia Julai, 2008 wastaafu wote wanaolipwa pensheni zao kila baada ya miezi sita, watakuwa wakilipwa pensheni zao kila mwezi kupitia akaunti zao binafsi za benki. Kwa kutumia utaratibu huu, mstaafu ataweza kuchukuwa penseheni yake kila atakapoihitaji maana itakuwa katika akaunti yake. Ili kuweza kutekeleza utaratibu huu bila ya matatizo, kuanzia tarehe 31 Januari, 2008 hadi tarehe 15 Machi, 2008, Wizara ya Fedha na Uchumi imefanya zoezi la kuwafungulia akaunti katika benki iliyo karibu wastaafu wasiokuwa na akaunti. Utaratibu wa kuwalipa wastaafu kupitia benki utakapoanza mwezi Julai, mwaka 2008, utawaondoshea matatizo wastaafu wote wanaolipwa pensheni zao kila baada ya miezi sita ikiwa ni pamoja na wanajeshi.

**MHE. USSI AME PANDU:** Ahsante Mheshimiwa Spika nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ni ukweli ulio wazi na usiofichika wanajeshi wetu hawa wakati wa kustaafu huwa wanakabiliwa na ugumu wa ukali wa maisha. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili. Je, ni kigezo gani walitumia katika kuwalipa wastaafu hao kwa muda wa miezi sita?

Pili, je Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa ni wakati muafaka kubadilisha utaratibu huo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF):** Mheshimiwa Spika, kwanza tumeshabadilisha utaratibu kuanzia Julai, wastaafu watalipwa kupitia akaunti zao za benki. Lakini la pili suala la kigezo kilichotumika katika kuwalipa wastaafu. Kigezo kikubwa katika kukokotoa mafao ya wastaafu ni mshahara wake wa mwisho na muda aliofanya kazi. Kwa hivyo, kama mwanajeshi mshahara wake wa mwisho ulikuwa ni mkubwa, muda aliofanya kazi ni mkubwa *definitely* atakuwa na pensheni kubwa zaidi kuliko wale wengine.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali lililoulizwa kuhusu wanajeshi linafanana sana na matatizo ya waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wengi wao wakiwa Tabora naomba Wizara ifafanue kama majibu haya yalikuwishapelekwa kwa njia ya elimu kwa wahusika kwa sababu sisi Wabunge tunapata tabu sana mlipowasimamishia kuwalipa pensheni zao bila wao kujua. Leo hii kila siku wanatuuliza kulikoni, tumesimamishiwa pensheni zetu, wajibuni na wasikie wenyewe kwa nini hamuwalipi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimwambie Mheshimiwa Kaboyonga kwamba wastaafu wa jeshi hawafanani kabisa na wastaafu wa Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjwa na tukamalizana nao lakini kwa wale ambao waliendelea kufanya kazi, tunatoa matangazo kupitia katika vyombo vya habari, magazeti mbalimbali juu ya utaratibu wa kupokea pensheni zao.



**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya askari hufikia wakati wao wa kustaafu wakiwa bado wanadai madai yao mbalimbali kama ya likizo, uhamisho na kadhalika. Je, madai hayo hukoma baada ya kustaafu au huingizwa kwenye pensheni zao na kama sio hivyo haioni kwamba Serikali haiwatendei haki watumishi hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madai ya askari ya likizo na mambo mengine ni madai tofauti na pensheni. Askari anapostaafu kama madai haya hajalipwa utaratibu wa kulipa madai haya utaendelea lakini hautaingizwa katika pensheni yake.

Na. 135

### **Misururu Mirefu Katika Mabenki**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wengi sasa wanaweka fedha zao benki, na wakati mwingi kunakuwa na misururu mirefu ya watu wakisubiri kupatiwa huduma katika matawi ya benki hasa *NBC*, *NMB* na *CRDB* ambapo hupoteza muda mrefu wa kazi zao, wakisubiri huduma kwenye benki hizo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba muda ni fedha, na kwamba pamoja na benki hizo kubinafsishwa bado wananchi wanayo haki ya kupatiwa huduma nzuri zisizowapotezea muda mwingi wa shughuli zao?

(b) Je, kuwepo kwa misururu mirefu katika benki hizo sio dalili kwamba biashara imekua lakini wenye benki hawako tayari kupanua nafasi za biashara na kuzingatia faida kubwa zaidi (*maximization of profit*)?

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Jerry Solomon Sumari. Kwa faida ya wananchi ambao wanaendelea kuangalia mambo yanavyoendelea hapa, Wizara hii ina Naibu Mawaziri wawili. Yule wa kwanza ni Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na huyu ni Jeremiah Solomon Sumari. Endelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na misururu kwenye baadhi ya mabanki mengi hapa nchini. Hii inatokana na sababu mbalimbali, baadhi zikiwa zifuatazo:-

1. Baada ya benki hizi kubinafsishwa na huduma mbalimbali kuboreshwa, wananchi wengi zaidi wamejiunga nazo kama wateja.
2. Mahitaji ya Wananchi wetu ya huduma za kibenki, mwamko wao katika kutumia huduma za kibenki, kama vile kuweka na kutoa fedha, huduma za mikopo na huduma za kutuma na kupokea fedha ndani na nje ya nchi yameongezeka.
3. Huduma ya malipo ya mishahara kupitia matawi ya benki mbalimbali ifikapo mwisho wa mwezi kwa wafanyakazi mbalimbali wa Serikali na sekta binafsi vilevile imeongezeka.
4. Uchache wa matawi ya mabanki hasa sehemu za wilayani na vijijini husababisha wananchi wengi wa maeneo hayo kufuata huduma hizi za kibenki katika matawi machache yaliyopo na hivyo kusababisha misongamano na misururu mirefu.
5. Wananchi kupewa fursa ya kuwa na kiwango cha chini cha kuendesha akaunti pamoja na unafuu wa gharama za huduma zinazotolewa na benki umeongeza idadi ya wateja wanaokwenda benki mara kwa mara.

(b) Mheshimiwa Spika, mabanki yaliyopo nchini yanatambua umuhimu wa kutoa huduma bora kwa wateja wao kwa sababu ya kuwepo kwa ushindani mkali kwenye sekta ya fedha. Mabanki huchukua hatua mbalimbali kuboresha huduma kwa wateja wao, na pia ili kuondoa tatizo la misururu kwenye matawi yao. Hii ni pamoja na:-

- (i) Kuendelea kufungua matawi mengi zaidi na/au kupanua na kuboresha matawi yaliyopo.
- (ii) Kuelimisha wafanyakazi wao juu ya umuhimu wa kutoa huduma bora na kwa ufanisi zaidi.
- (iii) Kuweka na kuongeza mashine maalum za kuweka na kutoa fedha katika sehemu nyingi zenye biashara.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya

Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua kwa sababu wakati Benki ya Taifa ya Biashara, *NBC*, ina binafsiswa Serikali ilitoa ahadi kwa wananchi kwamba itaanzishwa benki yao na benki hiyo ni *NMB* na wanangojea. Sasa napenda kuelewa lini *NMB* watafungua tawi pale Bumbuli, ikizingatiwa kwamba lile ni eneo la kulima chai na wakulima wale wanalipwa kila mwezi na ziko fedha nyingi ambazo haziingii katika mzunguko na kutumika? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ahadi ya Serikali kwamba katika kubinafsisha *NBC* ingefunguliwa benki ya wananchi inayoitwa *NMB*, ni kweli Septemba 97 *NBC* ilipobinafsishwa viliumbwa vyombo vitatu vya fedha. *NBC* yenyewe iliyojulikana kama *NBC 97, NBC Holding* na halafu *NMB* yenyewe ambayo mwaka wa 1995 waliuza hisa zao na kuleta wawekezaji wa kigeni. Lakini swali lake la pili kuhusu kufungua tawi la *NMB* pale kwenye jimbo lake Bumbuli, namuomba Mheshimiwa Shellukindo, tushirikiane tubanane tuangalie jinsi ambavyo tunaweza kufanya hilo kutokea. (*Makofi*).

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuwa, *NMB* Masasi ndiyo hiyo hiyo inayohudumia na Wilaya ya Nanyumbu. Je, Serikali sasa hioni haja ya kusogeza huduma wilayani Nanyumbu ili kupunguza misururu mirefu iliyoopo katika tawi la *NMB* Masasi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tawi la *NMB* lililo Masasi ndilo linalohudumia wananchi wa Nanyumbu. Na yeye vilevile kama nilivyomuahidi Mheshimiwa Shellukindo, naomba tushirikiane tuende, na tutakwenda pamoja *NMB* kutazama jinsi mipango yao ilivyowekwa tujiridhishe ni wapi ambako wamepanga kufungua matawi.

Ikiwa Nanyumbu sio moja ya sehemu ambazo wamepanga kufungua matawi basi tuone kama kuna uwezekano wa kuingizwa kwenye hii orodha ya kufungua matawi haya. Na hiyo iwahusishe Waheshimiwa Wabunge, wote tulio hapa kwasababu lengo letu kama Serikali kwa kweli, ni kuwa wananchi wasogezewe hizi huduma za fedha pale walipo. Na kazi ya Serikali hapa, inagwaje hatuwezi kuwashurutisha *NMB* kufungua, au benki yoyote kufungua matawi, lakini Serikali inafanya kazi kwa karibu sana na hizi benki na tunawahimiza na kuwaomba wafungue matawi kwa kasi inayowezekana ili hizo huduma ziwafikie wananchi.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, hivi majuzi siku ya Jumapili, Mheshimiwa waziri Mkuu, alisifia sana benki ya *Community* ya Mbinga na kuonesha nia

ya kwamba *Community bank* ni ukombozi kwa wananchi. Je, serikali ipo tayari kutenga bajeti ya mwaka huu ili kusaidia wananchi kila wilaya wafungue *Community Bank?* (*Makofi*).

**SPIKA:** Ahsante sana kwa swali zuri ambalo pengine linahusu pia na Urambo. Mheshimiwa Naibu waziri? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Viti Maalum, Devota Likokola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa waziri Mkuu, alisifia benki ya wananchi ya Mbinga na ilipaswa kusifiwa wamefanya vizuri sana. Lakini hizi ni benki za wananchi, na maombi yetu kama Serikali ni wananchi katika sehemu mbalimbali wajipange vizuri, watafute ushauri ambao unapatikana benki kuu na sisi Wizara ya Fedha tutakuwa tayari vilevile kushirikiana nao hawa wananchi katika kwanza kutoa maelezo, kutoa ufafanuzi wa jinsi hizi benki zinavyotakiwa zifunguliwe. Na pale ambapo wanakwama basi sisi serikali, sio kifedha hapana, tutakuwa tayari kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa jibu la swali lake ambalo na lenyewe ni moja kwa moja. Je, Serikali mwaka huu itatoa fedha ili kufungua tawi la benki ya wananchi Songea? Jibu ni hapana, nikimwambia ndiyo nitaongopa. Jibu ni hapana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa Urambo, hii ingawaje ningependa sana kusema, hii ni *issue* maalum kwasababu ya Mheshimiwa Spika, vilevile nakuomba Mheshimiwa Spika, uungane na wananchi wa Urambo na kwasababu wewe ni una uwezo, una *speed*, na kadhalika basi tunategemea kuwa Urambo tutakuwa na Benki ya wananchi mapema iwezekanavyo. (*Makofi/Kicheko*).

Na. 136

### **Fedha Zinazorejeshwa Hazina**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kila mwaka serikali inakuwa na Bajeti ya mapato na matumizi kulingana na hali halisi ya uchumi wetu unavyoruhusu; na kwa kuwa, inapofikia mwisho wa mwaka wa fedha, Idara za Serikali hurudisha Hazina fedha zote zilizosalia:-

- (a) Je, kwa mwaka 2006/2007 Wizara ngapi na zipi zilirejesha Hazina fedha ambazo hazikutumika?
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilirejeshwa Hazina?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007, Wizara na Idara za Serikali 50 na Mikoa 21 ilirejesha fedha ambazo hazikutumika kufikia tarehe 30 Juni, mwaka 2007. Kuzitaja Wizara na Idara zote hizo itachukua muda, lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge, ikiwa atahitaji orodha hiyo, basi tutampatia.

(b) Mheshimiwa Spika, Kiasi ambacho kilirejeshwa na Wizara, Idara za Serikali na Mikoa ni shilingi bilioni 4,511,936,127.13.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la la nyongeza. Kwa kuwa, wananchi siku zote wanadai maendeleo katika mikoa yao na vijijini. Kwa kuwa, imefikia hadi fedha hizi kurejeshwa, mabilioni. Huoni kwamba wafanyakazi ni kuleta uzembe na kutelekeza zile ahadi ambazo zinatakiwa katika maeneo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge Yahya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kwamba taratibu za matumizi za Serikali haziruhusu mwisho wa mwaka wa Serikali kuwa na kiporo cha matumizi kwa mwaka ule unaoishia tarehe 30 mwezi wa sita. Isipokuwa kwa kibali maalum cha Hazina. Kwa hiyo endapo kutakuwa kumesalia fedha ambazo hazijatumika basi kanuni na taratibu na sheria za matumizi ya fedha za Serikali zinasema kwamba lazima zile fedha zirejeshwe. Na niseme kwamba kuna sababu nyingi ambazo zinaweza kupelekea kukasalia fedha ambazo hazikutumika.

Mheshimiwa Spika, moja ni kutokamilika kwa makubaliano ya matumizi yale na kutokuwa na mikataba ya matumizi yale. Lalkini vilevile mara nyingine kwa sababu za fedha hizi za matumizi zinazopelekwa mikoani kwa mfano, zinatokana na makusanyo ya kodi mara nyingine tukio ni kwamba zinaweza hata kule kwa wale Maafisa ambao wanatakiwa watumie hawakuzipata hizi fedha muda wa kutosha kuwawezesha kuzitumia. Kwamba ni uzembe ambao unarudisha maendeleo nyuma, tungependa zote zitumike kwasababu ndizo zinakuwa kwenye bajesti. Lakini kwa sababu nilizosema tunajua dhahiri kwamba haiwezekani. Inawezekana kwamba kunatokea kwamba kweli kuna mradi ambao haukutengewa fedha, hukupata matumizi yake, lakini huo kwasababu unakuwa na matumizi mwaka unaofuata basi tunaamini kwamba hawacheleweshewi sana maendeleo yao kwa kurejesha hizi fedha Hazina kutokana na taratibu za fedha. (*Makofi*).

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Riziki, swali la nyongeza. Tutamalizia na Mheshimiwa Msindai, huwezi kumwacha kwenye mambo ya fedha ukamwacha *CRDB*. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali langu moja tu la nyongeza. Kwasababu Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba kurejeshwa kwa fedha kunatokana pengine na kwamba malengo ambayo yalipangiwa fedha zile pengine hayakukamilika au utekelezaji wa shughuli. Je, Serikali haioni kwamba kila mwaka ambapo tunatenga fedha kwa ajili ya matumizi Fulani, na matumizi yale kwamba hatukufikia malengo, ina maana kwamba kila siku badala ya kupiga hatua mbele tunarudi nyuma. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba yale malengo yaliyopangiwa fedha zile yanatekelezwa ipasavyo? (*Makofi*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati makisio haya ya bajeti yanapotengenezwa mategemeo yetu ni kwamba kwanza tutapata makusanyo ya fedha za kutosha kwaajili ya matumizi yanayohitajika kutokana na bajeti yenyewe. Lakini kama nilivyosema ni dhahiri kwamba tunajua kwamba kwasababu ya sheria na taratibu za matumizi ya Serikali na ni sheria nzuri kwamba huwezi kuweka kiporo kama nilivyosema na kuvuka mwaka wa matumizi wa Serikali, basi tunajua kwamba kutakuwa na masalio ambayo sio masalio ya kutisha, hatakidogo. Na kwamba tunaridhika zile fedha zinazorudishwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali, kwa kiasi chake ambacho ukilinganisha na matumizi mengine ya Serikali, kwa mwaka ule sio kikubwa sana, sio cha kutisha sana. Basi wananchi kwa ujumla wao hawatakuwa wamekwamishwa kwenye maendeleo yao.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, mwaka wa fedha wa Serikali unaanza tarehe moja mwezi wa saba. Na kwa kuwa, tumeshuhudia fedha nyingi za Serikali na wafadhili wetu huchelewa kutoka, mara nyingine mpaka mwezi Oktoba au mpaka Disemba. Serikali inasemaje ili kuondoa tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba ni kweli katika kipindi kile cha bajesti hapa Bungeni ni kirefu, mwaka jana kilikuwa cha siku 65 na kwamba kisheria mpaka Bunge lipitisha maombi yaliyo kwenye bajeti ndipo matumizi yaanze. Kwahiyo kuna muonekano kwamba serikali itachelewa kufanya matumizi ya zile fedha ambazo zinapitishwa kwenye bajeti. Lakini kwanza niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ana madaraka maalum kufanya matumizi ambayo ni ya dharura, lakini vilevile mara tu Waheshimiwa Wabunge, na Bunge linapopitisha ile bajeti basi matumizi yanaanza na uzoefu unaonesha

kwamba hatuchelewi sana na miradi haichelewi sana kupelekewa pesa. Ni kweli lakini kwamba mara nyingine wafadhili wanachelewa kutimiza ahadi zao za kutusaidia na ndio sababu katika kupanga bajeti zetu za siku za usoni tunaamini kwamba ni muhimu kujitahidi kwa kadiri iwezekanavyo kujitegemea katika matumizi ya Serikali. Na hivyo ndivyo tunavyojipanga pale Wizarani, na tunaamini kwamba katika miaka mitatu ijayo tutaweza kutoa taarifa kwamba sasa ndio tumejitegemea katika matumizi kwa kiasi kinachoridhisha.

Na. 137

### **Upungufu wa Maji na Umwagiliaji**

**MHE. FRED T. MPENDAZOE** aliuliza:-

Kwa kuwa, huduma ya maji inayotolewa katika Shule ya Sekondari Shinyanga kwa sasa hutolewa na Mgodu wa Almasi wa Mwadui:-

- (a) Je, Serikali inayo taarifa juu ya kero ya upungufu wa huduma ya maji katika sekondari ya Shinyanga?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kutatua kero hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Jimbo la Kishapu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tulizo nazo shule ya Sekondari ya Shinyanga ina wanafunzi wapatao 800, walimu 24 na wafanyakazi wengine 6 pamoja na familia zao. Mahitaji ya maji kwa makadirio ya matumizi ya kawaida kwa siku ni lita 83,000 ambapo kwa mwezi ni lita 2,460,000 sawa na mita za ujazo 2,460 kwa mwezi. Mgodu wa Mwadui una mkataba wa kutoa maji kwa shule ya Sekondari ya Shinyanga mita za ujazo 5,000 kwa mwezi bila malipo. Hivyo kulingana na mahitaji ya maji shuleni, kiasi cha maji kinachotolewa na mgodi kinatosha.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu imechagua vijiji 10 vitakavyoingizwa kwenye programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Maeneo yatakayonufaika ni pamoja na kijiji cha Maganzo na Shule ya Sekondari ya Shinyanga. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2008/2009 baada ya mchakato wa kupata Mhandisi mshauri kukamilika. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo wakati mchakato unaendelea.

**SPIKA:** Inaelekea hana subira. Mheshimiwa Pendazoe, swali la nyongeza?

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba kusisitiza kwamba kero ya maji katika shule ya Sekondari ya Shinyanga ipo, na mkataba wa Mwadui kupeleka maji katika shule ya sekondari ya Shinyanga ulifanya mwaka 1994 wakati shule ya Sekondari ya Shinyanga, ikiwa na wanafunzi wachache na wakazi wachache ukijumlisha na walimu. Kwahiyo ninasisitiza kwamba kero ipo na ningeshauri Serikali iweze kwenda kuhakikisha kero hiyo ya wanafunzi. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza:-

1. Kwa kuwa, wananchi wa wilaya ya Kishapu wamejenga shule za sekondari 17, ambazo nyingi zinakabiliwa na kero ya maji. Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kukabiliana na kero hii?

2. Swali la pili na la nyongeza, kwa kuwa, mradi wa *Mwadui Community Diamond Partnership* uliozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2007, una madhumuni ya kupeleka huduma za jamii kwa wananchi wanaoishi karibu na Mgoji huo wa Mwadui ikiwemo shule ya Sekondari ya Shinyanga, shule ya Sekondari ya Idukilo, Shule ya Sekondari ya Umigumbi, shule ya Sekondari ya Songwa na mji wa Maganzo. Je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu kwamba upo umuhimu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kushiriki kwa karibu katika mradi huu ili kuweza kutatua kero ya maji kwenye shule za sekondari nilizozitaja?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpendazoe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka maji katika shule za sekondari. Si shule tu za sekondari, hata shule zingine zilizoko katika maeneo hayo utaratibu wetu ni kutoa maji kwaajili ya kuzihudumia. Sasa kuhusu mkakati ambao tunao. Hatuna mkakati maalum kwaajili ya shule tu, isipokuwa tunao mkakati wa kuendeleza sekta nzima ya maji. Mkakati ambao ni wa mwaka 2006 mpaka 2015, Mkakati ambao unatekelezwa sasa na programu ya kuendeleza sekta ya maji. Lakini nikijirudisha kwenye suala la shule, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mpendazoe, kwamba wakati hii programu sasa inaendelea, mwezi huu wa saba Mshauri Mwelekezi, atakuwa tayari ameshaanza kazi. Na mojawapo ya hadidu za rejea ambazo tumempa ni kuhakikisha kwamba anakagua shule za sekondari zilizopo, taasisi zingine kama zahanati, vituo vya afya, halafu tumemshauri kwamba aangalie uwezekano wa kuingiza programu ya kuvuna maji. Katika utaratibu huu taasisi hizi za kiserikali zitapata miradi ya kuvuna maji, watajengewa matanki, halafu tunatarajia kwamba jamii nayo itaiga kutoka pale.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika mkakati mwingine sisi kiserikali tumeona kwamba ni vizuri basi katika maeneo kame ambayo yanajumlisha pia na mkoa wa Shinyanga, wilaya ya Kishapu ambako anatoka Mheshimiwa Mbunge, kwamba tuingize programu ya kujenga mabwawa. Mikoa kame yote hii ya Dodoma, Shinyanga, Tabora, Singida, tumekwisha anza, tumeshaweka utaratibu wa kujenga mabwawa. Mwaka jana tumeanza na bilioni 18.5 lakini kwa bahati mbaya zilizopatikana ni bilioni nane na nusu ndiyo maana mabwawa hayakujengwa kama tulivyotarajia.



Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaratibu upo wa kuzijali shule hizo. (*Makofi*).

Na. 138

### **Upatikanaji wa Maji Himo**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji ni uhai na yanahitajika kwa matumizi mbalimbali lakini maji hayo yanaendelea kuwa adimu kwasababu ya uharibifu wa mazingira unaofanywa na binadamu:-

(a) Je, ni kitu gani kinachoifanya Serikali kushindwa kusambaza maji kwenye mji wa Himo licha ya maagizo aliyotoa Mheshimiwa Rais, alipotembelea jimbo la Vunjo mwezi wa nane mwaka 2007?

(b) Je, ni lini Serikali itawapatia maji safi na salama wananchi wa Himo?

(c) Kwa kuwa, *KILIWATER* wamefunga na kubomoa Vilula vya maji Kata za Mwika Kaskazini na Kusini na kufanya wananchi wakose maji safi na salama ambapo ni kero kubwa kwa wananchi. Je, kwanini *KILIWATER* wanakaidi kuwarudishia wananchi vilula vya maji pamoja na kwamba wananchi wa maeneo hayo wako tayari kulipia maji kama yakipatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, alipotembelea Jimbo la Vunjo mwezi Agosti 2007, aliambiwa na wananchi kuwa kuna tatizo kubwa la maji kwenye mji wa Himo. Upungufu wa maji katika mji wa Himo unatokana na wananchi wa kijiji cha Mkolowony kukataa maji ya mtiririko ya chanzo cha Shokony kuingizwa kwenye mtandao wa Bomba katika mji wa Himo. Sababu wanazotoa za kukatalia maji hayo ni pamoja na kutaka watumie maji hayo bure kwaajili ya umwagiliaji wakati wa kiangazi, ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa madogo madogo yanayopata maji kutoka kwenye mfereji unaotoka katika chanzo cha Shokony na kuhofia vilevile kukosa maji unapotokea ukame wa muda mrefu. Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi hao waelewe umuhimu na kukubali maji ya chemchemi ya Shokony kutumiwa pia na wananchi wa mji wa Himo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo hilo inatekeleza miradi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa wananchi wa mji wa Himo wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosha. Miradi hiyo ni pamoja na uchimbaji wa kisima kirefu katika eneo la Kilema Pofu, ambacho uchimbaji wake ulikamilika mwezi Januari 2007 na

kibanda cha mashine hivi sasa kinaendelea ku jengwa. Aidha, usanifu wa mradi wa maji wenye urefu wa kilometa 6 kutoka katika mradi wa Kilema Mandaka kwa ajili ya eneo la Njia Panda umefanyika.

Ujenzi wa mradi utanza mwezi Julai 2008, kwa ushirikiano kati ya Serikali na Shirika lisilo la Kiserikali la Ujerumani linalojulikana kwa jina la Aktionskreis Ostafrika (AKO). Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2008/2009 imepanga kuchimba kisima kirefu katika mji wa Himo, eneo la Mieresini.

(c) Kampuni ya *KILIWATER* haijabomoa Vilula katika eneo la Mwika wala haijafunga maji katika Vilula bila sababu ya msingi. Vilula hivyo vilifungwa baada ya wananchi kukataa kuunda vikundi vya watumiaji maji ambavyo ndivyo vitasiamamia uendeshaji na matengenezo ya Vilula hivuyo mara vinapoharibika. Wanakijiji wa Mwika wamekataa masharti ya kuwekewa dira kwenye Vilula hivyo kutokana na mazoea ya kutumia maji bure. Aidha, baadhi ya Vilula vimefungwa kutokana na umuhimu wake kwisha baada ya watu wengi kuwa na matawi ya maji majumbani mwao. Wananchi wa Mwika watakapo kuwa tayari kufungiwa dira za maji kwenye Vilula, Kampuni ya *KILIWATER* iko tayari kurejesha huduma ya maji katika vilula hivyo ili vitoe huduma kwa kulipia.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayatoshelezi kabisa ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza yafuatayo. Mji wa Himo wanaishi watazania Mhandisi wa maji wa Wilaya aliwahi kuniambia maboma ya kupeleka maji mji wa Himo yapo pesa za quiques alipata wananchi wa Himo wako tayari kuchimba mitaro kwa ajili ya kuweka mambo hayo. Maeneo ya kutoa maji yapo ukiachanana hiyo ya Mkolowony. Je, pamoja na agizo la Rais Mheshimiwa Waziri haioni kwamba mhandisi wa maji amezembea kabisa katika suala hilo kwa kutotimiza wajibu wake na ni hatua gani atachuliwa?

Si kweli kwamba Mwika wamekaa kulipia maji na si kweli *KILIWATER* hawajabomoa vilula, sasa kwa kuwa tatizo hilo ni kubwa na wananchi wa Mwika wanaendelea kuteseka. Je, Waziri yuko tayari tukimaliza kikao hiki tuongozane tuende Mwika nikamuonyeshe vilula vilivyobomolewa na matanki ambayo hayana maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Kwikiwin, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Kimaro kwamba Kwikiwin ni miradi midogo midogo ambayo tumeidhinishia fedha kwa ajili kufanya marekebisho madogo madogo tu tena ya haraka ndiyo maana yanaitwa kwikiwin, unapofika kwenye utaratibu wa miradi mikubwa basi inabidi tutumie taratibu zingine tuingize katika program tuweze kupata fedha nyingi zaidi. Hata hivyo mimi ninavyojua ni kwamba katika mradi wa Himo huu mradi unaozungumza yapo matatizo mengine ambayo ni yakitaalam ambayo yanashughulikiwa lakini pia yapo matatizo mengine ambayo sio ya kitaalam nafikiri ingefaa tukayashughulikia mimi na Mheshimiwa Kimaro twende wote pale tuyaone kama walivyofanya kule wamemuita Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa naye amejaribu kuyarekebisharekebisha.

Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Kimaro kwamba niko tayari twende naye tushirikiane pia na Serikali ya mkoa kutatua hayo matatizo ambayo si ya utaalum wala si ya kifedha.

Lakini kuhusu suala la kwamba *KILIWATER* hawakubomoa wala hawakufunga, katika jibu la msingi nimesema si kweli kwamba hawakubomoa bila sababu za msingi sababu mojawapo ikiwa ni hiyo kwamba wamefunga ili watu waweze kulipia maji hayo kwa sababu dhana ya maji ni *god given* limeshapitwa na wakati. Lakini naomba niseme kwa kifupi tu kwamba tatizo la Himo ni kubwa na lina mambo mengi zaidi ya haya tunayozungumza tutakwenda kuyazungumza kule kule.

Na. 139

### **Vyuo Vya Wananchi (FDCs)**

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (K.n.y. MHE. TEDDY KASSELLA-BANTU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni ukweli usiopingika kuwa, vyuo vya wananchi (*FDCs*) vinahitajika sana katika Elimu hadi vijijini na vinasaidia sana lakini vinatoa vyeti ambavyo havitambuliki:-

(a) Je, ni lini Serikali itavitambua vyeti hivyo kama vile vinavyotolewa na Chuo cha *VETA*?

(b) Kwa kuwa, Elimu ya shule ya Msingi yaani darsa la saba imepitwa na wakati. Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kutoa elimu ya Sekondari kwa miaka miwili kwa watu wazima wanaoishi karibu na vyuo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba vyuo vya maendeleo ya wananchi (*FDCs*) vinahitajika na vinasaidia sana katika kuchochea maendeleo vijijini. Ni kweli vyeti vinavyotolewa na vyuo hivi havitambuliwi katika soko la ajira. Vyuo hivi vinatoa vyeti vya ushiriki kwa sababu madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kutoa mafunzo yasiyo rasmi (*Informal*) ya stadi za kazi ambazo zitamuwezesha mshiriki kujitegemea kiuchumi kwa kujijiri mwenyewe. Aidha mafunzo yanayotolewa

katika vyuo hivi yanalenga mahitaji ya wananchi ya kujiletea maendeleo katika maeneo wanayoishi hususan vijijini. Kwa mantiki hii Serikali haina utaratibu wa kuvitambua vyeti hivi kama vile vinavyotolewa na *VETA*.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwanachuo anayependa kuingia kwenye soko la ajira ni lazima afanye mtihani wa *VETA*. Hivyo vyuo vyetu vinamuwezesha mwanachuo kufanya mtihani wa *VETA* lakini anajigharimia mwenyewe.

(b)Elimu ya shule ya msingi yaani ya darasa la saba inayotolewa hapa nchini ni muhimu na haijapitwa na wakati. Elimu hii ndiyo msingi na ndiyo inayoweka mazingira mazuri na endelevu ya kumuwezesha mtu kuendelea na hatua zingine za masomo ya juu kama vile ya Sekondari, Vyuo Vya Ufundi na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeona upo umuhimu wa vyuo vyetu vya maendeleo ya wananchi (*FDCs*) kuongeza uelewa wa elimu inayotolewa kwa wanachuo na wananchi wanaoishi jirani ya vyuo kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ili kuendeleza azma hii vyuo kadhaa vya *FDCs* vimejisajili kama kama vituo vya elimu ya watu wazima ili viweze kuendesha masomo ya Sekondari ya miaka miwili. Elimu hii inaendeshwa sambamba na mafunzo ya kawaida ya stadi za kazi. Vyuo ambavyo vimeanza mfumo huu wa elimu ni Singida *FDC*, sengerema *FDC* na Malampaka *FDC*. Hatua hii itachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wanachuo katika vyuo hivi.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amekiri kwamba vyuo hivi vimeazishwa na vimeazishwa Serikali lakini vyeti vyake havitambuliki. Lakini wote tunatambua kwamba vijiji hakuna vyuo vya *VETA*. Je, kwanini Serikali haiunganishi nguvu na kuvipa hivi vyuo uwezo wa kuweza kutoa vyeti ili hawa wananchi wanapopata mafunzo waweze kutambulika na saa nyingine kuajiriwa kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, kwa vile vyuo hivi baadhi yake kama chuo cha Ruaha na tunavyuo kama Ulembwe, Ilula na chuo cha Njombe ambavyo vinaweza kubadilika kutoa vyetu vya maendeleo ya jamii na kuweza kufanya wanafunzi wengi wa fani ya maendeleo ya jamii kupata nafasi ya kusoma, je, Serikali itakuwa tayari pamoja na kwamba vyuo hivi viko huko kwenye jamii kutoa vyeti vya *VETA* lakini pia kutoa mafunzo ya cheti cha maendeleo ya jamii?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali vyuo hivi vilianzishwa katika awamu ya pili ya tatu ya elimu ya watu wazima mwaka 1975 ili kuweza kuinua kiwango cha elimu na kuwaongezea wananchi stadi ambazo zitawasaidia kujiletea maendeleo, kwa mfano ujenzi wa nyumba, kulipia mabomba pamoja na ufundi seremala.

Mheshimiwa Spika, lakini bado ili adhima ya kuleta maendeleo vijijini ipo na ndiyo sababu basi kwenye vyuo vingine tumeanzisha mfumo wa kusaidia wale wanafunzi vijana wanaotaka kuingia kwenye soko la ajira tumejisajili na *VETA* waweze kufanya mitihani ya *VETA* na wanafaulu vizuri. Kwa hiyo tutaendelea kuongeza huduma hii katika vyuo vingine.

Pili, baadhi ya vyuo vya maendeleo ya wananchi kuna mpango wa kuvibadilisha sasa hivi viweze kutoa elimu ya maendeleo ya jamii na hii tunafanya hivyo kwa sababu tunajua kwamba elimu ya maendeleo ya jamii sasa hivi inahitajika sana kutayarisha wananchi watakaochoea maendeleo ya jamii. Mimi napenda nikubaliane na Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o kwamba ni vyema hivi vyuo basi tukaingiza elimu ya ufundi lakini tujue elimu ya ufundi lakini tujue kuwa elimu ya ufundi inahitaji matayarisho makubwa maabara pamoja na karakana. Sasa ili kuendeleza hili tuna chuo kimoja ambacho tumekibakiza cha Lushoto ndiyo kitakuwa kinatoa mafunzo ya maendeleo ya jamii ngazi ya cheti pamoja na ufundi. Chuo cha Misungwi kinatoa diploma ya maendeleo ya jamii, kama tutaona kwamba kuna sababu na tukapata fedha za kutosha tunaweza tukaongeza tena vyuo kwa awamu kutegemea na uwezo wetu.

Na. 140

### **Ruzuku Kwa Dawa Bora ya Mifugo**

**MHE. GOSBERT BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo; na kwa kuwa baadhi ya dawa hizo zenye ubora wa hali ya juu, kwa mfano *dominex* na *paranex* ambazo huuwa kupe na mbung'o, hayakuwepo kwenye ruzuku ya Serikali na hivyo kuendelea kuuzwa kwa bei ya juu sana kati ya shilingi 40,000/= na 60,000/= kwa lita na kwamba wafugaji wengi hupendelea dawa hizo, lakini hawana uwezo wa kuzinunua.

Je, ni lini Serikali itasikia kilio cha wafugaji nchini na kutoa ruzuku kwa dawa za mifugo zenye ubora ikiwa ni pamoja na dawa za *dominex* na *paranex*.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia kilio cha wafugaji kuhusu mahitaji makubwa na bei kubwa ya dawa za kuogesha mifugo ili kudhibiti kupe na magonjwa wanayoeneza; Serikali kuanzia mwaka 2006/2007 ilianza kutoa ruzuku kwa dawa hizo. Katika utaratibu wa kutoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo, Serikali inalipia gharama ya asilimia 40 ambapo wafugaji wanalipa asilimia 60 ya bei ya soko la dawa. Awamu ya

kwanza ya ruzuku ilihusisha mikoa 18 ya Tanzania Bara isipokuwa mikoa ya Dar-es-Salaam, Lindi na Mtwara. Awamu ya pili inayotekelezwa mwaka huu 2007/2008 itahusisha mikoa yote ambapo jumla ya lita 54,843 za dawa aina ya pareto (*synthetic pyrethroids*) zitanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, dawa zote zinazotumika kuogeshea mifugo zina ubora uliohakikiwa na kituo cha *Tropical Pesticide research Institute (TPRI)* kilichopo Arusha kuwa zinafanya kazi kulingana na maelezo ya mtengenezaji (*dossier*).

Kabla ya kununua dawa za ruzuku, mikoa na Halmashauri za wilaya hutoa mapendekezo kwa Wizara yangu aina ya dawa ambazo wanazihitaji katika maeneo yao.

Wizara inafuata utaratibu wa zabuni kuwapata wasambazaji wa dawa hizo kwa kushirikiana na mikoa na Halmashauri za Wilaya. Kwa utaratibu huo, mkoa wa Kagera ulipendekeza kupelekewa dawa aina ya *bayticol* ambayo kiutaalamu ipo kundi moja na dawa za *dominex* na *paranex* ambazo zote zina viuatilifu vya pareto. Dawa zote tatu zina ubora na uwezo wa kuu kupe, mbug'o na wadudu wengine.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa maelezo ya utaratibu wa kutoa ruzuku ya dawa za kuiogesha mifugo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mapendekezo yatakayowasilishwa na mikoa na Halmashauri husika. Hata hivyo, kwa mwaka 2007/2008, dawa za kundi la pareto ndizo zilizopendekezwa kutumika. Mkoa wa Kagera katika awamu hii umependekeza kutumia dawa ya *flumethrin* na tayari imekwisha kuagizwa kutoka nje ya nchi. Wizara itaendelea kuwasiliana na mkoa wa Kagera mwaka ujao 2008/2009 kubaini dawa inayofaa kwa mazingira ya Kagera. (*Makofi*)

**MHE. GOSBERT BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na pia nimpongeze Mheshimiwa Wanyacha kwa majibu yake mazuri lakini wananchi wa mkoa wa Kagera hususani wilaya ya Karagwe wamekuwa wakipendelea dawa aina *dominex* na *paranex* kwa sababu ndiyo inayokidhi kutibu wadudu kupe na wengine katika maeneo hayo. Sasa je, nataka nijue Serikali iko kuanzia mwaka huu wa fedha unaokuja kutuletea dawa *dominex* na *paranex* badala ya hii nyingine aliyoisema?

Kwa kuwa wilaya ya Karagwe iko mpakani na mara nyingi imekuwa ikivamiwa na wahamiaji haramu kutoka nchi jirani za Rwanda na Uganda wakija na mifugo ambayo husababisha magonjwa pamoja na upungufu wa ardhi. Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua inatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Gosbert Blandes kwa namna anavyofuatilia hali ya mifugo katika jimbo pamoja nampongeza kwamba ni mfugaji hodari ambayo kwa kwetu sisi ni kitu kizuri. Dawa *dominex* ya *paranex* *actually* bei yake ni nafuu kuliko hata biotico tuliyopeleka. Kwa hiyo kama tutapokea maombi kama Wizara yangu itapokea maombi kwamba tuwapeleke *dominex* ama *paranex* hatutakuwa na matatizo kabisa sisi tutazipeleka hizo dawa huko mwaka ujao.

Kuhusu nchi jirani, Rwanda, Uganda na Burundi kuvamia maeneo ya nchi yetu na kuleta mifugo yao kuchungia kwetu Wizara yangu inayo habari hizo na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifungo na Uvuvi wakati akifungua baraza la wanyama pamoja na bodi ya NARCO ameagiza kwamba kama kuna watu wanaingiza ng'ombe kutoka Uganda ama nchi jirani hao ng'ombe wanatakiwa kukamatwa mara moja, wanatakiwa kukamatwa mara moja na kama sheria inaruhusu wapigwe mnada na hayo maagizo Serikali inayotoa kwa leo. Na vilevile kama kuna watu wamekuja kuvamia *Ranch* zetu na kuzichukua kama mali yao na kuanza kuwekeza hapa na *Ranch* zile ardhi sheria ya ardhi hairuhusu. Kwa hiyo, kama wapo hao watu waondoke na vyombo vya dola vinatakiwa kuwachukulia hatua mara moja.

**SPIKA:** Nadhani itabidi nimpe mfugaji Mbunge Michael Laizer swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza kwa kuwa tumepata mwaka huu na sisi tumepata dawa za ruzuku tofauti na miaka iliyopita lakini dawa ni ndogo haitoshelezi. Je, Serikali iko tayari kuongeza bajeti ya mwaka 2008/2009 ili dawa itosheleze katika maeneo yote ya wafugaji pamoja na chanjo rythief ambayo haipatikani tunanunua kwa bei ya juu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza mwaka huu tulitarajia kwamba tuliomba tutengewe bilioni tano ili tuweze kukidhi kutoa hizi dawa za ruzuku lakini bilioni moja na milioni 200 na kwa hiyo kwa kweli hatutaweza kutosheleza mahitaji. Lakini kama Serikali kama Wizara yangu itapatiwa bajeti ya kutosha hatutakuwa na shida ya kununua dawa zaidi na kuwaongezea na kuzipeleka mikoani ama Halmashauri kama Mheshimiwa Laizer alivyoshauri naomba sana Wizara ya Fedha basi itutengee bajeti ya kutosha. (*Makofi*)

Na. 141

### **Matumizi ya Mbolea ya SA**

**MHE. VITA R. M. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Namtumbo wamekuwa wakilalamika kitendo cha kuondolewa kwa mbolea aina ya SA na badala yake watumie aina ya NPK ambayo imesababisha kupungua kwa mavuno ya mazao yao kwa kuamini kuwa mbolea ya NPK hairutubishi ardhi kama ilivyo kwa mbolea ya SA:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid M. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba mbolea aina ya SA (*Sulphate of Ammonia*) ambayo hutumiwa wakati wa kukuzia nafaka haijakataza na Serikali mahali popote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali ombi la Mheshimiwa Mbunge, kufanya utafiti shirikishi kuhusu matumizi ya mbolea aina ya SA kwa lengo la kuchunguza malalamiko ya wakulima wa Namtumbo na kutoa elimu zaidi kwa wadau juu ya aina na viwango sahihi vya matumizi ya mbolea za kilimo.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mafupi na mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa Ruvuma wakulima wanasema walikatazwa kutumia SA na haipo katika mgao wa ruzuku kama Serikali nasema haijakatazwa kutumika je, ni kiasi gani mwaka jana kilipelekwa Mkoani Ruvuma? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba hakuna kiasi cha Sulphate of Ammonia kilichopelekwa Mkoani Ruvuma hata mkoa mwingine mwaka jana. Kwanza niseme *Sulphate of Ammonia* virutubisho vyake ni *Sulphate* na *Nitrogen* ambayo *Sulphate* na *Nitrogen* ambayo *Sulphate* inaongeza tindikali kwenye udongo kwa hiyo huharibu mashamba, kulinganisha na *Urea*, *Urea* haina madhara makubwa kama *Sulphate of Ammonia*. Kwa hiyo, badala ya kutumia *Sulphate of Ammonia* kwenye mashamba ya mahindi tunatumia *Urea* na badala ya kutumia *Sulphate of Ammonia* kwenye tumbaku kwa sababu ina *Nitrogen* nyingi na *Nitrogen* inaharibu majani ya tumbaku tunatumia NPK. (*Makofi*)

Na. 142

### **Kuboresha Pembejeo za Kilimo kwa Wakulima**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kuboresha kilimo hapa nchini kwa kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea mbegu na kadhhalika:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa wakala waliopewa kazi ya kusambaza pembejeo hizo wengi wao wako mikoani na wilayani na hivyo kushindwa kuwafikishia wakulima huduma hizo kirahisi?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa mpaka sasa wapo wakulima wengi sana ambao hawajafaidika kabisa na ruzuku hiyo ya mbolea na mbegu?

(c) Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kupeleka mbolea na mbegu moja kwa moja kwenye vyama vya ushirika ili wakulima wapate huduma hiyo kirahisi na kwa wakati?



**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua kuwa mawakala waliopewa kazi ya kusambaza pembejeo zenye ruzuku wengi wao wako katika miji mikuu ya Mikoa na Wilaya na hivyo pembejeo haziwafikii wakulima kwa urahisi. Ili kumpunguzia mkulima gharama na pia kuhakikisha pembejeo zinafika vijijini wakati wote, Serikali imeanza kubaini wauza pembejeo wa vijijini (*rural agro-dealers*) ambao watapewa mafunzo ya biashara ya pembejeo na kupewa mikopo na mablenki kwa ajili ya kununulia pembejeo na kuzifikisha vijijini. Hii itakwenda sambamba na kutoa ruzuku ya pembejeo moja kwa moja kwa wakulima kwa kutumia vocha.

(b) Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba pembejeo zenye ruzuku hususan mbolea na mbegu bora zinawanufaisha wakulima walio wengi. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara itakuwa vigumu sana kutoa ruzuku ya pembejeo kukidhi mahitaji ya wakulima wote nchini.

Kwa hiyo, natoa wito kwa viongozi wote wilayani na vijijini kuwa makini katika kubaini wakulima wenye uwezo mdogo wa kununua pembejeo wakati mpango wa vocha utakapoanza mwaka huu wa 2008/2009.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba wakati wa kubaini wauza pembejeo wa vijijini, vyama vya ushirika imara navyo vijumuishwe katika utaratibu huu utakaoanzishwa mwaka huu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa ni dhahiri kwamba vyama vya ushirika ni kweli vinafanyakazi nzuri na vilikuwa vinasaidia sana wakulima kupata pembejeo kwa kirahisi na kwa karibu. Je, Serikali ina mpango sasa wa kufufua vyama vya ushirika maeneo yote ya wakulima ili kuhakikisha kwamba utakapoanza huu mpango aliosema wakulima wote wanapata huduma hiyo kwa haraka na kwa urahisi? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Urambo wakulima wake wameathirikasana na tatizo la kukosa pembejeo hizi kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri sasa hivi atatuhakikishia kwamba mwaka huu wakulima wa Urambo watapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba wanapata pembejeo hizo kwa muda unaostahili na kwa bei iliyopangwa na Serikali? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili swali kama unavyoona ni muhimu sana. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubali kwamba kwa sasa hivi vyama vya ushirika ambavyo vina uhai na vinavyoweza kufanya hii kazi ni 3000 hapa nchini kwa sasa hivi.

Pili, katika suala la *modernization* ya ushirika ili vyama hivi viweze kufanyakazi kama unavyosema tayari tulishaanzisha mchakato wa uchaguzi na vyama vya ushirika vilivyo vingi tayari vina viongozi wapya na vyama vingine kama unavyoona kwenye vyama vya korosho tumeshapeleka watendaji ambao wamewezesha kununua korosho kwa mfumo wa stakabadhi ya mazao. Kwa hiyo, hivyo ndivyo tunavyoimarisha vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na kufutiwa madeni. Walishafutiwa madeni na madeni mengine yameshalipwa kule kwenye zile benki kwa hiyo, vyama vingine vinakopesheka kwa mfano *SHIRECU, NCU* pamoja na vyama vya wakulima wa korosho. La pili, kuhusu suala la kufikisha mbolea kwa bei na kwa kiwango kinachotakiwa Urambo nikiri kabisa kwamba Mikoa ndiyo kwenye Kamati zake za Mikoa ndiyo inayohusika kupeleka mbolea kwenye Wilaya zinazohusika. Sisi taifa tunapanga mbolea kutokana na mazao yale ambayo tulishayasema tumbaku na mahindi. Lakini kule Mikoani ndiyo wanaohakikisha kwamba wanapeleka mbolea kutokana na mahitaji ya Wilaya husika. Nawaomba Viongozi wa Mkoa na Kamati za mbolea wahakikishe kwamba Wilaya ya Urambo inapewa kipaumbele kama Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Magdalena Sakaya walivyoniomba. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonekana Serikali haina uwezo wa kuweza kupeleka mbolea kila mahali, lakini inaendelea kupeleka mbolea kidogo kidogo na kuharibu ardhi kwa sababu ardhi ukishaiwekea mbolea tena huwezi ukaendelea kulima bila mbolea. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vizuri sasa Serikali ikaamua kupeleka mbolea ya kutosha katika eneo moja tu kuliko kupeleka kidogo kidogo katika sehemu mbalimbali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kusema kwamba mbolea haiharibu ardhi, mbolea inarutubisha, mbolea ina virutubisho. Lakini usipoweka kwa viwango vinavyotakiwa ni kweli itaharibu ardhi yako. Pili, mbolea ya kutosha kama nilivyosema kwamba mahitaji ya nchi kwa mbolea ni tani 385,000 kwa nchi nzima Serikali haina uwezo wa kutoa mbolea ya ruzuku ya tani 385,000. Tunachoweza ni kupeleka kwenye *strategic areas* ili iweze kuleta *impact*. Kwa mfano, mbolea tumepeleka kwenye *Southern highlands* kwa mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa ili tuweze kupata mahindi mengi kwa ajili ya kuhifadhi *food security* ya nchi. Kwa hiyo, tutaendelea kupeleka mbolea maeneo ya *strategic areas* ili tuweze kupata *impact*, matokeo yanayoonekana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kidogo kwa sababu tulianza na matangazo na kuwasilishwa hati. Kwa hiyo, nadhani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tutaweza pia kuyafikia maswali ya Wizara ya Miundombinu. Swali linalofuata ni la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi linaulizwa na Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko wa Muhambwe.

## Hali ya Usalama – Wananchi – Kibondo

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, hali ya usalama wa wananchi wa Kibondo si ya kuaminika kutokana na uvamizi wa mara kwa mara wa majambazi wanaotoka nje ya mipaka yetu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha ulinzi mpakani ili kupunguza uingizaji holela wa watu toka nchi jirani ya Burundi?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya Askari wa Jeshi la Polisi Wilayani Kibondo ili kukabiliana na hali ya ujambazi uliokithiri katika Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha ulinzi na usalama mipakani ili kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu na wahalifu kutoka nje na ndani ya nchi. Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali katika kuimarisha usalama wa nchi ukiwemo wa wananchi wa Kibondo.

Mheshimiwa Spika, haitakuwa vizuri kuelezea kwa undani mikakati inayotekelezwa na Serikali katika kudhibiti ujambazi mipakani. Hata hivyo, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba mikakati ya jumla ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuimarisha operesheni za kudumu dhidi ya majambazi na wahalifu wengine.
- (ii) Kuimarisha doria na misako ya mara kwa mara na kuimarisha mawasiliano baina ya Jeshi la Polisi na raia kupitia polisi jamii.
- (iii) Kufanya tathimini ya uhalifu (*Crime threat analysis*) mara kwa mara kwa lengo la kubaini mwelekeo wa uhalifu na maeneo tete na kisha kuelekeza nguvu za ziada katika maeneo hayo.
- (iv) Kufanya zoezi la kutambua na kuhakiki wahamiaji haramu ili taratibu za kuwarudisha makwao zifanyike.
- (v) Kufanya mikutano ya ujirani mwema kati ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kibondo na Viongozi wa Wilaya za nchi jirani zinazopakana na Wilaya ya Kibondo ili kubadilishana taarifa za uhalifu.

(vi) Kuimarisha ushirikiano kati ya Polisi na idara nyingine za Serikali hususan vyombo vya dola kwa lengo la kufanya operesheni za pamoja za kubadilishana taarifa za uhalifu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti vema ujambazi katika Wilaya ya Kibondo, Jeshi la Polisi lina kikosi maalum cha askari waliopatiwa mafunzo maalum ambao wanashirikiana na Askari Polisi Wilayani Kibondo kuendesha na operesheni maalum ya kudhibiti ujambazi wilayani humo. Aidha, tutaendelea kuongeza idadi ya askari katika vituo vyote vya Polisi Wilayani Kibondo na Mkoa kwa ujumla kulingana na mahitaji.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa lakini ni kwamba hali ilivyo inaonyesha wazi kwamba silaha zinazotumiwa na adui ni kubwa zaidi ya silaha ambazo Jeshi letu la Polisi wanazo pale. Kwa mfano, adui anatumia *light machine gun* pamoja na *woes gun* hali ambayo Jeshi letu la Polisi hawana silaha hizo na kusababisha wakati mwingine Polisi kushindwa kupambana na maadui au mauaji yanayotokea.

Je, Naibu Waziri anaweza kunieleza kuna mkakati gani wa kuweka silaha ambazo zitakuwa na uwezo wa kupambana na nguvu za adui? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, anayoyasema ni kweli na Serikali inafahamu aina ya silaha ambazo zinatumiwa na majambazi. Lakini pia naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali imekuwa inafanya operesheni mbalimbali katika maeneo ya Kibondo na katika maeneo mengine ya mipakani ambako wanatoka wahalifu hawa na mara nyingi tumekuwa tunakamata silaha ambazo wanakuwa nazo.

Kitu ambacho nataka kusema ni kwamba tumekuwa na operesheni maalum na yeye atakubali kwamba katika mapori ya Uvinza, Kanembwa, Mtendeli na Kumhasha ambayo ni katika maeneo ya Kibondo tumefanya kazi nzuri ya kusafisha. Pia tumeweka utaratibu maalum ambapo Askari wamekuwa wanasindikiza magari ya abiria na mizigo kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo.

Hesabu au tarakimu kwa sasa zinatonyesha kwamba hali ya uhalifu inapungua ukilinganisha na miaka mitatu, minne iliyopita. Hakika bado ujambazi upo, lakini pia na jitihada tunazozifanya ni kubwa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge asiamini kwamba silaha walizo nazo ni kubwa kuliko tulizo nazo sisi, isipokuwa kitu ninachosema ni kwamba hatuwezi kuweka bayana ni silaha za aina gani tulizonazo au mikakati gani tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

## Ubovu wa Barabara Rukwa

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Matai – Mwimbi hadi Ilonga imekuwa ikishughulikiwa na *TANROADS* Mkoa wa Rukwa na kwa kuwa kuna maeneo korofi kama ya Kalepula na Mombo ambayo hayajakarabatiwa vema:-

- (a) Je, ni lini maeneo hayo yatakarabatiwa vizuri?
- (b) Je, ni kwanini *TANROADS* Mkoa imechukua muda mrefu kupitisha uamuzi wa kuunganisha barabara hiyo toka Ndalambo – Kakosi – Kapele hadi Ilonga ili kurahisisha usafiri wa kufika Kasanga?
- (c) Je, ni lini barabara ya Laela – Njia Panda hadi Miumbi itaboreshwa ili ipitike vema wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya barabara yaliyotajwa ya Kalepula na Mombo pamoja na Laela – Njia Panda hadi Mwimbi yapo katika barabara mbili za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoani Rukwa kama ifuatavyo:-

- (i) Maeneo ya Kalepula, Mombo na Ilonga yapo katika barabara ya Mkoa ya Njiapanda ya Kalepula – Mambwenkoswe (Ilonga) yenye urefu wa kilometa 60.
- (ii) Sehemu za Matai – Mwimbi na Laela – Njiapanda hadi Mwimbi zipo katika barabara ya Mkoa ya Laela – Mwimbi Kizombwe (Matai) yenye urefu wa kilometa 92.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka ili kuzifanyia matengenezo na ukarabati barabara za Mkoa za Njiapanda ya Kalepula-Mambwenkoswe (Ilonga) na Laela - Mwimbi – Kizombwe Matai ili kuziwezesha kupitika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, barabara ya Njia Panda ya Kalepula – Mambwenkoswe (Ilonga) imetengewa jumla ya shilingi milioni 211.082 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi, matengenezo ya madaraja, ujenzi wa *drift* ya Ndolwa na ukarabati. Hadi sasa matengenezo ya sehemu korofi na ukarabati katika barabara hii yamefanyika katika maeneo ya Kalembe, Kasusu na Ilonga ambayo yalikuwa mabaya zaidi. Maeneo yaliyobaki ikiwa ni pamoja na Kalepula na Mombo yamefanyiwa matengenezo ya

kawaida. Maeneo haya yataendelea kufanyiwa matengenezo na ukarabati katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzitengea fedha za matengenezo na ukarabati kila mwaka barabara hizi ili ziweze kuboreshwa na kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kakozi – Ilonga (km.50.40) barabara hiyo ni ya Wilaya inayohudumiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. *TANROADS* kwa sasa hawawezi kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa sababu hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na TAMISEMI ili kujua mipango yao ya matengenezo na maendeleo ya barabara hiyo.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Barabara zetu katika Mkoa wa Rukwa nyingi ni za udongo tu na mvua zilizo katika Mkoa wa Rukwa ni nyingi kiasi ambacho zinaharibu barabara zetu. Je, isingekuwa vizuri Wizara ikaona ni jinsi gani ya kuongeza Bajeti ya Mkoa huu wa Rukwa kwa sababu barabara zote baada ya mvua huwa zinaharibika na zinahitaji fedha kwa ajili ya matengenezo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna ahadi ambazo zinatolewa na viongozi wa Serikali na hizi ahadi zinapotekelzwa huwa zinaongeza imani ya wananchi wa Serikali yao. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba barabara ya Sumbawanga kwenda Matai na Kasanga kuwa itajengwa kwa lami. Je, Wizara hii imeshafikia kiwango gani kuhakikisha kwamba ahadi ya Rais inatekelezwa kama alivyoahidi ili Serikali ipate imani ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mkoa wa Rukwa ni Mkoa ambao sisi kama Wizara ya Miundombinu na Serikali kwa ujumla tunaiwekea kipaumbele cha kuongeza fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake kutokana na ukweli kwamba Mkoa huo ni kati ya Mikoa ambayo ilikuwa nyuma sana kimiundombinu.

Sasa alilolipendekeza kwamba tuendelee kuongeza Bajeti kwa ajili ya kutengeneza Barabara za Mkoa huo zitoke kwenye udongo angalau nyingi zifike kwenye changarawe tumelizingatia na tutakuwa tunafanya hivyo mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Rais ya kujenga barabara Sumbawanga-Matai –Kasanga ni ahadi ambayo ni muhimu kwa sababu bandari ile na barabara ile ni muhimu sana. *(Makofi)*

Lakini ukweli ni kwamba Bajeti ya Serikali ndiyo imekuwa kikwazo. Lakini kwa sababu ni ahadi bado tunaangalia katika miaka ijayo tuendelee kuiboresha kwa sasa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe wakati tunajenga uwezo wa Serikali wa kujenga baadaye barabara hiyo kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Kakozi-Kapele-Kasinde-Ilonga-Matai hadi Kasanga si muhimu tu kwa kurahisisha usafiri katika Mkoa wa Mbeya na Rukwa bali pia ni muhimu kwa ulinzi wa doria kwenye mpaka wa nchi yetu na Zambia na kwa kuwa hapo tarehe 20/2/2008, Wizara ya Miundombinu iliagiza *TANROADS* kufanya tathmini na kutoa makadirio ya ujenzi wa barabara hiyo ya kutoka Kakozi hadi Ilonga na *TANROADS* wakatoa makadirio ya Sh. 1.4bn/= na kusema kwamba watajitahidi kwa msimu ama mwaka wa fedha wa 2008/2009 barabara hii ijengwe. Je, sasa maadam hayo makadirio yamekwishawekwa Wizara haioni umuhimu wa kuanza kuitengeneza hiyo barabara ili kuweza kurahisisha usafiri pamoja na ulinzi wa doria sehemu hii?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, hapa kuna mambo mawili, kwanza kuna suala la barabara ya Kakozi kwenda Ilonga ambayo kwa sasa kwa kweli ni ya Wilaya. Iko chini ya TAMISEMI iweze yenyewe kupandishwa iunganishwe na ile ya Mkoa ambayo ipo kwenye Mkoa wa Rukwa kuelekea mpaka kule Ziwani.

Sasa kama tulivyokuwa tukijibu hapa kwa kweli suala la kupandisha barabara hizi mchakato huo bado ni mrefu na haujakamilika na kwa kweli kwa mwaka huu unaokuja wa fedha hatutaweza kuweka fedha za bajeti ya barabara zile zilizopendekezwa kupandishwa kwa sababu mchakato ule bado. Lakini ni kweli kwamba *TANROADS* walifanya makadirio pamoja na kipande hiki ambacho kipo chini ya Wilaya. Sasa itategemea Bajeti itakayokuwa imeidhinishwa na Serikali kama zitakuwa zimeidhinishwa hizi fedha basi barabara hiyo itaunganishwa itengenezwe wakati tunangojea sehemu hii ya Wilaya kupandishwa daraja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana pamoja na kumpa pole Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuondokewa na Waziri wake lakini naomba swali langu namba 145 lipatiwe majibu. (*Kicheko*)

Na. 145

### **Kutengeneza Barabara ya Tingi – Kipatimu**

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA** aliuliza:-

- (a) Je, nini hatma ya barabara ya Tingi – Kipatimu ambayo Mkandarasi wake amehamisha vyombo na wafanyakazi wake, wakati barabara hiyo bado haijakamilika?
- (b) Kwa kuwa eneo la Tingi – Kipatimu ni la milima mikali. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mpanda bila kujali pole yake lakini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tingi – Kipatimu yenye urefu wa kilometa 50 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Lindi.

Barabara hii ni miongoni mwa barabara nne za Mkoa wa Lindi zilizopangwa kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa lengo la kukarabati jumla ya kilometa 200 tangu mwaka wa fedha 2003/2004 kwa ufadhili kutoka nje. Kutokana na kuchelewa kukamilisha taratibu za manunuzi, baada ya kupata bei za zabuni kutoka kwa Makandarasi mwaka 2005/2006, ilionyesha bayana kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa kinaweza kukarabati kilometa 114 tu. Kutokana na hali hiyo, barabara hii ambayo awali ilipangiwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe kilometa 50, sasa itafanyiwa ukarabati kwa kilometa 17 tu, kuanzia Chumo hadi Kipatimu pamoja na daraja la Mingumbi (Mto wa Liomanga).

Mkandarasi aliyepata zabuni ni *M/S DB Shapriya & Co. Ltd* wa Dar es Salaam, ambaye alipaswa kujenga kipande cha barabara cha urefu wa kilometa 17 pamoja na daraja la Mingumbi kwa gharama ya Sh. 1,132,664,000/=. Kazi hii ilipangwa itekelezwe kwa muda wa miezi kumi na nne kuanzia tarehe 29/10/2006 na kukamilika ifikapo tarehe 22/12/2007. Hata hivyo, Mkandarasi alichelewa kuanza kazi hiyo, badala yake alianza kazi mwezi Novemba 2006. Ilipofika tarehe 8 Desemba 2007, Mkandarasi huyu aliondoka na kuhamisha vifaa vya kazi eneo la kazi bila taarifa ya Mhandisi Mshauri wala mwajiri (*TANROADS*). *TANROADS* inalishughulikia suala hili kufuatana na vipengele vilivyopo katika mkataba wa kazi uliokuwa umesainiwa kati ya Mkandarasi *M/S DB Shapriya* na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mhandisi Mshauri anaandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi mwingine atakayekamilisha kazi ya ukarabati wa kilometa 17 zilizopangwa kujengwa katika barabara ya Tingi hadi Kipatimu. Zabuni kwa ajili ya kazi hiyo zinataraajiwa kutangazwa mwezi Mei, 2008 na Mkandarasi mpya ataanza kazi ifikapo mwezi Agosti, 2008.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Tingi – Kipatimu inapita katika maeneo ya milima mikali hivyo kustahili kujengwa kwa kiwango cha lami ili iweze kudumu. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali kwa sasa, Serikali haina uwezo wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Wizara yangu itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili ipitike muda wote bila matatizo.



**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa barabara ya Tingi-Kipatimu watu wengi waliwekewa alama ya X kwamba wasiendeleze kujenga maeneo ambayo barabara inapita. Sasa je, malipo yao yapo kwenye msimamo gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara ya Tingi-Kipatimu haiwezekaniki mpaka tujue barabara ya Ndundu-Somanga. Sasa naomba kuuliza, je, Ndundu-Somanga ipo kwenye hali gani? Pia, je, ile changarawe iliyobakia pale kwenye Daraja la Mkapa niende kwa nani nikamwombe ili nikatumie katika barabara inayotoka Nyamwage kwenda Kipatimu? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, sijui kama unaruhusu maswali matatu aliyouliza Mheshimiwa Mpanda lakini nikianza kujibu swali lake la kwanza la barabara ya Tingi-Kipatimu kwamba kulikuwa na X. Ni kweli na kama ambavyo tumekuwa tukizungumza naye, pamoja tunapokagua barabara au kupitia kwenye Jimbo lake ni kwamba kuna wananchi wengine ambao walistahili na wengine hawakustahili bado tathmini ilikuwa inaendelea kuangalia kwamba wanaostahili waweze kulipwa na wale ambao hawastahili kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya barabara basi watajulishwa. Mchakato huo utakamilika hivi karibuni na mimi na yeye tutaendelea kufuatilia ili tuweze kujua hatma ya hao wananchi. Kuhusu barabara ya Ndundu-Somanga kama ambavyo tumeshajibu hapa ni kwamba, tunategemea kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Nne tutakuwa tumekubaliana na tumewekeana sahihi mkataba na Mkandarasi ambaye tumezungumza naye ili kazi hiyo iweze kuanza haraka iwezekanavyo. Sasa hii ya mchanga naomba amwone *Regional Manager* wa sehemu hii ili aone kama anaweza kupata mchanga huo. (*Makofi*)

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo haya ya barabara yanafanana kabisa na matatizo kabisa ya barabara za *Old Shinyanga-Saarawe* hasa katika Mbuga ya Manigana kuna Mkandarasi anafanya kazi chini ya kiwango na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri nilimwomba na aliahidi kwenye Bunge lako hili Tukufu kuzuru barabara za Jimbo la Solwa ili nikamwonyeshe matatizo hayo yanayozikabili barabara zetu, namwomba tena kwa mara ya pili. Je, ni lini na siku gani na mwezi gani tutakwenda naye pamoja nikamwonyeshe ili tuondoe matatizo ya barabara ya Jimbo la Solwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli matatizo ya Mkandarasi katika barabara hiyo ya *Old Shinyanga-Saarawe* alishanieleza na mimi nimemwagiza Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Shinyanga anipe majibu. Hata hivyo, ombi lake na mimi na yeye kwenda kukagua barabara za Jimbo la Solwa nimelizingatia na namwomba tuone namna ya kupanga ili tukague Jimbo lake kabla ya Bunge la Bajeti. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita kabisa tumebakiza swali moja tutalipangia wakati mwingine. Taarifa, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesafiri kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya mazishi ya Marehemu Ditopile na ameniachia ujumbe kwamba atakayeshikilia uongozi wa shughuli za Serikali humu Bungeni ni Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais masuala ya Muungano. Namwona ameketi kiti ambacho sicho, lakini inaeleweka maana yake kiti hicho kingine nadhani ni kigumu kidogo. (*Kicheko*)

Basi tunamwombea kheri mpaka kesho atakaporejea Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamtakia aweze kushika mambo ya shughuli za Serikali kwa kipindi hicho. (*Makofi*)

Kuhusu wageni, nafurahi kutangaza wageni wafuatao ambao wametufikia. Kuna wageni wa Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama ifuatavyo:-

Bwana Gabriel Mbunda, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Mambo ya Ndi, yule pale, ahsante sana. Bwana Paul Chagonja, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Polisi, yule pale. Bwana Lucas Mwita, Naibu Kamishna Magereza, yule pale na *uniform* kabisa. Bwana Ali Lyangwike, Naibu Kamishna Zimamoto na Uokoaji, yule pale. Bwana Cathbert Sambaligula, Mkurugenzi Msaidizi Uhamiaji. Bwana Magnus Ulungi, Mkurugenzi Msaidizi Uhamiaji, yule pale. Bwana Charles Nzuki, Mkurugenzi Msaidizi Wakimbizi na Bibi Aneth Laurent, Mrakibu wa Magereza, yule pale. (*Makofi*)

Karibuni sana na kila mara tunafurahi mnapokuja Watendaji kuona shughuli za Bunge karibuni sana. Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye yuko safarini kule Kisiwa cha Jessey, Uingereza.

**WABUNGE FULANI:** Aaahaa!!

**SPIKA:** Ndiyo, kuna ajabu gani sasa? Kuna ujumbe umekwenda kwa ajili ya Mabunge ya Madola....

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**SPIKA:** Wapo wengi tu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. ni ujumbe wetu tu wa kawaida ila safari hii inafanyika pale Kisiwa cha Jessey. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Anna Makinda ambaye ni Naibu Spika na Mbunge wa Njombe Kusini ni Wajumbe wa Bodi ya Tuitangage *SACCOS Limited*, wapo kumi na wawili sitawataja wote, wanaongozwa na Mheshimiwa Marcus John Ingole, ambaye ni Mwenyekiti, aha. Wale pale tayari wamesimama, pamoja na Makamu Mwenyekiti Richard Mongule, apunge mkono tumwone. Halafu Ndugu Victor Luvunga Afisa Kilimo, Tarafa ya Igumile, karibuni sana wageni wetu kutoka Njombe. Tunafurahi sana kuwakaribisha hapa. Mimi binafsi napenda kuwafahamisha kwamba Naibu Spika ananisaidia vizuri sana na naona ni baraka kufanya naye kazi. Kwa hiyo, mumtunze huko Njombe. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o ambao ni Dr. Regina Gregory kutoka Heidelberg University, Ujerumani, yule pale na Mary White Cuber - Team leader mradi wa CBHIGTZ na mume wake Yun Pien Cuber, mume hakuja. *Welcome to Tanzania, we are always happy to see friends from abroad to be with us in development programmes of our people, You are most welcome. (Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa ni Umoja wa wanachuo kutoka Vyuo Vikuu vilivyopo hapa Dodoma watokao Wilaya ya Kwimba. Jumla yao ni 35, lakini wanaongozwa na Ndugu Emmanuel Kasalala. Naomba apunge mkono, yule pale ahsante sana. Tunawashukuru sana, kaibuni sana tunawatakia mema katika masomo. Wapo Wajumbe wa MUWEDA, wapo 30 kutoka Mzumbe Morogoro. Wageni wa Mzumbe naona hawakutokea. Wapo wanafunzi 50 kutoka shule ya Kiwanja cha Ndege, leo hawapo, nadhani wametoka. Taarifa ya vikao. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Na. 231, saa saba mchana, Jengo la Utawala. Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati saa tano mara baada ya matangazo haya, asubuhi hii katika ukumbi Na. 428.

Waheshimiwa Wabunge nawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi (*Steering Committee*) ya Bunge, tukutane saa saba na nusu ofisini kwangu katika Ukumbi wa mikutano pale Ofisi ya Spika kwa kikao kifupi sana.

Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, ameniomba nitangaze kwamba Wabunge wote kutoka Mkoa wa Kilimanjaro wakutane leo saa saba mchana chumba Na. 432, katika jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tunayo timu ya mchezo wa *pool* na nimeletewa taarifa hapa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami ambaye ni mmoja wa kiongozi wa mchezo wa muda wa *pool* kwamba kutakuwa na mazoezi ya wachezaji wote wa *pool* ili kuzingatia kwamba mwezi Juni, 2008, kuna timu zitakazokuja kushindana na Waheshimiwa Wabunge kwa mchezo huo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa George Simbachawene kumbe ndiyo mwalimu na kocha. Kwa hiyo, wanawaomba muanze mazoezi, na kwamba muwaone Waheshimiwa Wabunge hao Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa George Simbachawene ili kuweza kupata nafasi ya kukutana na kuyaweka mambo sawa.

Waheshimiwa Wabunge, awali ilionekana kwamba tungeweza kuwa na uchaguzi wa Waheshimiwa Wabunge wale watakaolingia katika vyombo vingine kama vile Mabunge mengine ya Kanda na kadhalika.

Sasa kwa mujibu wa Nyongeza ya Tano, Kanuni za Bunge, Kanuni ya 4(2) kuna muda uliowekwa baina ya kutangazwa nafasi na kufanyika uchaguzi, siku saba zinaishia

leo. Kwa hiyo, chaguzi zetu sasa zitakuwa kesho, kwa ratiba ilivyokuwa inaonekana pengine ingeweza kuwa leo jioni lakini itakuwa ni kinyume cha Kanuni. Kwa hiyo, chaguzi hizo zitafanyika kesho. Ahsante sana. Sasa tunaendelea na shughuli inayofuata. Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 (*The Electricit Bill, 2007*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya wachangiaji kumi na moja, na kulingana na jinsi walivyoniletea maombi pengine wana shughuli nyingine. Basi nitawataja kwa mpangilio ambao pengine siyo ulivyo katika tangazo, lakini ninazo sababu za kufanya hivyo. Tutaanza na Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle Shibuda, halafu Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa, Clemence Lyamba, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Anna Killango Malecela na hatimaye tutamalizia na Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwenye saa saba kasorobo hivi. Kwa sababu tutaufunga mjadala yaani wachangiaji toka kwenye *floor* mwisho ni saa 7.00 mchana ili Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na timu yake waweze kujiandaa, na naona Naibu Waziri hayupo. Basi Mheshimiwa Waziri ataanza ku-*wind up* saa 11.00 jioni. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo wakati huo huo Mheshimiwa Magalle Shibuda ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya awali kuchangia Muswada huu wa umeme. Baada ya shukrani hizo nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote walioshiriki katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa sababu Muswada huu ulikuwa na utata tangu ulivyoletwa, lakini inaonekana wameufanyia ukarabati wa kutosha, na hatimaye Muswada huu umeonyesha kuwapendeza Waheshimiwa Wabunge wengi. Hivyo ni matumaini yangu kwamba utaungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na mimi kabla sijaanza kuchangia niunge mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja nikiwa na matumaini makubwa kabisa kwamba Muswada huu utazaa matunda mengi katika kuboresha huduma ya umeme katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeunga mkono Muswada huu nikiwa na sababu za kutosha. Kwanza, nina matumaini makubwa sana kwamba endapo tukiupitisha utaleta uboreshaji katika Shirika letu la *TANESCO* kwa sababu ya ushindani. Biashara ukitaka ichanganye ni ushindani, na si ushindani tu. Vilevile nina uhakika kabisa watumishi wetu endapo

walikuwa wanalegalega, sasa hivi ni wakati wao mzuri kabisa kufanya kazi zao ipasavyo ili waweze kwenda na soko la uwekezaji kwa Mashirika ambayo yataingia baada ya kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, vilevile bei za umeme wa *TANESCO* wewe mwenyewe ni shahidi na wenzangu ni mashahidi jinsi ambavyo zilikuwa zimepanda sana. Sasa nina matumaini kabisa endapo Muswada huu utapita hata bei za umeme zinaweza zikafika mahali zikashuka kwa sababu ya ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa nitumie nafasi hii kutoa ushauri wangu. Ndani ya Muswada wameelekeza kwamba Shirika hili la *TANESCO* litapewa kipaumbele na litaimarishwa. Mimi naomba kama walivyoomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu maombi haya yasiwe lelemama isije ikawa mzazi aliyekuwa na mtoto mmoja alipopata mtoto wa pili, basi mapenzi yote yakahamia kwa mtoto wa pili, mapenzi kwa mtoto wa kwanza yakapungua ama yakaisha. Naomba sana pamoja na ushindani, na pamoja na kuruhusu mashirika mengine, naomba Shirika hili la *TANESCO*, Shirika letu, na ni Shirika la Taifa na Serikali ina uwezo kabisa kabisa kuliimarisha Shirika hili. Ndani ya kuliimarisha Shirika hili ni pamoja na kusaidia kuondoa madeni.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lina madeni, na linakabiliwa na madeni mengi pamoja na kwamba na lenyewe lilikuwa linadai na linaendelea kukusanya madeni yake, lakini bado nalo linadaiwa.

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa kutosha, tukienda Wilaya ya Manyoni tu hapo wapo wateja wengi waliotoa fedha zao kwa ajili ya kuunganishiwa umeme kwenye nyumba zao, lakini wateja hao mpaka sasa hivi hawajaunganishiwa umeme, na sasa ni mwaka na kitu, na inasemekana Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya aliyekuwa anahudumia alipokea fedha, na baada ya Shirika kubaini kwamba amekula zile fedha amefukuzwa kazi. Pamoja na huyo Meneja kufukuzwa kazi je, hao wateja ambao tayari fedha zao zilikwishapokelewa na Shirika ni lini basi wataunganishiwa umeme? Kama kweli tunataka kuingia kwenye soko la ushindani, naomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa anamaliza madeni ya wateja wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Manyoni na maeneo mengi katika nchi yetu. Akifanya hivyo atakuwa amechukua hatua nzuri katika kulisafisha Shirika la *TANESCO* na kuliweka katika eneo zuri la kuboreka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba sasa nizungumzie kuhusu Sheria ya umiliki wa mita. Wapo wananchi wengi wenye nyumba zao, hawana uwezo wa kuunganisha umeme kwenye nyumba zao, na bahati nzuri nyumba hizo wanazipangisha. Mpangaji anapopanga kwenye nyumba ambayo haina umeme mara nyingine kwa sababu umeme ni kitu muhimu huamua kuunganisha umeme kwa jina la kwake huyo mpangaji, na wakati huo huo mpangaji huyo hufika mahali hujenga nyumba yake. Sasa kizaa zaa kinakuja pale mpangaji anapoamua kuhama kwenye nyumba hiyo aliyopanga na kuhamia kwenye nyumba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba Sheria hii itazama upya suala la umiliki wa mita ili mpangaji anapohama, basi aruhusiwe kuhama na mita yake, kwa sababu hiyo ni halali yake, aliunganisha umeme kwa gharama zake. Sidhani kama tutakuwa tunamtendea haki mpangaji huyo atakapohama na kunyimwa mita yake.

Mheshimiwa Spika, hili limetokea, sisemi kwa kubahatisha, Manyoni hilo limetokea, huyo mpangaji hajahama na mita kisa nyumba hiyo ilikuwa ya mtumishi wa TANESCO, basi amenyang'anywa hiyo mita huo ni uonevu. Naomba sana uonevu huo utazamwe kwa jino la huruma kabisa mpangaji aruhusiwe kuhama na mita yake kwa sababu huwa ameinunua kwa gharama yake. Maana tunapomnyima inakuwa hatumtendei haki, na siyo Manyoni tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeongea na Waheshimiwa Wabunge wengi, matatizo haya yapo katika maeneo mengi tu hata Mkoa wa Kagera huko, Mheshimiwa Ruth Msafiri hapa amesema mambo haya yapo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri katika Muswada wake atazame upya namna ya kumiliki mita za umeme.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu nimeufurahia sana kwa sababu endapo tutaingia kwenye biashara ya ushindani kwa maana ya mashirika mengine kuwekeza kwenye suala la umeme, nina matumaini makubwa kabisa Mkoa wa Singida sasa tutakuwa tumepona.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida umeme upo, lakini ni maeneo machache tu ambayo yana umeme, na umeme ni miundombinu mojawapo ambayo inasaidia wananchi wetu kuinua uchumi wao na kuweza kufanya shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, ukienda Manyoni hapo kwa Mheshimiwa John Chiligati ninamwonea huruma, na hivi mwenzangu ana dhamana ya Serikali hata kutetea Jimbo lake hawezi, naomba nimsemea baba yangu. Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ana Kata moja tu yenye umeme ambayo ni Kata iliyopo Manyoni Mjini.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunaingia kwenye utandawazi naomba sana tuangalie maeneo ambayo hayana umeme, kwa sasa yapate umeme kwa sababu tutakuwa na biashara huria. Hata ukienda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Paul Lwanji ana Kata mbili tu za Nyalada na Itigi ambazo zina umeme. Kata nyingine zote katika Manyoni hazina umeme. Nataka nitoe mfano wa wilaya moja tu, kata zote katika wilaya ya Manyoni ambapo kuna Kata 21 ni Kata tatu tu zenyewe umeme, na umeme huo upo kwenye makao makuu ya kata tu, haujasogea hata kwenye kijiji kimoja. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tunaingia kwenye biashara huria sasa itakapoanza biashara hiyo, naomba Mkoa wa Singida na Wilaya zake zipewe kipaumbele katika kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la nguzo. Suala la nguzo ni kero kwa wananchi wetu kwa kweli, wananchi wetu wana hamu sana kuwa na umeme kwenye nyumba zao, lakini unakuta mwananchi anajenga nyumba ili aunganishiwe umeme,

lakini zinatakiwa nguzo mbili, tatu, na gharama ya nguzo ni ghali. Wananchi wanashindwa kuunganisha umeme kwenye nyumba zao kwa sababu ya gharama za nguzo.

Naiomba sasa Serikali kupitia Muswada huu suala la nguzo litazamwe upya. Wananchi wasipewe mzigo mzito ambao utawafanya washindwe kuunganisha umeme kwenye nyumba zao, na siyo wananchi tu. Kuna miradi ya maendeleo Manyoni, kuna mradi wa maji upo umbali kama kilomita 10 kutoka Manyoni mjini, na ili uendeshwe mradi huo mashine inatakiwa isukumwe kwa umeme, na umeme kuutoa mjini Manyoni kuupeleka kwenye *site* ya maji ni gharama kubwa. Wilaya imeambiwa itoe shilingi milioni 168, hebu niambie Wilaya kama Wilaya itaweza hiyo kazi?

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la nguzo za umeme litazamwe upya kwa sababu gharama yake ni kubwa na si wananchi wengi wanaoweza kumudu gharama hiyo na hata miradi yetu mingi ya maendeleo inakwama kutokana na gharama kubwa za nguzo za umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu madeni. Wananchi wanaotumia umeme wanajitahidi sana kulipa madeni yao pale wanapolimbikiza baada ya kutumia umeme. Lakini tatizo watumiaji wa umeme waliopo kwenye kata ama wilaya wanapolipa deni lao halifutwi, deni kwenye kompyuta linabakia, anaambiwa eti mpaka gharama hizo ama deni hilo lipelekewe mkoani ndipo lifutwe. Matokeo yake unakuta deni hilo linaendelea kuonekana kwenye ankara ya umeme ya kila mwezi, mwezi wa pili, mwezi wa tatu, kitu ambacho kinawapa usumbufu sana wateja. Na wateja wengi si waelewa wa kutosha, unaweza kukuta mteja akalipia deni moja hata mara mbili, mara tatu, akidhani ni gharama yake ya mwezi huo, kumbe bado anarudishiwa lile deni ambalo tayari alikwisha kulipa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitashukuru sana kupitisha Muswada huu kama wataangalia upya katika ulipaji wa madeni ya wateja pale wanapolipa, basi wafutiwe pale pale, deni hilo lisiendeleo kuonekana kwenye ankara ya kila mwezi. Kwa sababu watakapoendelea kuonyesha lile deni hawamtendei haki mteja, na mteja huyo ataendelea kulipa deni wakati tayari deni hilo alikwisha kulipa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, natumaini kabisa Mheshimiwa Waziri amenisikia atatekeleza hayo, na maeneo ambayo hayana umeme katika Mkoa wa Singida yatapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa mara ya pili. (*Makofi*)

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, mimi sina matatizo kabisa na madhumuni na sababu za kuwepo Muswada huu wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007. Wahenga husema “ umoja ni nguvu”, ni kweli kabisa wakati umefika *TANESCO* sasa ipate watu wa

kusaidiana nayo katika kuimarisha mahitaji ya uzalishaji wa umeme katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kwamba wananchi sasa hivi wamechoka na adha ya kukatika umeme katika maeneo mbalimbali, na hususan katika kipindi cha ukame. Lakini nina masikitiko makubwa sana kule Maswa wakati mvua zinanyesha, na hivyo kuna maji ya kuzalisha umeme, umeme ndiyo unakatika mara kwa mara. Wakati faida ya Muswada huu ni kwamba hasa katika kipindi cha ukame pawepo na uzalishaji wa umeme wa kutosha. Kwa hiyo, naiomba Serikali na ninamwomba Mheshimiwa Waziri achunguze sana ufanisi wa utendaji wa Shirika la *TANESCO*. Haitakuwa na faida kwamba Serikali inakusudia kulibeba Shirika hili, lakini lina uchakavu wa utendaji, kwa nini kunatokea uchakavu huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wamekaa kwenye maeneo kwa miaka saba, kumi wanafanya kazi kwa mazoea. Sasa hao watu wanakuwa hawana ugunduzi, hawana kujituma, wanakuwa na mawazo mgando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati umefika Shirika la *TANESCO* Wizara ilisimamie. Wizara ilisimamie Shirika hili kuhakikisha kwamba watendaji wake wanakuwa na ufanisi na wajengewe *capacity building* ya kushindana na mashirika yanayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuelewa wazi kabisa kwamba Watanzania tunamtegemea sana yeye kwa sababu yeye ni pambazuko jipya lisilo na ndoa, lisilokuwa na kutu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na upeo wa Mikataba mipya itakayofanana na matarajio ya Watanzania kwa tabia zake za utu na ubinadamu na ustaarabu wa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua Muswada huu una ushawishi wa kila aina, una uchambuzi wa kiuchumi kwa faida na maslahi ya Tanzania. Natambua kuna *EWURA* imeandaliwa utaratibu wa kuwa na refarii lakini hayupo katika utaratibu wa kusaidia Mashirika kupeleka umeme vijijini. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, na naiomba Serikali ibuni ni utaratibu gani na nani hasa atakuwa mhimili ambaye atathibitika kuwa na juhudi za kupeleka umeme vijijini. Kuna changamoto nyingi za kutosha, zimetajwa katika maelezo ya wachangiaji mbalimbali walionitangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hoja kubwa kwa Watanzania wa Maswa, Mkoa wa Shinyanga na Tanzania nzima Bara na Visiwani ni upandaji wa gharama za umeme. Hilo ndiyo tatizo kubwa. Wananchi wa vijijini Maswa wamechoka kutumia minyaa hasa akinamama zangu wanapopuliza mpaka mnyaa ushike moto, macho hubadilika na kuwa mekundu na watu wenye tafakari za akili wanasema dalili za mchawi ni macho mekundu. Naiomba Serikali itazame kwa huruma Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mwanza ambako kuna maneno maneno ya minong'ono kwamba akinamama wazee wenye macho mekundu ni dalili ya uchawi. Kwa hiyo, naomba umeme utufikie kwa haraka na upendeleo maalumu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, watoto vijijini wamechoka kutokwenda skuli mpaka wakatafute kuni. Lakini umeme huo pamoja na kusema kwamba utazalishwa mwingi, utazalishwa kwa tabaka la watu wa miji. Je, vijijini watawezaje kuupata umeme huo ikiwa gharama tu hivi sasa hata mtu wa mjini anaona shida? Vijijini uchumi wa kaya ni wa msimu wa pato la pamba linalolimwa mara moja kwa mwaka. Naiomba Serikali izingatie na ione huruma ya kwamba maisha bora yanayopatikana katika majiji na miji, wananchi nao vijijini wanataka maisha bora ya huo huo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi yetu ina mwongozo mkubwa mzuri sana, na tunaamini kabisa kwamba Serikali inaongozwa na kutekeleza matakwa ya Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Ibara ya 8(1)(a) mpaka (d) inasema: “Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya jamii, na kwa hiyo:-

(a) Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.

(b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi.

(c) Serikali itawajibika kwa wananchi.

(d) Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.”

Mheshimiwa Spika, naomba Ibara hii isomeke na Ibara ya 9(c) na (d), naomba ninukuu Ibara ndogo (c) na (d) kama ifuatavyo:- (c) inasema kwamba: “Shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Tanzania unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kunyonya mtu mwingine.” (d) inasema: “Maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kunukuu hayo sasa naiomba Serikali na namwomba Waziri watuthibitishie Watanzania kwamba mikataba itakayotayarishwa baada ya Sheria hii kupitishwa haitokuwa na unyonyaji kama Mikataba iliyotayarishwa baada ya sheria hii kupitishwa ya kufaulisha uwekezaji katika madini. Mikataba iliyotayarishwa baada ya sheria ya kufaulisha mikataba ya uwekezaji katika madini ina unyonyaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kuwa Serikali itakuwa imejifunza, ninaomba kusema lugha ya kusema kwamba patakuwa na makusanyo makubwa kwa faida ya uchumi, kwa faida ya Taifa ni nzuri sana. Lakini Katiba inasema Tanzania na wananchi wake wanafaidika vipi na rasilimali hiyo kwa sababu mnapozungumzia mapato ya Taifa sawa, hayo mapato ya Taifa yanamsaidiaje mwananchi kijijini kuondoa umaskini wake? Naomba Sheria zitungwe ambazo zitaendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kila baada ya kupitishwa Sheria na Bunge hili panakuwa na Mikataba na wawekezaji wanakuja na lugha za ulaghai.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna lugha moja ambayo sasa wakati umefika tuiache Tanzania. Mtoto anapozaliwa anatambaa, anatembea legelege, anakomaa anakuwa imara. Hivi lini sisi Tanzania tutaacha lugha ya kusema kwamba tunawavutia wawekezaji. Kwa nini mikataba yetu iwe ya kunyonywa? Kila siku tunasema masharti ya kuwavutia wawekezaji. Rais George Bush amekwishafika Tanzania. Hivi Tanzania hatujajulikana tu? Tuendeleo kuwa na Mikataba ya ajabu ajabu ya kusema tunawavutia wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina ugomvi na Serikali, lakini wakati umefika Waheshimiwa Wabunge niwaombe kwamba tuungane kwa pamoja kukatalia masuala ambayo yanaletwa na Serikali kwa lugha za kuposa. Mtu anapopeleka posa anakuwa na maneno matamu sana. Lakini siri ya 'mtungi aijuyae kata baada ya harusi'. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sina ugomvi na EWURA. Lakini nina jambo moja ambalo linanitisha. Hii Mikataba sasa ni viwawa, wadudu wa uhuru wa Tanzania na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Mikataba hii hivi sasa ni mchwa, huku nje twang'ara, lakini ndani tumepukutika, ni hatari kwa Chama cha Mapinduzi kwa Mikataba hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, nuru na pambazuko jipya katika Awamu ya Nne, ahakikishe Mikataba inakuwa na upeo mpya wa kuzingatia maslahi siyo maslahi ya viwawa, wadudu wa uhuru wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali, hao wawekezaji binafsi wana kitu kinachoitwa *cooperate social responsibility*, uchangiaji katika maslahi ya jamii. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, na naiomba Serikali angalau asilimia 30 ya umeme watakozalisha uingizwe katika TANESCO kwa dhana ya kupeleka umeme vijijini. Sisi tuna rasilimali kwa nini kila saa tuwe wanyonge? Hao watu wanakuja kwa sababu wanajua hawawezi kwenda mahali pengine isipokuwa Tanzania tuna utajiri wa amani na utulivu na ndiyo sumaku ya kumvutia mwekezaji. Kwa hiyo, naomba asilimia 30 ya umeme utakozalishwa na mtu binafsi aupeleke kijijini. Ninaomba kiwepo kifungu kwenye Kanuni aidha kama ni Sheria kiwepo kifungu cha kumwambia huyo mtu. Utu wetu unatuponza sana.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunaponzwa na ubinadamu wetu, tukidhani ubinadamu wetu kila binadamu ana utu huo. Hata Mikataba yetu ina ubinadamu, tutajadiliana kama patakuwa na tofauti, tunaponzeka, tubadilike twende na wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa iendane na dunia ya sasa. Rais George Bush alikaa hapa nchini kwa muda wa siku tatu. Sasa bado mnasema kwamba tunawavutia wawekezaji, tutawavutia mpaka lini au mnataka tubakie na mashimo? Naiomba Serikali inisaidie kuelewa hata Amerika inawavutia wawekezaji, Ufaransa inawavutia wawekezaji kutoka Japan, Marekani inawavutia wawekezaji kutoka China. Je, Mikataba yao ni ya

kunyonya kwamba wanawavutia wawekezaji au sisi ni kichwa cha mwendawazimu cha kujifunzia kinyozi? Naiomba Serikali ituondoe katika aibu hiyo. Naomba Mikataba hiyo sasa ijenge dhana ambayo inatamkwa na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba rasilimali zetu zitatumika kwa maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Tanzania tusiwe maskini wa bahati ya kuwa na rasilimali. Maana yake sasa Watanzania tunaonekana ni watu ambao ni bahati mbaya kuwa na rasilimali, lakini ni matajiri wa Mikataba *fake*, aibu kubwa sana hiyo!

Mheshimiwa Spika, imani bila matendo mema hufa. Watanzania wana imani na Serikali yao lakini imani yao itakufa kama panapatikana watendaji ambao hawana imani na maslahi ya nchi yetu na hawana uzalendo. Wala huwezi ukalaumu msahafu kwa udhaifu wa shehe wala huwezi ukalaumu biblia kwa udhaifu wa Askofu. Sasa ninakuoneni mkipime na mjitazame watendaji ndani ya Serikali ni nani hasa wanaokaa wakaamua wale uhondo baada ya kupitishwa sheria. Naiomba Serikali sasa iondokane na aibu ya kuwa na mikataba kwa matendo ya uungwana wa kurejesha imani kwa Watanzania kwamba tuliwekeza vijana wetu wakaenda kusoma shule na wakaenda nje ya nchi ili wakavune warudi hapa waonyeshe uzalendo wao kwa Tanzania. Vijijini wamechoka na mikataba na kila siku tunapewa pole. Hivi toka lini pole ikaondoa ukiwa wa mjane? Naomba sasa Serikali ikarabati kuteguka kwa fikra. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili sasa.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimika Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shibuda, inavutia namna unavyowasilisha hoja kwa Kiswahili kilicho fasaha kabisa na hoja zinakuwa nzito. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Anastazia Wambura, ajiandae Mheshimiwa Juma Killimbah, atakayefuata baada ya hapo ni Mheshimiwa Bujiku Sakila.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa tatu asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowasilisha Muswada huu kwa ufundi na kwa utaalumu na vilevile napenda sana kuipongeza Kamati kwa kuuboresha huu Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 na hivyo kuuwezesha kukubalika na Waheshimiwa Wabunge ambao ni wengi kama si wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ninazo sababu za kuunga mkono hoja hii au Muswada huu na sababu ya kwanza ni ile changamoto ambazo Wizara yenyewe imezibainisha. Ni changamoto

nyingi na kuonyesha kwamba inaweza kuhitajika kiasi cha shilingi trilioni 1.6 ili kuanza kuzifanyia kazi baadhi ya changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, nina moja ambalo limenigusa kati ya hizi changamboto nacho ni kirusi kimoja kinachoitwa rushwa. Nadhani tunafahamu kabisa kwamba maradhi yanayotokana na kirusi au virusi ni kazi kweli kweli kuyatibu ni kazi ngumu hasa. Kwa hiyo, kwa upande wa *TANESCO* kirusi hiki cha rushwa hata tukiweka trilioni ngapi itakuwa ni vigumu sana kukitibu hiki. Lakini nadhani suluhisho bora kwa sasa kwa *TANESCO* kwa kweli ni kuleta ushindani kama unavyopendekeza huu Muswada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo sababu ya pili ya kuunga mkono hii hoja na sababu hii ni mwelekeo na mfano mzuri ambao umeonyeshwa na Kampuni moja inayozalisha umeme wa gesi kule Mtwara na Lindi na Kampuni hii inaitwa *ARTUMAS*. Kampuni hii inasema kwamba sheria ikiruhusu, kufikia Novemba, 2009 itakuwa imefanya kazi nyingi tu na mojawapo ni kukarabati miundombinu ya umeme ili kuzuia upotevu wa *voltage* kutokana na uchakavu wa miundombinu hii na vilevile kuzuia kukatika katika kwa umeme. Lakini pamoja na hayo itajitahidi kuunganisha laini kutoka Mtwara hadi Tandahimba, vilevile kutoka maeneo ya Nyangao hadi Ndanda. Itaunganisha pia laini kutoka Nachingwea hadi Ruvuma. Hii ni kazi nzuri, *concept* hapa ni kwamba *ARTUMAS* itakapoendelea kupanua uzalishaji basi bei kwa mtumiaji wa mwisho kwa mlaji itakuwa ni ya chini. Kwa hiyo, hiki ni kiashiria kizuri kwamba baada ya muda mfupi maeneo yale ya Kusini, vijiji vingi vinaweza kupatiwa mwanga kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tunatunga sheria lakini naamini kwamba sheria hii itakapopita itakuwa ni ufunguo kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa. Lakini kuwa na sheria ni upande mmoja, lakini kuichukulia sheria ni upande wa pili. Kuna mwandishi mmoja anaitwa Suzan Jeffer yeye anasema hivi, samahani nitatumia ile lugha aliyotumia anasema: “*Security is not having things, it is handling things*”. Hii ni kweli kabisa. Ni kweli kwamba usalama si kuwa na vitu bali ni kuvichukulia. Kwa hiyo, labda ninachotaka kusema ni kwamba mafanikio au matatizo yatakayotokana na huu Muswada yatategemea ni jinsi gani tutai-*handle* hii sheria na ni jinsi gani pia tutawa-*handle* hawa washindani ambao tunaweza kuwapata hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu mfupi naomba niingie kwenye vifungu ambavyo naona vinanipa utata, pengine vinaweza vikaleta utata baadaye kwa wale ambao wata-*implement* hii sheria. Tuanzie labda ukurasa wa 10 kuna kifungu cha 8(1)(a). Hapa panazungumzia, samahani naomba nisome: “*The following activities shall require a licence namely zipo (a) mpaka (h) generation, transmission, kuna kifungu (a) ambacho kinasema system operation.*”

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kututafsiria hii *system operation* au *system*. Kwa sababu katika Muswada huu tunakuta kuna vitu kama *generations system*, tutakuta *transmission system*, *distribution system* ipo, *power system* pia inaonekana. Lakini sasa mtu anaweza akawa na leseni ya *transmission* halafu hapo hapo pengine tuseme anakuwa na leseni ya *transmission system operation*. Sasa haya

naona kama yanachanganya kidogo. Kwa hiyo, naomba hii *system* au *system operation* ipewe tafsiri.

Mheshimiwa Spika, naomba niende tena kwenye ukurasa wa 11, Kifungu cha 9(2) ambacho pia kwa ridhaa yako naomba nisome, kinasema: “*The authority shall when considering application for licence take into account.*” Kuna mlolongo hapa wa mambo (a) mpaka (h). Ninapendekeza kwamba kiongezwe kifungu (i) ambacho kitahusu *sustainability of the activity*. Hii ni sehemu ambayo inayohusu kumfikiria yule mwombaji wa leseni. Kwa hiyo, yapo masuala ya mazingira, masuala ya kijamii, masuala mengi tu pamoja na uwezo wa kiuchumi. Lakini nadhani tumesahau hili suala la uendelevu wa zile shughuli ambazo zitafanyika. Nalisema hili kutokana na kwamba jana kulikuwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja naye aliuliza swali kama hili kwamba itakuwakuwaje kama mwekezaji amekwenda mahali halafu baada ya muda mfupi akaamua kujitoa tena kwenye ile shughuli kabla hawajaingia wawekezaji wengine. Lakini vilevile ilikwishawahi kutokea kipindi fulani ilitokea *Airline* fulani hapa Tanzania ika-*operate* kwa muda mfupi na baadaye ikawa imeondoka na kutokomea na pesa za watu.

Mheshimiwa Spika, naomba tena twende katika kifungu cha 10(1)(a) na vilevile kifungu cha 10(1)(b). Naomba nisome 10(1): “*The authority may suspend, vary or revoke a licence if the licensee violates terms and conditions of the licence, or any rule or regulations made under this Act whereby-..*” Ile (b) inasema: “*The violation occurs in a place repeatedly or persists for a considerable period of time.*”

Mheshimiwa Spika, hii “*considerable period of time*” nina wasiwasi nayo. Kwa sababu inaweza ikawa labda ni wiki moja au mwezi au mwaka au ni miaka kumi. Kwa hiyo, hapa labda inategemeana kunaweza kukawepo na mvutano *authority* ikasema labda mwezi mmoja lakini yule mwekezaji akasema hiyo *considerable time* ni miaka miwili. Kwa hiyo, nafikiri itakuwa ni vizuri tungeweka *limit* kwamba hii *time* ni muda gani.

Mheshimiwa Spika, naomba tena niende ukurasa wa 17, Kifungu cha 17(2)(b). Hiki nacho kinasema kwamba: “*Subject to subsection (1) of section 9, a transmission licensee shall be required to- (b) maintain, improve and expand his transmission facilities in an economical manner, taking due account of the Power System Expansion Plan*”. Hapa wasiwasi wangu kwamba linaweza likatokea lile ambalo limetokea kwa upande wa uzalishaji wa sementi ambapo tuna viwanda vingi na vinazalisha sementi kwa wingi sana. Lakini hivi karibuni imetokea shida ya bei kupanda sana na uadimikaji wa sementi kwa kisingizio kwamba sio *economical* pengine kusafirisha sementi kutoka Mbeya kuja Dar es Salaam au kwenda maeneo mengine. Kwa hiyo basi hawa wawekezaji wa sementi wamekuwa waki-*export* na sisi kulazimika ku-*import* sementi. Nina wasiwasi kwamba hii kama haikutafsiriwa vizuri mwekezaji wa umeme anaweza akasema sio *economical* kwenda mahali fulani japo mbele hapa pameonyesha kwamba labda ata-*take account* ya *Power System Expansion Plan*. Nadhani ni vizuri pakafafanuliwa kama ni hii *economical manner* ni kuzuia *power loss* au kutumia *low production cost* au ni kitu gani hasa walikuwa wanamaanisha hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba niende ukurasa wa 29 kifungu cha 35(4) ambacho nacho kinazungumzia kwamba mwekezaji huyu kama atatumia *infrastructure* za *public* yeye asilipe chochote. Lakini tunasahau kwamba kuna wawekezaji wa *solar power* wale wanaweza wasitumie ardhi kwa sababu hiki kipengele kinahusiana na ardhi. Hawa wanaweza wasitumie ardhi lakini wakaamua kutumia *public buildings* kwenye zile *panels* na wawekezaji wengine ambao ni wengi nchi nyingine wanakodi, huwa wanalipa kwa mwezi au kwa mwaka. Sasa iweje sisi Tanzania mwekezaji huyu ametumia jengo la shule au hospitali lakini sheria haisemi chochote kwamba atahitajika kuifanyia matengenezo au kulipia kitu chochote. Kwa hiyo, naomba hiki kipengele nacho kiangaliwe vizuri na kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kuna hii karatasi ya marekebisho nilikuwa naomba tuangalie huu ukurasa wa kwanza ile *amendment*. Kuna sentensi moja hapa ina- *define high voltage* lakini kuna “*two*” nilikuwa naomba ihamie kwenye *equally two or above*, ifutwe pale. Ukurasa wa 5 kuna neno moja *installation* limerudiwa mara mbili kwa hiyo, naomba *installation* ya pili ikatwe kwenye kipengele cha (*T*) *clause* 41, *installation* moja imerudiwa nadhani kimakosa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba pamoja na kwamba hii sheria itaruhusu wawekezaji mbalimbali lakini *TANESCO* kama walivyotangulia kusema wenzangu isisahaulike, iboreshwe. Lakini vilevile tuwe makini na kile kirusi ambacho nadhani ni hatari sana katika kutekeleza hii sheria. Nadhani tukitumia vizuri hii sheria tutaondokana na yale masuala ya watoto wetu kusomea vibatari, akina mama wetu kukoboa nafaka kwa kutumia mawe kwa sababu zana zile za mawe kwa kweli zimepitwa na wakati. Lakini wapo wanaokoboa nafaka kwa kutumia mawe. Kwa hiyo, naomba tuitumie vizuri hii sheria ili kusudi tuweze kuleta ukombozi na kuleta mwanga katika nchi yetu. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Muswada huu. Muswada ulio mbele yetu Muswada ni muhimu kabisa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii Mheshimiwa William Mganga Ngeleja. Pia nimpongeze Mheshimiwa Adam Malima, vilevile niwapongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri na kazi nzuri walioifanya kuhusiana na Muswada huu. Pia nisisahau Kamati ya Bunge, Kamati ambayo imefanya kazi kwa umakini sana ikiwa chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu kwanza nianzie kwa kusema nauunga mkono upite kwa asilimia mia moja. Lakini wakati tukiendelea na Muswada huu kuna mambo mengi ambayo yamejitokeza na ambayo pengine wananchi wamekuwa wakituhoji na wamekuwa wakituhoji kwa nia njema tu kwa sababu sisi ni wawakilishi wao. Wanasema nyinyi Waheshimiwa Wabunge mara ya kwanza mlisimama mkaonyesha kwenye semina mkaupinga sana Muswada huu, mkasema hauna maslahi na

wananchi. Wanauliza hivyo kwa nia njema ili na wao wapate uelewa, lakini sasa wanasema mbona mnaelekea kuukubali?

Mheshimiwa Spika, ningepomba nitumie fursa hii ili wananchi watuelewe kwamba Bunge hili Tukufu tupo kwa ajili ya kujadili masuala ya maslahi yanayowahusu wao wenyewe wananchi. Tupo kuangalia yale mambo ambayo yote tunaamini kwamba yatakuwa mema na yatafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Kwa hiyo, walipotuona wakati ule tulipokuwa tunafanya pengine kwa nia tu ya kutaka kuuboresha huu Muswada tulikuwa bado tunataka tujihakikishie kwamba hiki kitakacholekwa ndani ya Bunge hili Tukufu na tukaja tukakipitisha basi kisiwe na shaka tena, kiende na kikafanye kazi inayokusudiwa na kwa kumletea maendeleo mwananchi. Ndiyo lilikuwa lengo letu kabisa.

Mheshimiwa Spika, yako mengine ambayo hata wenzangu waliochangia wameonyesha shaka. Wengine wakasema tunapopitisha Muswada namna hii inaweza kutokea matatizo baadaye katika utekelezaji wa sheria, kunaonekana kunakuwa na shaka. Lakini nasema hapana shaka. Bunge hili Tukufu lipo kwa ajili ya kupitisha mambo mbalimbali yanayohusu sheria za nchi. Sheria ikija ikileta matatizo tutarudi ndani ya Bunge hili Tukufu na tutafanya kazi hiyo na tumechaguliwa na wananchi ili tufanye kazi hiyo. Kwa hiyo, hilo halina shaka kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujiridhisha kwa masuala mbalimbali ikiwepo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 hadi 2010, ikiwepo Sera ya Nishati na Madini, tumehakikisha na tunaona kwamba huu ni wakati muafaka sasa kutoka katika ile hali ya uchumi hodhi ili twende katika soko huria kwa maana ya kukaribisha wawekezaji. Hii imetamkwa wazi wazi ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 hadi 2010. Kwa hiyo, huwezi ukakidhi matakwa ya Ilani kama hutaleta Muswada na ukapitishwa ikawa kama sheria. Ni kwamba lazima ulete ndani ya Bunge upitishwe ili iwe sheria ndiyo utakuwa umekidhi matakwa ya Ilani, kwa hiyo, tuko sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, nimeshiriki kwa hatua zote zile za awali za kuupitisha huu Muswada ndani katika ngazi ya Kamati na nilishiriki ili nijihakikishie kwamba haya tunayokwenda nayo ndiyo ambayo tutakuwa tunayapitisha. Mimi naweza nikasema sitakuwa na mgogoro sana kuhusiana na vifungu ambavyo vipo ndani ya sheria yenyewe, sina mgogoro kabisa. Isipokuwa nitakuwa na hoja labda na maoni kidogo hapo ambapo nitakapopita mbele na wakati huenda nikaja nikachangia kutokana na jinsi ambavyo ninaweza nikauboresha zaidi ili iwe una maslahi na mafanikio zaidi huo tuendako.

Mheshimiwa Spika, naweza nikazungumzia eneo moja katika hivi vifungu nilivyovieleza na hii nadhani katika kuuboresha tu. Katika Muswada wenyewe sehemu ya 3 kipengele cha 9 kile kinachosema “*The licence issued under section 8 shall among others, contains...*” Hapo yametajwa blaa blaa kutoka (a) mpaka (g). Hapo inasema kutakuwa na “*technical financial and other necessary information as may be required by the authority*”.

Mheshimiwa Spika, hapa nilitaka tu suala la *financial* ili kukwepa masuala kama ya *RICHMOND*. Nilikuwa nataka lazima iwekwe wazi kwamba tunahitaji huyu mtu atakayekuja kupewa leseni ya aina hii kama atapewa leseni ya kuzalisha tunataka awe na kiwango kitakachowekwa bayana. Kwa sababu tuepukane na watu ambao wanaweza wakaja wakaingia kwa kuomba wakapata leseni lakini wakawa hawana uwezo wa kutoa huduma. Lakini pia tunapozungumzia suala la *technical, which number of technicians?* Ni wangapi wanaotakiwa na wawe na uwezo gani? Kwa mfano, upande wa uzalishaji wanatakiwa wawe wangapi? Upande wa usambazaji wawe na vyeti gani, lazima ijulikane. Hii itatusaidia tu katika kuondoa wale watu ambao tunasema wanaweza wakadandia na wakaja wakafanya labda katika hii hatua na kuweza kuharibu kazi nzuri ambayo leo tunapitisha na baadaye ikaonekana kumbe hatukupitisha kitu ambacho kilikuwa kina maana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda hili eneo Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anafanya majumuisho pamoja na wataalamu wake ili waone ule umuhimu na kwa ajili ya kuweza kujilinda sisi wenyewe na kulinda Wizara yenyewe na kulinda hali halisi ya utoaji wa leseni ambao watakuwa na jukumu hili watu wa *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la *TANESCO*. Naamini kwamba pamoja na kwamba tunapitisha sheria hii bado *TANESCO* ndio wenye jukumu hadi sasa la kusambaza na kugawa umeme nchi nzima, hilo hatuwezi tukakwepa. Kwa sababu bado tupo kwenye mchakato na kwa kuwa bado tupo kwenye mchakato na kazi bado inaendelea nataka niwatahadharishe *TANESCO* kuhusu suala moja ambalo kwa kweli naona kwa namna moja ama nyingine wanazembea. Hii ni lazima tuwaseme. Tunaelewa kwamba tunachangia Muswada lakini si bajeti ila lazima tuseme kwa sababu tunazungumzia mambo yanayohusu umeme.

Mheshimiwa Spika, bado uzembe unaofanyika uko wa wazi kabisa. Mwaka 2006 niliwahi kuwasiliana na *TANESCO* wao wenyewe kwa mahitaji ya kupelekewa umeme kutoka eneo la Shelui kwenda eneo la Mgongo lenye kilomita kama 5 hivi ambako kule kuna Kituo cha afya cha Tarafa. Na wakati ule wakanifanyia hesabu wakaniambia gharama zote mpaka kupeleka umeme ilikadiriwa kiasi cha shilingi milioni 17. Sasa nikawaambia fanyeni kwa sababu kama mzungumzaji mmoja alivyozungumza jana na wakati ule kweli nguzo zilikuwa zipo, wakaniambia hili sio suala letu ni suala la wakala wa umeme vijijini lakini tutaangalia hali ya bajeti itakavyokuwa ili tuweze kupeleka umeme. Mwaka jana nimeendelea, nikaambiwa bei imeongezeka kutoka shilingi milioni 17 imefika milioni 54. Sasa nikawaambia hii bei kama tungepeleka mwaka huo uliopita ambao ni 2006 ingekuwa shilingi milioni 17.

Mheshimiwa Spika, lakini juzi nimemwandikia Mheshimiwa Waziri Ngeleja mwenyewe na aliponijibu akaniambia kwamba gharama ya kupeleka umeme kutoka Shelui hadi hapo Mgongo ni kiasi cha shilingi milioni 84. Unajua hizi gharama ukija ukiangalia hizi ni hesabu za kawaida kabisa yaani kama ungeweza ukatupelekea umeme toka mwaka 2006 kwa kiasi cha shilingi milioni 17 leo hii tusingefikia shilingi milioni 84. Na hii naisema shilingi milioni 84 lakini tusipopeleka mwaka huu umeme pale Mgongo nawahakikishia nitaambiwa mwakani itakuwa shilingi milioni mia moja na kitu.



Mheshimiwa Spika, zipo *transformer* ziliachwa, yako maeneo yanapitiwa na gridi ya Taifa na ule umeme uliopozwa unapitia katika baadhi ya vijiji. Nimewahi kufanya *consultation* na Wizara nikawaambia hebu waambieni TANESCO hizi *transformer* zilizoachwa na Kampuni ya *Chico* nisaidieni muwape vijiji vile wapate umeme. *Transformer* zipo mpaka sasa hivi, wale *Chico* wameanza kuondoa vitu vyao vya kazi lakini zile *transformer* zipo na hazijafanyiwa kazi na wala hakuna dalili ya kuwapa umeme wanavijiji. Namwomba zile *transformer* zije zifanyiwe kazi kwa vijiji husika vinginevyo hamtaweza kuzihamisha.

Mkizihamisha hatutaelewana na ile ni mali ya umma na wale wananchi wa pale wanaohusika ndio wananchi wenyewe na umma wenyewe ndio ule. Kwa hiyo, naomba zisije zikabebwa zikapelekwa mahali pengine. Kwa sababu zilifanya kazi zimekaa zaidi ya miaka 4 na wananchi wamezilinda. Sasa wananchi hawatakuwa na amani kuona zile *transformer* leo zinabebwa zinapelekwa mahali pengine ili zikafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoongea awali nimesema sina mgogoro kabisa na huu Muswada, najua kwamba lazima sasa tunaingia kwenye ushindani na mahali popote penye ushindani ni lazima panatokea maendeleo. Ushindani wenye maana na sisi hatuwezi kuupinga na hii haitakuwa nchi ya kwanza kukaribisha ushindani wa vitu katika sekta hii ya umeme. Tunayo mifano ya Uingereza, wamefanya vitu kama hivyo, suala la huu umeme umekuwa vizuri na nchi kadha wa kadhaa. Kwa hiyo, sisi hatutakuwa wa kwanza. Nimesema sina mgogoro kabisa na huu Muswada na nasema nauunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majina mawili ya Waheshimiwa Wabunge waliotaka kuchangia Muswada huu yalirukwa kwa bahati mbaya, nao ni Mheshimiwa Prof. Mwalyosi na Mheshimiwa John Paul Lwanji. Kwa hiyo, nimefanya mashauriano naona inawezekana saa 11.00 tukaongeza kama saa moja hivi ikafika hadi saa 12.00 ili kutoa nafasi kwa wale ambao walitaka kuchangia wapate nafasi. Baada ya hapo ndiyo nitamwita Waziri kwenye saa 12.00 halafu tunadhani tutazitumia vizuri dakika 45 saa 1.00. Kama atatumia dakika zote 60 Mheshimiwa Waziri basi saa 1.00 nadhani dakika 45 kwa Kamati tunaweza tukamaliza.

Kwa sasa mimi natoka kwa sababu naandaa Kikao cha Kamati ya Uongozi ambacho kinaanza saa 7.00 na Mheshimiwa Ndugai atakuja hapa lakini mtiririko ambao sasa unafuata ni Mheshimiwa Bujiku Sakila halafu rafiki yangu Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, hajasema siku nyingi na ameniomba udhuru kidogo. Naona baada ya Mheshimiwa Sakila afuate Mheshimiwa Ndesamburo halafu ndio Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kwa mtiririko ule nilioutangaza awali. Sasa namwomba Mheshimiwa Ndugai aje ili aweze kuendeleza shughuli zilizosalia kwa hii saa moja.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y.Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Bujiku Sakila.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Lakini kabla ya kusahau kabisa napenda kusema kwamba napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Inahitaji ujasiri na hekima kubwa sana kuleta Muswada huu hasa baada ya wimbi kubwa lililojitokeza. Kwa hiyo, kutokana na ujasiri ndiyo maana nawapongeza sana. Aidha, napenda nitumie nafasi hii kuipongeza Kamati iliyotumia muda wake kujadili kuupitia Muswada huu, imefanya kazi nzuri sana, imerahisisha kazi yetu na nafikiri tunakwenda vizuri, nawapongeza sana.

Lengo la Muswada huu ni umeme kwa Watanzania. Nchi yetu iliamua kuunda Shirika la *TANESCO* kwa nia hiyo njema ili wananchi waweze kupata umeme. Leo tupo hapa tunaunda Sheria kwa ajiri ya kufikia lengo hili ambalo halijafikiwa. Niweze kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Mimi naona kwamba Muswada huu utatuletea Sheria ya uwezeshaji utakaolenga kuleta umeme kwa wananchi wetu. Nauangalia umeme kwa sababu ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu. Kipindi hiki tulichonacho Tanzania katika ulimwengu wa teknolojia, teknolojia hii inatarajiwa kuleta umeme. Umeme huu kama haujafika vijijini na kama haujawafikia wananchi wengi teknolojia hii haiwezi kupatikana. Mimi nilikuwa najaribu kuangalia, wananchi wameshiriki katika ujenzi wa shule za Sekondari za Kata karibu nchi nzima. Katika shule hizi tunahitaji wanafunzi wapate elimu ya kutosha. Baadhi ya Wabunge hapa wanaongelea juu ya maabara, maabara hizi zitahitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna mradi kabambe wa kilimo, bila umeme kijijini nina mashaka kama matunda ya mradi huu yatakuwa na maana sana katika nchi yetu. Ndiyo maana kwa sababu mimi naona huu Muswada unatupeleka kwenye Sheria ya kuwaletea wananchi umeme, naona ni vyema niunge mkono ili tuone kama inawezekana. Mimi nina maombi kadhaa. Kwanza, nina ombi kwa *TANESCO*. Nafahamu *TANESCO* wana mashaka mashaka sana juu ya Sheria hii inayoundwa, mimi naomba sana wasijisikie vibaya na hasa kwa sababu Serikali imekwishawahakikishia kwamba haitawaacha. Naomba sana *TANESCO* waukubali ukweli kwamba kazi hii waliyokuwa wamepewa ilikuwa ni kazi ngumu, nzito, yenye gharama kubwa na kwamba kwa uwezo wao inaelekea wamekwishafika kikomo. Tumepewa taarifa kwamba tangu *TANESCO* ianzishwe hadi leo wananchi vijijini ni asilimia moja tu waliopata umeme. Mijini ni asilimia 11, kwa hiyo, lazima wakubali kwamba ni kazi kubwa sana na wanahitaji msaada. Kama mtu una shamba kubwa sana kipindi cha palizi kimefika na unaona huwezi kumaliza palizi katika kipindi muafaka unaalika majirani wanakuja kukusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *TANESCO* wakubali kwamba tunawasaidia kuwaalika majirani waje wawasaidie katika kazi hii muhimu kwa taifa letu. Mimi nafahamu mashaka ya *TANESCO*, mashaka ya baadhi ya Wabunge, mashaka ya wananchi na mashaka yangu mimi mwenyewe. Tunavyopitisha Sheria hii *TANESCO* tunaiweka kitanzi na kupona kwao kunategemea mambo yafuatayo: (i) Serikali ikubali

kwa dhati kuwasaidia na (ii) *TANESCO* yenyewe ijirekebishe. *TANESCO* kama haijajirekebisha itakwenda na maji, hapa hakuna suluhu, tutadanganyana kwamba itaendelea kuwepo, itakufa na kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ni mali yetu, iliundwa na Serikali yetu, imeshindwa kufanya kazi yake hii. *TANESCO* ina uchungu na Watanzania. Leo tunaleta kutoka nje waje wafanye kazi hii kwa namna gani watu hawa watakuwa na mapenzi makubwa zaidi kuliko Watanzania ambao wapo katika shirika la *TANESCO*? Tunaikubali Sheria hii ipite kwa uchungu mkubwa sana na kwa mfidhaiko. *TANESCO* imetuangusha na wenyewe wakubali kwamba imetuangusha na ni vyema tuangalie nyuma kitu gani kilichotokea na wajitathmini kwa dhati kuona kwamba ni kitu gani kilichotokea mpaka kufikia hatua hii. Nilisikiliza baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge katika kipindi hiki ambapo *TANESCO* ina hali mbaya sana, bado wanapeana bili za bure na bahati nzuri sana Mjumbe wa Bodi alikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashangaa, hivi ng'ombe anaumwa na amekonda unaendelea kumkamua, unategemea nini? Si atakufa tu! Kwa hiyo, ni vyema tu *TANESCO* waanze kujirekebisha na kuangalia wana sehemu gani katika maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *EWURA* kama sehemu nyingine ya kuweza kuwaokoa *TANESCO* ifanye kazi yake vizuri. Tukiwaachia *TANESCO* wanaenda na Shirika linaenda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili ni kwa *REA*. Kwa bajeti ya kipindi kilichopita niliarifiwa kwamba kulikuwa na shilingi bilioni kumi na napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri wakati wanahitimisha watuambie zile shilingi bilioni kumi zimekwishafanya kazi na zimefanya kazi wapi? Kama hazijafanya zipo wapi na kama zipo *REA* napenda kushauri kitu kimoja kwamba fedha hizo zipelekwe kwenye shule zetu za Kata kwa maana ya kupeleka miradi ya *solar*. Tunahitaji *solar* katika shule hizi za Kata ili kiwe kivutio kwa walimu wetu isaidie wanafunzi wetu angalau waweze kujisomea usiku ili matokeo yawe bora zaidi. Kama fedha hizi zimekwishatumika naomba sana kwa ushirikiano na *REA* wajaribu kutafuta fedha na kufanya mpango mahususi kwa ajili ya kuzipelekea shule hizi *solar*. Walimu wa vijijini shule nyingi za kata ziko vijijini wangependa kujisikia sawa sawa na wenzao wa mijini ambao kuna umeme. Kupeleka *solar* kwenye shule moja, walimu wakiangalia *TV* kama wana kompyuta wanaweza kuwa na kompyuta yao na kuweza kuchaji simu zao. Hakuna kufikiria kutoroka au kukataa kwenda kwenye shule ile. Shule nyingi za Kata wanapata walimu lakini wanashindwa kwenda kwa sababu ya kukosa umeme. *REA* ningependa watusaidie kupitia mpango wa *Solar*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Wizara hii kutokana na Sheria hii ikipita ni kwamba naomba sana Sheria hii isije ikasababisha miradi ambayo imeanza au inayoendelea isije ikapungua kasi ya utekelezaji. Nafahamu na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri baadhi ya vijiji vyangu vimeingia kwenye mpango wa *MCC* na naomba sana Sheria hii isije ikachelewesha utekelezaji wa mradi huu. Nafahamu kuna

vijiji vya Ulumwarwa, Emirama, Mwamashimba na Sungu kwenda Mhande lakini vilevile kwa sababu utapita karibu sana na vijiji ambavyo havijaguswa ambavyo Mheshimiwa Waziri, naomba aviandike, ni Kijiji cha Ilula, Shirima na kijiji cha Lunele. Nitashukuru sana kama mradi huu utaingiza vijiji hivyo. Hata nisipokuwepo kila utakapopita kwenye barabara hiyo watakupigia makofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema naunga hoja mkono hoja hii ilimradi haya niliyoomba hasa kwa upande wa *TANESCO* yatekelezwe. Bado tunaihitaji *TANESCO* tena sana na hiyo ndiyo mali yetu na roho yetu na kwa sababu ya mfadhaiko tu ndiyo maana tunakubali Sheria hii ipite. Tunaomba sana wajirekebishe na watusaidie na kwa kweli ni aibu mzazi kumua mtoto wake, ni jambo la aibu. Lakini hatuna njia, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PHILEMONI NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu. Najua wananchi wengi wana mashaka na huu muswada na kwa kuwa matumaini yao ni kwamba wanataka gharama za umeme zishuke kwa sababu gharama za sasa ni watu wachache sana wanaoweza kuzilipa. Matatizo yanakuja kwa sababu ya mzigo mzito ambao *TANESCO* wamebebishwa na wanasiasa. Mnakumbuka sio siku nyingi *NET GROUP SOLUTION* kutola *South Africa* waliingizwa *TANESCO* kwa bunduki na wakawavunja moyo mpaka wafanyakazi wa *TANESCO* ambao walikuwa wana mori mzuri wa kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka wazi watumiaji wa *TANESCO* ni wachache sana. Mzigo wote wa kulipa madeni *TANESCO* wanalipa wateja wa *TANESCO*, hawalipi wananchi wengine wote kama tunavyokopa mikopo ya barabara, mikopo ya elimu, tunachangia *treasury* na tunalipa. Lakini inapokuja *TANESCO* ni sisi ambao tunatumia umeme peke yetu ndiyo tunaolipa umeme. Mimi ningeomba ili *TANESCO* iweze kupunguza bei na iweze kuingia kwenye ushindani wa wawekezaji ambao tunatazamia watakuja, Serikali ichukue madeni yote kuanzia sasa ili *TANESCO* iwe *at per* na wale watakaokuja na iweze kufanya kazi yake sawa sawa. Kama tutaendelea kuwaachia mzigo na kuwapa ruzuku kwani naamini Serikali yetu inapesa sana; kama inaweza ikawalipia wawekezaji wa Reli kuwalipia mishahara itakuwaje ishindwe kuwalipia *TANESCO* ili wananchi wapate umeme? (*Makofi*)

Kwa hiyo, Serikali ina pesa, tusije tukaambiwa haina pesa, ina pesa nyingi na inakopesha mpaka wawekezaji. Kwa hiyo, hiyo ni dosari moja na nasema awamu ya tatu ya Serikali yetu imeingiza nchi hii katika matatizo makubwa. Mikataba mibovu mpaka kugawa nyumba zetu ambao ni urithi wetu kwa watu wachache kuwagawia bure nyumba za *Oysterbay* kiwanja chenyewe ni zaidi ya shilingi milioni 200 mtu anapewa kwa shilingi milioni 20. Ni mikataba ya Awamu ya Tatu na ile imepewewa kuwafanya viongozi, ile ni rushwa inayowafanya viongozi wasiweze kuisema Serikali au kuwasema viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawakaribisha wawekezaji tusiwe na uoga wa kusema kwanini watakuja hawa pale. Sisi tuna uwezo wa kuwagiwa maeneo ambayo watakwenda. Sio kwamba tutaleta wang'ang'anie hapa mjini kwa kuwa wanaona kuna

pesa. Tutasema wewe umekuja utakwenda Ngara, wewe umekuja utakwenda Lindi kama ARTUMAS alivyosema wewe unataka kuwekeza nenda Tanga, Dodoma au wapi. Itakuwa ndiyo sisi tunapanga anayetaka afanye asiyetaka aende zake. Sisi Wabunge na Watanzania kwa ujumla *mini-power projects* za vijijini kwetu maana umeme una njia nyingi za kuzalisha na Tanzania tuna utajiri wa jua kali, upepo. Kwa hiyo, tunaweza kutumia *wind mill* tukapata umeme, tukatumia *solar*, tukapata umeme hata vijijini *overnight* unakuta vijiji vyote vina umeme. Maana ile *mini-project* ni kitu kidogo sana wala uwekezaji wake sio mkubwa ni kwamba tunafikiria makubwa lakini tunaacha kufikiria jambo hili, hata *generator* ya kilowati 200 inatosheleza kijiji kidogo.

Lakini tunang'ang'ania kusema kwamba ni lazima *TANESCO* au Serikali ifanye na sisi tuji-*organise* katika vijiji vyetu tujaribu kujisaidia wenyewe na tuone tunafanya nini. Hii *monopoly* iliyokuwa nayo *TANESCO* ilikuwa ni mbaya. Kwa mfano, kile kiwanda cha *TPC* Moshi kwa kuchoma tu takataka za miwa wana-*produce* kilowati 12, wao wanatumia 2 tu. Miaka miwili wameshindwa kuuza umeme ili hata usaidie watu wengine na ni wangapi wanaweza. Sio lazima tu-*produce* kilowati 100 au 200 hapana! Hata nusu kilo itasaidia kijiji na sehemu kubwa na matatizo yatatutoka. Tusiwe na wasiwasi, nadhani hii ni njia mojawapo ya kuwawezesha wananchi wa Tanzania wawekeze katika umeme na wao wawe matajiri waondokane na umaskini. Ni njia mojawapo.

Mwenzangu kama bwana Mangi kule kwako kuna maporomoko ya milima, mito, ukitaka kutengeneza umeme ni kazi ndogo tu. Ukiwaambia wana-Siha hutachangisha utakuwa una umeme wa kutosha katika Jimbo lako bila hata kuhangaika na *TANESCO*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge upo mbali na *microphone*!

**MHE. PHILEMONI NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sasa narudi kwenye *mic* na mimi niendeleo na hoja yangu. Nilikuwa namtazama Bwana Mwanri maana yake jana alitupa *philosophy* ya akina *Karl Max* hapa ikanishangaza kidogo. Wawekezaji hawa ambao wametulangua ambao sasa hivi wapo katika nchi ile ni marufuku kwao, watoto au uzao wao kuwapa huu mradi. Wale tuwafukuze kabisa na tuwakatae kabisa, waje wanya wenye nia njema. Maana yake hawa wameshatuibia vya kutosha na kama tutaendelea kuwakaribisha na tuwaambie wakae. Kwa kweli tutakuwa tumejimaliza wenyewe bila kutaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ni tajiri na ninasema inaweza kuliongezea taifa pato. Sasa hivi inalipa zaidi ya 90 *percent* ya mapato yake kwenye madeni. Kama ingekuwa haina madeni pato la taifa lingekuwa ni kiasi gain? Na miradi ya *TANESCO* mingine kama sasa tuna matatizo ya miti ya umeme waliiuza kwa mtu. Kwa nini wasirudishe lile shamba likarudishwa ili tusije tukaanza kuagiza miti ya *TANESCO* kutoka *South Africa* na sisi miti iko hapa Tanzania. Kwa kweli hainipi hoja nzuri katika kichwa changu. Kwa kweli sio vizuri kabisa. Lazima tujaribu tutafute njia ya kurudisha lile shamba, kama hakuna waanze shamba jipya la kupanda miti kwani leo si tuna miaka mingine mingi ya kwenda. Huko mbele tutanunua miti kutoka *South Africa*, mpaka lini? Na sisi tunataka umeme Tanzania nzima tunasema Tanzania *even two percent* ya nchi

nzima haina umeme. Kwa hiyo, *need* ya miti iko bado sana. Ningeomba *TANESCO* ifanye mpango wa kurudisha lile shamba la sivyo waanze shamba jipya la kupanda miti ili tusiendeleo kupata hasara.

*TANESCO* katika *connection charges*, mtu unatakiwa mpaka ulipe laki tano halafu siku wakitaka kukata umeme japokuwa wewe ulichangia wanakata na ile yote. Mimi naiomba Serikali kama tunachangia miundombinu ya *TANESCO* tuwe *share holder* wa kampuni zile. Pesa zinunue *share* katika *TANESCO* ili wajue na sisi tuna *stake* katika ile kampuni kuliko mtu kulipa pesa nyingi namna hiyo halafu zinakwenda bure wala hujui zinakwenda wapi, wala hurudishiwi, wala hufanyi chochote. Kwa hiyo, mimi naomba zile pesa ambazo tunatoa kwa *connection charges* na kama unataka *three phase* inafika mpaka milioni moja, iwe ni *share* zako katika kampuni ya *TANESCO* na wajue hivyo. La sivyo ni jukumu lao kuleta umeme mpaka kwenye nyumba yako, watu wa Posta wanafanya hivyo mpaka kichwa cha simu wanakuletea halafu ndiyo wanaanza kukutoza. Kwa nini *TANESCO* wanatutoza kabla hawajatuletea umeme ndani? Hili ni kosa, labda tuseme ni kwa sababu ya umaskini walionao, shauri ya madeni waliyokuwa nayo. Lakini kama Serikali ingekubali kuyaondoa yale madeni wanaweza kupata faida kubwa na wakachangia pato la Taifa na wote tukafaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu kabla hata hatujawakaribisha wawekezaji, zile sehemu zetu zilizo pembezoni karibu na Zambia, Burundi, Uganda au Kenya ni vyema tukakubaliana na nchi zile tukapata umeme wa majirani ambao utakuwa rahisi kuliko wa wawekezaji ambao watakuja hapa nchini. Kwa hiyo, tungejaribu sana kuzungumza na Zambia tukapata umeme ambao wana umeme mwingi wa kutosha ambao ungetupunguzia matatizo mengi sana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nipigiwe kengele nyingine naiunga mkono hoja na kama masahihisho ya Wabunge yatafuatwa nadhani Watanzania watafaidika na umeme utateremka ili mtu wa kawaida aweze kupata isiwe ni *luxury* kwa watu wachache. (*Makofi*)

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada ulio mbele yetu hapa. Naomba kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kuweza kuchambua na kukubaliana na mapendekezo mbalimbali ambayo yamependekezwa na Wabunge na kuweza kuuboresha Muswada huu. Nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamekwishazungumzwa na Wabunge wenzangu na mimi napenda kusema kwamba kama tunataka maendeleo, kama tunataka kufikia malengo yale ya milenia ni lazima wananchi wawe na umeme na umeme isiwe kama ni kitu ambacho wewe ni lazima uwe nacho, lazima uwe na nafasi fulani. Kila mwananchi awe na umeme na umeme pia kama utakuwa unapatikana hata nyumba bora wananchi watajenga kwa sababu itakuwa kwamba mtu ataona vibaya wenziwe wakiwa na umeme na yeye nyumba yake si bora. Kwa hiyo, ingeweza hata kutuboreshea makazi na mazingira. Mazingira yanaharibika kwa sababu tunakata kuni kwa ajili ya kupikia na

kwa ajili ya kumulikia ndani ya nyumba. Kwa hiyo, suala la kuwa na umeme ni muhimu na sehemu ya mahitaji muhimu kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule nyingi vijijini, tuna miradi mingi vijijini, wataalamu wa ugani wako vijijini, hivi ni nani ambaye anaendelea amesoma kwenye chuo ambacho kina umeme, kina kila kitu na huduma muhimu lakini anakwenda kukaa mahala ambapo hakuna mwanga? Ndiyo maana tunapata tatizo kwamba kuna maeneo mengine wataalamu hawataki kwenda kwa sababu wanakuwa nje ya dunia, hawasilizi habari zilizoko duniani. Kwa hiyo, anaona bora asiende kwa kukosekana umeme kuliko akae mahali ambapo hapati habari zozote za duniani wakati alikuwa anasoma shuleni na amejifunza mambo mengi anayohitaji kuyafanyia kazi. Hawezi kuangalia TV, hata redio yenyewe mawe shida, hawezi hata kuwasiliana na wenzie, kwa hiyo, inakuwa ni kazi. Ni umeme tu utakaokuwa mkombozi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zilizofunguliwa, tunazungumza kwamba wanafunzi ni lazima wasome somo la kompyuta, lakini watasomaje kompyuta wakati hawana umeme? Kwa hiyo, hawa wanafunzi wanaosoma shule za vijijini wao wanakuwa tofauti, wakati wote tunataka wanafunzi, watoto wote wapate elimu bora na kila mtoto apate elimu sawa na mweziwe. Lakini hawa wanasoma huko, hawajawahi kuiona hata kompyuta kwa sababu umeme haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kutoa ushauri kwamba tuhakikishe kuwa umeme unafika vijijini kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa na umeme wa *solar* ili shule zetu ziweze kuwa pia ni shule za kisasa, waweze kusoma ili hao wanafunzi wanapomaliza shule za sekondari, wanakwenda *High School*, wakienda Chuo Kikuu basi wawe sawa na wenzao waliokuwa wanasoma kwenye maeneo ambayo yana huduma muhimu kama huduma za umme. Kwa hiyo, shule hizo ziweze kuwa na umeme wa *solar* au jenereta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia huduma za afya, tunasema Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na huduma ya afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa zahanati. Hivi itawezekanaje wakati hata hizo huduma zingine zinashindikana kufanyika kwa sababu ni giza? Hata tumeambiwa kwamba upasuaji mdogo utafanyika labda kwenye vituo vya afya au huko kwenye zahanati vijijini. Zitafanyikaje kama hatuwezi kuboresha huduma za umeme kwa njia mbalimbali? Hilo nalo ni muhimu ili tuweze kuboresha huduma za afya ambazo zitapunguza vifo vya akina mama wajawazito, ni lazima tuhakikishe kwamba huduma za umeme zinaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo kuna watu mbalimbali yakiwemo mashirika ya dini, wamejitahidi sana kutafuta vyanzo vya umeme wa maji au maporomoko. Kwa mfano, Njombe Lupembe kuna watu wa *Safer Matembwe* wameweka umeme vijijini. Tuna watu kwa mfano hospitali ya Ikonda wameweka umeme. Lakini yawezekana maeneo mbalimbali yapo na umeme huu walikuwa labda wanazalisha ambao unazidi mahitaji yao ingawaje kwa mfano, Ikonda ule umeme wao hautoshi mahitaji. Lakini kuna mifano kama hii ambayo labda walikuwa wanazalisha umeme, labda unazidi mahitaji, lakini kwa sababu sheria haikuwepo ya kuwaruhusu kuzalisha umeme wa ziada

na kuuza hawakufikia malengo yao. Kwa hiyo, tungeanza na hao kuwaimarisha. Kama anaweza kuzalisha umeme wa vijiji viwili, basi azalishe vijiji viwili au vitatu kufuatana na eneo ambalo anaweza kulifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maporomoko au mto ambao unaweza kutuzalishia umeme, kwa mfano, Makete, tuna Lumakanya ambao unaweza kutoa megawati 220 ambazo tayari na *TANESCO* imekwishaufanyia uchunguzi ikagundua kwamba umeme huo upo na wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara yake alikwenda kule akauona. Kama tungeweza kuzalisha huo umeme ungeweza kumaliza mahitaji yote ya Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vijana wataachaje kutoka nje ya Wilaya kwenda kutafuta mahala bora kama kila mahala kuna giza na hawawezi kuanzisha miradi ya kiuchumi ile inayowawezesha wakae kwenye Wilaya zao. Tutapambanaje na UKIMWI kama hatuna vyanzo vya mapato na tutapata vyanzo vya mapato tu kama tutakuwa na umeme.

Vijana watapasua mbao, watoto wa kike watafanya miradi mbalimbali ambayo siyo miradi ya kutumia nguvu kubwa kwa sababu kama kuna umeme, unaweza kurahisisha kazi za kufanya, unaweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Lakini kwa sababu hakuna umeme ndiyo maana tunaona miji yetu inajaa vijana, wanahama kutoka vijijini kwa sababu hakuna huduma muhimu kama huduma za umeme. Kwa hiyo, tukianzisha hilo, tutaona kwamba vijana wengi wataendelea kukaa vijijini. Hakuna kijana asiyetaka kukaa kwao, lakini atakaeje huko wakati anajua kwamba kuna mahali kwingine ambako kuna huduma muhimu na akienda huko anaweza akapata maisha yake na wakati mwingine hayo maisha anayotegemea kwamba yako mjini hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kuwafanya vijana waweze kukaa vijijini, ni lazima tuboreshe huduma za umeme na kuhakikisha kwamba umeme huo unapatikana. Umeme kama wa maporomoko ya Mto Luhuji unaweza kutoa umeme mwingi sana na jana nilikuwa nasikia Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu swali hapa, alisema ule mtambo uliopo Njombe, utahamishiwa kwenda Mafia. Nikajihoji mbona Ludewa hakuna umeme? Kwa nini mtambo unakwenda mbali wakati maeneo yale ya Mkoa wa Iringa hayana umeme? Nilipenda nijue hilo, kwa nini huo mtambo unatoka Njombe unapelekwa kwingine wakati tuna maeneo mengi sana hayana umeme? Ludewa iko gizani na huduma nyingi hazifanyiki kwa sababu jenereta inatumia mafuta mengi, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiboresha huduma za umeme, vijiji vyetu vingi tulivyonavyo ambavyo ni vijiji miji, kwa mfano, Ikonda, Bulongwa, Lupila, mahali kama Isimani, Idodi, Pawaga, Nzii, Kiponzelo, Wasa, mahala kama Mbuyuni, Mtandika, Bomang'ombe, kule kote ni maeneo ambayo yanaweza kuwa ni miji midogo kwa sababu huduma za umeme zitakuwepo. Wananchi wataingia katika shughuli za kiuchumi na wanaweza wakazalisha viwanda vidogo vidogo. Sisi tuna matunda yanaoza tu huko, msimu wa matunda yanaoza, hatuwezi kusindika kwa sababu hatuna umeme.



Mimi nafikiri kwamba kama vyanzo hivi vya umeme vingeweza kutumika vizuri tungeweza kupata umeme wa kututosha kabisa. Tunaweza pia kupata umeme kutoka mto Rufiji, tukaweza kuwa na umeme ambao unatosheleza. Lakini umeme huu nafikiri kwamba vijijini kama nilivyosema, tungeanza kutafuta watu wale wanaowezeza wawekeze kwa kufuata kanda na kujua vijiji vingapi kila Wilaya vimepata umeme. Kama hatufanyi hivyo tutakuta uwiano haupo, sehemu nyingine zitapata umeme, utakuta vijiji vingine vimepata na sehemu zingine hazina. Sasa nafikiri kwamba tuanze kufikiria uwiano, tuna viwanda, je, huu umeme kila Wilaya ni vijiji vingapi vimefikiwa na tumesema kwamba kuna vyanzo mbalimbali; kuna maji, jenereta, kuna *solar* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, shule zote tuhakikishe kwamba shule inapooanza kujengwa, basi ule mchango wa wananchi wanapochangia sijui matofali, ujenzi, Serikali ihakikishe kwamba umeme unawekwa, iwe kama sehemu ya mahitaji muhimu. Watoto wetu wanakaa gizani, sasa vijijini huko ikifika giza, kazi ni nini? Kila mtu gizani, saa kumi na mbili giza limeingia! Na sisi tulioko mijini, kuna *recreations*, mtu hana mahali pa kwenda kuburudika, tunafanyaje? Kwa sababu kama kuna umeme, kutakuwa na vituo vya maendeleo, kutakuwa na *community centres* ambako watu hubadilishana mawazo. Kwa hiyo, tukijenga shule Serikali ihakikishe kwamba inachangia kwa kuwawekeza umeme kama umeme wa *solar*, kwa njia yoyote itakayoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba Wizara ihakikishe kwamba viwanda kwa mfano, Mufindi kuna wawekezaji wa Kitanzania ambao wanataka kuwekeza katika Kiwanda cha Chai. Lakini wanashindwa kwa sababu ya umeme. Mahala ambako tunaona ni *potential* kwa ajili ya miradi mbalimbali, basi huko kuangaliwe kwanza kwa sababu kuta-*create* ajira. Tunahitaji ajira milioni moja. Kama tutaweka umeme, tutahakikisha kwamba hiyo ajira tutaipata na akinamama wanaweza kupata pia ajira kwa kuanzisha viwanda vidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda niseme kwamba naunga mkono tena hoja hii na nina uhakika kwamba yale niliyoyasema yatazingatiwa ili maisha bora kwa Mtanzania yaweze kupatikana na pia tuweze kupunguza tatizo la UKIMWI kwa sababu vijana watakuwa hawahami kutoka vijijini kwenda mijini, watapata ajira huko kwa sababu watakuwa kwenye viwanda vidogo vidogo. Asante sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o. Kabla sijamwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, niwakumbushe tu kwamba jioni, tutakuwa na Mheshimiwa Shally Raymond, atakuwa msemaji wa kwanza, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Omar Qwaangw', Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa John Lwanji. Kama mnavyojua tutakuwa na nafasi nne kwa sababu Mheshimiwa Spika, amesema tutachangia kwa saa moja. Orodha niliyoitaja, ujanja ni kuwahi. Sasa mwisho namwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kupata nafasi ya mwisho ya kuchangia katika kipindi hiki cha mchana. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuwa ni Muswada ambao umezunguka zunguka sana. Lakini naomba niambie Serikali kitu kimoja, Serikali isipende Wabunge waseme “ndiyo“ kila wakati. Ni vyema Serikali ielewe kwamba Wabunge wanaposema “hapana“, wanasema “hapana“ wakiwa na hoja za msingi. “Hapana“ ni neno zito na zuri zaidi kuliko “ndiyo“. “Hapana“, Waingereza wanasema *is a very powerful no!* Na mtu akianza na hapana, mara kwa mara anaishia kwenye ndiyo kwa sababu hapana inaambatana na sababu za msingi. Tulipokuwa tunasema hapana, tulikuwa hatujaridhika na jinsi ambavyo Muswada ulivyokuja. Muswada ulikuwa hautupi dalili zozote za kuirekebisha *TANESCO*. Muswada huu ulikuwa hautuonyeshi watafika fikaje kwa wananchi wetu walioko vijijini ambao ndiyo asilimia kubwa ya wapiga kura wa nchi hii. Kwa hiyo, na sisi walitugusa kwenye *nerves*, tukaona kwamba tuseme hapana! Baada ya Waziri kushirikiana vizuri sana na Wabunge, alifanya marekebisho ambayo tumeridhika nayo, lakini hata hivyo, tuna maangalizo mengi sana ya kumpa ili aweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania wa mwaka 2008 siyo Mtanzania wa mwaka 1947. Hilo lieleweke kabisa kwa Serikali yetu. Mtanzania wa kipindi hiki anaijua haki yake, anaijua nchi yake, ana uelewa mkubwa, anafahamu kipi kinamstahiki yeye kama Mtanzania kwenye nchi yake na kipi si chake! Watanzania wa sasa hivi wana mwangaza mkubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali pamoja na marekebisho haya ambayo imeyafanya, lakini itakapokuwa kwenye utekelezaji, Serikali itekeleze kweli kama ilivyorekebisha. (*Makofi*)

Naomba niongelee mageuzi ya kiuchumi kidogo, lakini kiulimwengu. Mimi napenda kusoma vitabu na niseme ukweli, nimeiga kusoma vitabu kutoka kwa Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera. Maisha ya Mheshimiwa John Samwel Malecela ni kusoma vitabu na ukikaa na mwenzio anayesoma vitabu, nawe utasoma vitabu. Nimesoma kitabu cha historia ya mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi ya kiuchumi ulimwenguni yalianzia Ulaya siyo Marekani, Ulaya Karne ya 14 mpaka karne ya 17. Kilitokea kipindi kikaitwa kwa lugha ya Kiingereza *Renaissance* - mageuzi ya kiuchumi. Ikatokea *reformation*, mfumo wa kiuchumi ukaenda kwenye viwanda na ndiyo sasa ulimwengu ukaanza kunyanyuka. Mageuzi ya kiuchumi yaliletwa na *awareness*, yaliletwa na watu kufahamu haki zao. Lakini mageuzi yale yalianzia Ulaya, yakaenda yakasogea, yakasogea, yakafika mpaka huku kwetu sasa. Tuko kwenye kipindi cha mageuzi ya kiuchumi. Hakuna mageuzi ya kiuchumi yatakayofanikiwa bila ya kuwa na umeme wa uhakika. Na hata kule Ulaya viwanda vilifanikiwa tu kwa sababu kulikuwa na umeme wa uhakika. Na sisi tunakubali kwamba sasa hivi ni wakati muafaka tufungue milango, kama utekelezaji utakuwa mzuri, tuwe na umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye *TANESCO*. Hapa nitaongea kidogo. Hakuna nchi yoyote duniani kwa uelewa wangu ambayo inaishi ikampa mwekezaji ahodhi nishati ya umeme wa nchi yake, haipo! Na ukiona nchi inafanya hivyo

inampa mwekezaji *a hundred per cent* kuhodhi nishati ya umeme, basi nchi hiyo itakufa! Ni lazima sisi wenyewe Watanzania kwanza tujihakikishie kwamba *TANESCO* iko imara. Kwamba hata wale wawekezaji tukikwaruzana nao, wakifunga mizigo wakiondoka, nchi haiwi kwenye giza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano. Tuliingia mkataba na *South African Airways*, tukaunganisha *Air Tanzania* na *South African Airways* tukaenda nao, tukagombana nao. Nashukuru nilikuwa kwenye kamati ya kuunda Shirika jipya la Ndege. Akakamata ndege yetu kule *South Africa* akasema msipoleta shilingi milioni 500 siachii ndege yenu! Tukigombana na hawa watu kama tukiwapa umeme wetu huo, yaani nishati, wao ndiyo waende wakaishikilie, tukigombana nao wakitoa mitambo yao, wakiondoka, nchi itakuwa wapi? Ni giza! Nchi kuwa kwenye giza, ni nchi kufa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba lazima *TANESCO* lifufuke. Naomba niwakumbushe kwenye miaka ya 1970 jamani alikuwepo Mheshimiwa Alnoor Kassam na marehemu Salvatory Mosha, wakiwa wanaongoza *TANESCO*. Suala la nishati waliliweka kwenye *donors conference*, wakalitangaza ulimwengu mzima. Wakaeleweka, wakapewa pesa, *TANESCO* ikawa ni kati ya mashirika bora katika Afrika. Tukumbuke wenzetu walifanyaje fanyaje! Kipindi hicho *TANESCO* ilikuwa inajulikana kwa *World Bank Standard*. Hawa wenzetu walitangaza miradi yao, walitangaza sekta hii kila mahala. Namkumbuka Alnoor Kassam nilikuwa bado msichana mdogo, namkumbuka na marehemu Salvatory Mosha. Ndivyo tunavyopaswa kufanya sasa hivi.

Naendelea bado na *TANESCO*. Tutailaumu *TANESCO*, lakini lawama ya *TANESCO* ni ndogo. Lawama kubwa ni ya kwetu! Ndiyo! *TANESCO* ina lawama zake! Mimi naomba nizungumzie kitu kimoja. *TANESCO* nayo ilikuwa na mpango wake wa utekelezaji. Ilikuwa na *Power Sector Master Plan*. Ilikuwa na miradi yake imepanga Mchuchuma ya kutumia makaa ya mawe, ilikuwa imepanga Luhuji *Hydro*, ilikuwa imepanga Lumakali *Hydro*, ilikuwa imejipangia Lusumo *Hydro* na miradi mingine midogo midogo. Lakini kulikuwa na *interruption* kila wakati. Inaanza, tayari kunatokea mradi wa dharura, Inaanza kunatukea hiki mara kile! Kwa hiyo, haikuachiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali niwasihi sasa mshirikiane vizuri na *TANESCO*, mpango huu usiendelee kupuuzwa. Miradi yao waliyojipangia wenyewe, nao wapewe nafasi, wasipuuzwe na *master plan* zao. Kusiwe na *a lot of interruption in between*, hapo kati kati tayari wamekatishwa! Kwa kweli mipangilio yao, ukisoma *master plan* ya *TANESCO*, mimi napenda kusoma vitu, walikuwa na mipango mizuri sana. Namsihi sana Mheshimiwa Waziri katika hili. Akaangalie vizuri na ashirikiane nao ili twende. Na ni vyema miradi hii tukaitangaza kama ambavyo akina hayati Salvatory Mosha walivyotangaza, tulitangaze ulimwengu mzima ujue! Tushirikiane na wenzetu wa *SADC*, tushirikiane na *AU*, tushirikiane na *East African Community*, hakuna ubaya. Lakini huenda tukakomboa nchi yetu upande wa *TANESCO*. Mimi nia yangu ni kwamba hata wakiwepo wawekezaji lakini Shirika langu, Shirika mama la nchi yangu liwe na nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo kwa masikitiko. *TANESCO* imekuwa kama dodoki – *sponge*. *TANESCO* muda mrefu imekuwa inameza mipango mizuri ya nchi hii. Inameza mipango yote mibaya ya nchi hii tena wakati mwingine kwa kuagizwa tu, “ingia mkataba!” Eti “usikatae!” *TANESCO* inameza mpaka mipango tata! *TANESCO* anameza! Ni vyema Serikali ikaangalia katika hii mipango, ile mipango ambayo tunaiona haifai, basi tuiache, tuendelee na mipango ambayo ni mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali. Nina maswali ambayo naomba niulize. Tumekuwa na miradi mingi ya dharura. Tumekuwa na *IPTL*, ikai-*cost TANESCO capacity charge* ya 3.5 kwa mwezi, Songas 4.5 kwa mwezi (nikikosea Mheshimiwa Waziri atanirekebisha), *Dowans* wote mnajua. Sasa maswali ninayokuwa nayo, naomba Serikali itueleze Watanzania wote mambo yafuatayo:- Je, mikataba ya haya makampuni itakapofikia mwisho, Serikali mtaendelea kuwaongezea tena muda baada ya ukomo wao? Kuna faida na hasara gani ya kuendelea kuwa nao? Kama inawezekana, tunaweza tukaisitisha hii ambayo inakwenda mpaka 2015?

Lakini kuna *AILSTROM* iliyopo Mwanza, ilimaliza mkataba wake Machi, 2008. Na sasa hivi wote mnafahamu, Nyumba ya Mungu imekwishaanza kufurika, Kidatu imefurika, Mtera imefurika. Jana usiku nimeongea na Meneja, karibu wanataka kufungua milango. Kuna umuhimu wa kuendelea na *AILSTROM* iliyoko Mwanza ambayo imemaliza kazi yake? Hilo nitaomba kidogo mnisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambalo ndilo linanisumbua, Serikali itueleze vizuri mpango wake wa kufufua *TANESCO*. Wametueleza kwamba Serikali itatoa *1.6 trillion* kufufua *TANESCO*. Je, huu mpango ukoje? Watanzania waelewe, Waheshimiwa Wabunge waelewe, wafanyakazi wa *TANESCO* waelewe. Kwa sababu nimekwenda kufanya *research*, tayari mpango huu umeanza awamu ya kwanza.

Lakini sikuelewa, itabidi hapa Waziri anijibu vizuri. *TANESCO* wamekopeshwa takriban shilingi bilioni 300 na mabenki wakiongozwa na *Stanbic*. Serikali ilichofanya hapo ni ku-*guarantee* tu, lakini deni hili la *around 300 billion* italipa *TANESCO* pamoja na riba kubwa. Sasa bado nataka kuuliza; je, ndivyo tunavyoifufua *TANESCO* hivyo? Ndiyo ile *1.6 trillion* tuliyosema kwamba itatolewa ili *TANESCO* ifufuke? Mimi hapo nitaomba tuelezwe vizuri. Kama ndiyo tunaifufua *TANESCO* kwa njia ya kuifanya ikope, sisi tu-*guarantee*, nitaomba kusema kwamba tutakuwa hatujaifufua *TANESCO*. Nitaomba katika hili Serikali itueleze vizuri, inawapa *TANESCO* vipi *1.6 trillion*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bei ya umeme wenzangu wamelizungumzia. Lakini juzi nilitwa na wapiga kura wangu, nikamwaga Mheshimiwa Spika. Wapiga kura wangu wamesema wamechoka, wanaishi kwenye milima kule Kirangare, kuna miti ikifika saa tisa ni giza, inabidi walale, hakuna umeme. Lakini pia nguzo zimepita, wakitaka kuvuta *service line*, wanalipa 470,000/= mpaka 500,000/=. Jamani Mtanzania gani anaweza? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* anijibu na Watanzania wanakusubiri hapo. Je, Muswada huu ambao utakuwa sheria utawatoa hapo? Wateremshe, wafanyie maisha yao yawe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye angalizo zito kweli na Mheshimiwa Waziri hapa ndipo utakaposimamia au ndipo utakapoangukia. Aina ya wawekezaji wanaokuja, kuna wenzetu hapa Tanzania tayari wanaanza kukarabati vimitambo vyao! Hivi walivyokusanya kusanya juzi kwenye mambo ya *Richmond* na kadhalika. Wanangoja tupitithe sheria waingie hapa, hatuwataki! Tunataka wawekezaji wa uhakika.

Waje wawekezaji wapya, waangaliwe tabia zao kimataifa, waangaliwe uwezo wao kimataifa, waangaliwe sifa zao kimataifa na wagonganishwe! Na mrudi mwende mkaangalie walikotoka je, huko wana sifa stahili za kuingia kwenye nchi yetu? Isije nchi yetu ikawa ni kichwa cha mwendawazimu, mwenye uwezo, asiye na uwezo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii lakini natoa angalizo kubwa hilo kwamba wawekezaji wanaokuja waangaliwe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kama mnaovyoona Waheshimiwa bado tuna dakika tatu, nne. Nilipata ombi maalumu kutoka kwa Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, akinihakikishia kabisa kwamba dakika 3 zinamtosha. Kwa hiyo, moja kwa moja namwita Mheshimiwa Hamza Mwenegoha.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujua sasa kwamba kuna watu wanne na mimi naomba Mungu, mmoja achelewe jioni, naomba nifanye pata potea, ningoje jioni. Asante!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nakubali pata potea ya Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, lakini nimhakikishie kabisa kwamba jioni hatapata nafasi. Kwa sababu kama nilivyosema labda kama Mheshimiwa Spika, ataangalia na kuona hali itakavyokuwa wakati huo, lakini tuna saa moja kwa lengo la Mheshimiwa Waziri kuanza kujibu hoja nyingi ambazo zimetolewa kwa siku hizi karibu mbili na kitu. Wachangiaji wetu, wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Lyamba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati yuko hapa, Prof. Raphael Mwalyosi. Kuna wito umetolewa kuwa Maprofesa mnaofanya nini hapa? Tutakusikia jioni! Na mwisho Mheshimiwa John P. Lwanji. Kwa hiyo, baada ya maneno hayo, shughuli zilizopangwa leo asubuhi zinaishia hapa. Naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi leo jioni saa 11.00.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Samwel J. Sitta) Alikalia Kiti.*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba tumesambaza nyongeza ya Orodha ya Shughuli za leo, hii ni kwa ajili ya kuwawezesha kuzipata hati ambazo kesho zitajadiliwa. Bila kuwa na nyongeza za Orodha ya Shughuli isingewezekana mgawiwe hati za kuwasilishwa Mezani. Kwa hiyo, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI ZA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2005/2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za mitaa (LAAC) kwa mwaka 2005/2006

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 (*The Electricity Bill, 2007*)**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya shughuli zetu za kuanzia jana ninayo orodha ya wachangiaji wa Muswada watano.

Mtakumbuka kwamba asubuhi nilisema kwamba ninao wachangiaji wanne na nimeamua si vema tukamwacha mmoja, kwa hiyo, wote watano watapata nafasi ya kuchangia, nao ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na atatufungia pazia Mheshimiwa John P. Lwanji. Namwita sasa Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:**Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii ya kutoa mchango wangu. Awali ya yote kabisa naomba niseme kwamba naunga mkono muswada huu. Muswada huu wengi wamechangia nami naungana nao na huenda pia katika hayo nitakayochangia nikarudia rudia lakini kuna yale ambayo ni muhimu sana na kama sitatamka mwenyewe sitaweza kupata amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia katika maeneo matatu; la kwanza ni lile la bei za umeme, la pili ni lile eneo ambalo hadi sasa umeme haujapatikana kuanzia tupate uhuru; na la tatu ni namna ambavyo tunaweza kupata umeme wa kutosha kutokana na vyanzo mbalimbali na zaidi sana nitajikita kwenye kile chanzo cha Nishati kutoka kwenye jua.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba kadri maendeleo yanavyozidi kuwepo watu wengi wanaona kwamba umeme ni muhimu sana katika kila nyanja, ni muhimu katika matumizi ya nyumbani na pia katika uchumi wa nchi.

Gharama za umeme zimekuwa juu kiasi ambacho wengi wetu au wananchi wetu hawawezi sasa kupata umeme huo, ukianza umeme wa nguzo na umeme wowote popote pale ambako unawekwa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni maeneo mengine yamekuwa yakitoa umeme kwa kulipia kupitia *LUKU*, umeme huu pia ni ghali sana. Leo tunaujadili muswada huu lakini mimi najiuliza maswali mengi, hivi kweli baada ya kupitisha Muswada huu baadaye ukawa sheria na wakaja watu ku-*invest* je, umeme huu utashuka bei? Hilo ni swali ambalo ningependa Serikali itueleze wazi kama kutakuwako na nafuu yoyote.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumesikia huko kwenye maeneo ya Shinyanga na Mwanza vikongwe wanauawa kwa sababu macho yao yanakuwa mekundu lakini tunaalezwa kwamba si kweli kwamba watu hawa ni wachawi, ni kwa sababu ya nishati duni ya kutumia kinyesi cha Ngo'mbe kama kukokea moto na vitu kama hivyo na kusababisha macho yao kubadilika. Endapo watu hao wangukuwa wamepatiwa umeme je, hayo macho yangekuwa mekundu, na kama hayangukuwa mekundu wangetuhumiwa kwa kuwa wachawi?

Mheshimiwa Spika, naomba tunapofikiria umeme vijijini tuwakumbuke hao na niseme wazi kwamba vyanzo vya umeme ni vingi na upo huu umeme kutoka kwenye jua. Lingekuwa jambo zuri sana kupeleka umeme wa jua kwa sababu hata shule zetu tulizojenga hivi majuzi katika kila kata na hata zahanati zetu zingepata umeme kwa urahisi zaidi. Tatizo ninaloliona hapa ni gharama za kuunganisha umeme huo au vyombo vya umeme huo bado ni ghali. Hivi kweli vyombo hivi haviwezi kuondolewa kodi ili umeme huo uweze kuunganishwa kwa bei nafuu na watu wenyewe wakapata umeme kwa gharama ambayo wanaweza kumudu?Utakuta kwamba hela za bajeti tunazipitisha hapa Bungeni, wote waliochangia wamesema kwamba wangependa kabisa wakaona *impact* katika shughuli za umeme je, Waheshimiwa Wabunge kwa nini basi Serikali isifanye juhudi na ikaamua kuleta bajeti hiyo na tukaamua kuwapitishia kama shilingi bilioni 110 tu kuunganisha umeme huko vijijini?

Mheshimiwa Spika, mimi naona hilo jambo tuna uwezo nalo sisi kama tutasema safari hii tunataka umeme uende vijijini pamoja na ile *percent* ambayo tutachangia lakini vifaa hivyo vifungwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba hadi sasa ni takriban watu laki sita tu ambao wameweza kupatiwa huduma ya umeme, laki 6 kwa Tanzania yenye watu milioni 36, huko kwingine inakuwaje. Kuna nchi ambazo tulipata nazo uhuru miaka inayokaribiana kama Malaysia, huko umeme siyo tatizo tena, wameupa kipaumbele na kote kuna umeme, kwa nini sisi Watanzania tusiamue kwamba umeme ni lazima uwepo kila mahali bila kuchagua mijini au vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia umeme wa kutoka kwenye jua au *solar* kuna njia zingine pia za umeme, hizi ni njia za upepo. Umeme huu hauna gharama sana, ni kiasi cha wasomi wetu watuambie kwamba upepo huu unafaa au haufai na hapo pia tunaweza kupata chanzo cha umeme, hivi kwa nini tusingumie umeme wa aina hiyo?

Mheshimiwa Spika, muswada huu umeanza muda mrefu sana kuzungumziwa lakini Wabunge tulipata tabu, baadhi yetu hatukuwa na wataalamu wetu wa kutushauri na hapa inarudi kwako kwamba huu ni wakati muafaka kabisa wa kutupatia Wabunge wataalamu wa kuchambua mambo na kutuelekeza ni kitu gani kinafaa au hakifai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni bahati tu kwamba Wabunge wenyewe wametafuta njia zao wakaweza kujadili na kuweza kurahisisha na hatimaye kuhudhuria katika Kamati ya Nishati lakini bila hivyo ingekuwa vigumu sana na usingeweza kupata mchangiaji kwa sababu jibu lilikuwa ni hapana, lakini namshukuru Mungu kwamba mpaka sasa wote tumeanza kuunga mkono na Bunge lote hili linazungumza lugha moja kutaka muswada huu upite.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya muswada huu kupita na Wizara ya Nishati na Madini itakapoleta bajeti yake hapa, kipaumbele kitolewe kwa umeme wa vijijini bila kuchagua kwa sababu hata nilipotoka Mkoani Kilimanjaro, unakuta kwamba kuna ndizi zinaoza lakini kungekuwa na umeme zingeweza kukaushwa na zikauzwa baadaye. Kama sasa hivi mvua ni kubwa ndizi zinaoza, tungekuwa na viwanda vidogo vidogo tungekausha ndizi hizo na zikatumika baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kahawa, sasa hivi *pulpary* ingefanyika katika kijiji kimoja. Mimi nina mfano hai kabisa, tulimwita kiongozi wa ngazi za juu kabisa kuja kutufungulia *pulpary* lakini siku hiyo hatukuwa na umeme na hatukuweza kufungua. Ilikuwa ni aibu tupu, laiti kama umeme ungekuwepo angeweza kutufungulia hiyo *pulpary*.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba umeme huu utakapoelekezwa huko usingojee tu mpaka kuwepo na viwanda, umeme uwepo na viwanda hivyo vitaibuka, itakuwa vigumu sana kama tukisubiri mpaka wananchi waanzishe viwanda. Naomba ile kauli kwamba wananchi waanzishe kwanza viwanda ndipo umeme ufuata, dhana hiyo iondoke.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia atakapokuja kutoa maelezo au ufafanuzi Mheshimiwa Waziri aeleze kama inawezekana sasa umeme huu ukawepo katika hospitali zote? Hii naisema wazi kwa sababu watu wengi wamekufa kwa sababu ya kufanyiwa operesheni kwa vibatari na nina mfano hai kabisa hata akiniuliza nitamweleza, jambo ambalo ni la hatari sana. Waziri atueleze kipaumbele cha umeme huo kitakuwa ni wapi.

Mheshimiwa Spika, tumeizungumzia *EWURA*, na wengi wamezungumza kwamba inaweza ikasimamia jambo hili la bei za umeme mara moja. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali hapa alisema Serikali haitatoa ruzuku mijini bali itatolewa vijijini. *EWURA* inaweza ikarekebisha vipi jambo hilo ambapo tunaambiwa kwamba hali ya *TANESCO* ni mbaya. Madeni ya *TANESCO* ni makubwa sana na yatalipwa kwa uchangiaji wa wale



wateja wa rejareja. Wakati unalipa bili yako utakuta kuna *capacity charge*, kodi na labda hiyo *capacity charge* ndiyo ina-cover pia hiyo *contribution* ya mteja mmoja kulipia madeni hayo. Wakati *TANESCO* inakwenda kukopa haikushauriana na mtu bali Serikali. Kwa nini Serikali isichukue hatua madhubuti kabisa ikafuta haya madeni kabla hawajatubebesha sisi mzigo huo?

Mheshimiwa Spika, inakuwa ni vigumu sana kwa sababu hatuoni sababu yoyote ya sisi kuendelea kulipia bila kujua hatima yake ni nini. Mimi mwenyewe juzi nilikwenda kulipa bili ya umeme wa *LUKU* na hiyo ni *pre-paid* lakini nilitoa shilingi elfu 50 *TANESCO* nikapewa umeme wa shilingi elfu 24 ina maana 26,000 zimekwenda kwenye *capacity charge*. Nimeandikiwa *EWURA*, na kodi, hivi kweli kuna haja gani ya kulipia mapema? Kwa nini wasitufungie wote mita ili tuwe tunalipiwa umeme baada ya matumizi?

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaumiza sana na ndiyo maana naunga mkono nikisema kwamba huenda muswada huu ukipita tukapata wazalishaji umeme wa namna na nyingine na wasambazaji wengine na wasimamizi wakawa wengine wakiungana na *TANESCO* inaweza ikarahisisha.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Serikali ina kazi kubwa sana ya kuwawekea hawa wawekezaji mazingira mazuri, kwa sababu wawekezaji wengi Tanzania wanaogopa sana kuja kuwekeza kwa ajili ya bei kubwa ya umeme na hao wanaokuja sasa wanakuja kuwekeza kwenye umeme, kama hawatawekewa mazingira mazuri ina maana pia na wao hawataweza kutupa bei nzuri ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba pia vyombo vyetu kama vile vya *PPRA* viweze kupewa meno ili inapokuja sheria wao waweze kusimamia na hata kubadilisha chochote kama vile kuwashikilia wale ambao ni *accountable for*, ili waweze kujua jambo fulani likienda vipi wao wapo pale kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu chombo hicho kilinyimwa haki au kilikuwa hakina uwezo wa kusimamia sheria na tuliona matokeo ya upungufu huo, hata *EWURA* yenyewe inatakiwa isaidiwe siyo waendeleo na kazi na wao wazidi kupandisha bei.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hayo naamini kabisa muswada huu ukipita tutapata umeme wa kutosha, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami kutoa mchango wangu mdogo katika muswada huu muhimu kwa maslahi ya maendeleo na kuleta maisha bora kwa Watanzania katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote katika Wizara na Taasisi ya *EWURA* na bila kuwasahau Wabunge kwa ujumla ambao wametoa mchango mkubwa sana katika kuboresha muswada huu, vinginevyo ulikuwa umekuwa katika hali ambayo ulikuwa

ukataliwe tena, lakini kwa leo umefikia kiwango cha hali ya juu sana, nawapongeza wote. Kwa kauli hii ya utangulizi bila shaka mnajua moja kwa moja kwamba nitatamka rasmi kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi sasa hivi wanafuatilia kwa umakini sana muswada huu. Hivi jana na leo nimeendelea kupokea *text messages* zikiulizia na kufafanua jinsi wanavyopata adha za kulipia umeme na gharama kubwa za kuunganisha nguzo za umeme.

Sababu kubwa ya kuniuliza ni kwa vile mimi katika Kata yangu ndiye ninayepakana na mtambo wa Kidatu katika Jimbo la Mikumi na ninaishi katika maeneo yale. Kwa hiyo, wana shauku kubwa katika Jimbo na nchi nzima kujua hatima ya muswada huu itakuwa nini.

Mheshimiwa Spika, swali kubwa wanalouliza baada ya muswada huu kupita kama alivyozungumza msemaji aliyetangulia, malipo ya kuunganisha umeme yatakuweje, kwa sababu tumekwishaelezwa kwamba kuunganisha nguzo moja ni karibu shilingi milioni 1. Ikiwa nyumba yako iko jirani na haihitaji nguzo ni laki 5, ikiwa ni nguzo mbili karibu milioni 2. Kwa mwananchi wa kijijini hali hii ni ngumu kweli kweli, kwa hiyo, mtazamo uliopo ni wazi wanafurahia sana *capacity charge*, kwa mikataba itakayofuata haitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, wanajiuliza pia kwamba je, Serikali imemaliza mbinu zote za kuweza kuwashawishi watu wale ambao wanafua umeme sasa hivi kama *IPTL*, *AGGREKO*, *SONGAS* na kadhalika wasiweze kupunguza *capacity charges* kwa kuzingatia mikataba itakayotumika katika hii mikataba itakayofuata?

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ijitahidi kuangalia uwezekano wa ku-*renegotiate* ili *capacity charge* iweze kupungua na kuweza kuleta unafuu kwa gharama za umeme kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo limeulizwa moja kwa moja na mzungumzaji mmoja alizungumza leo asubuhi ni kwamba tulikuwa na shamba la miti ambalo lilikuwa linazalisha nguzo za umeme. Je, hakuna uwezekano wa kuingia majadiliano na aliyenunua shamba hili ili tukawa wabia katika shamba hilo na kuliendeleza ili huko mbele kwa maisha yote tuwe na uhakika wa bei nafuu ya nguzo za umeme kwa sababu ni moja kati ya *cost component* ambazo zinaongeza sana bei ya kuunganisha umeme? Kwa hiyo, tunategemea Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi juu ya uwezekano wa haya.

Mheshimiwa Spika, endapo muswada huu utakamilika na bei ya umeme na kuunganisha umeme ibaki kama ilivyo sasa, kwa kweli maisha bora kwa Mtanzania kwa maana ya kuwaletea unafuu wa huduma hii ya umeme ambayo ni huduma mtambuka inaweza kupunguza makali vijijini itakuwa bado ni mzigo mkubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wazo jingine kwamba kwa vile bei ya kuunganisha umeme kwa nguzo moja au mbili haimfanyi mteja aliyeunganishiwa umeme

kuzimiliki zile nguzo maisha yake yote bali inabaki ni mali ya *TANESCO* au yule aliyeweka kwa maisha yote.

Kwa nini thamani ya nguzo zile isiwe sehemu ya kulipia umeme kwa awali mpaka thamani ile itakapoisha ibaki ni mali ya *TANESCO*. Bila kufanya hivyo ni kumwonea mwananchi kwa sababu hamiliki chochote, tunaomba hilo Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu unapoamua kuchukua umeme wa *TANESCO* umeingia mkataba, wewe mteja na *TANESCO*, kwamba *TANESCO* itakupa umeme kwa saa 24 kwa kila mwezi kwa mwaka mzima. Hatutegemei umeme ukatike hata kama ni kwa *notice* kwa sababu huko ni kukiukwa kwa mkataba.

Tunapata hasara sana tunapoharibikiwa vitu tunavyovi-*freeze* katika vipozesho, na tunapata hasara kwa kuharibika kwa vifaa. Tunaelewa kwamba mitambo inahitaji *maintenance* hivyo nashauri kwamba ingekuwa ni busara kufuatana na hali halisi ilivyo katika saa ambazo *TANESCO* inapaswa kufua umeme.

Kwa mwaka mzima wapewe asilimia kumi ya saa zote za mwaka kama ni *allowance ya maintenance*, lakini akikata umeme zaidi ya saa zile apate *penalty* kidogo iende kwenye unafuu kwa mteja kwa sababu haikutegemewa kukatwa na si mkataba kwamba akatiwe umeme ili iwape *discipline* na wao pia ya kutokukata umeme kwa wakati wowote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, muswada huu utafungua njia kwa wawekezaji huru kuingia katika kufua umeme. Kazi kwa *TANESCO* ni kubadilika na kutoa huduma nzuri zaidi hivi sasa kuliko ilivyokuwa zamani.

Tumesikia kwa Wabunge kadhaa waliotangulia kuzungumzia *TANESCO* ingawa inalaumiwa, ni ukweli usiofichika kwamba Serikali kwa sehemu kubwa nayo imechangia kuifanya *TANESCO* isononeke na kudidimia ilivyo sasa, imeingiliwa mara kadhaa katika maamuzi ambayo kitaalamu yasingepaswa kuwa hivyo. Imetamka kuwa marehemu Moshia alikuwa hodari na timu yake kusimamia shirika hili ambalo lilikuwa na sifa katika Bara la Afrika, *World Bank* wanajua hilo.

Mheshimiwa Spika, ilivyokuja *NETGROUP* ilikuwa ni kitu cha kushitua jinsi walivyoondolewa watendaji wazuri, wakawekwa pembeni bila kazi na wakaingia *NETGROUP*. Matokeo yake sisi wadau na kilio chetu cha kupinga *NETGROUP* wasiingie yametufikisha hapa tulipo, tumewafukuza na mpaka leo hatujui kwa nini wamefukuzwa.

Hakuna walicholeta, kubwa walikusanya madeni ambayo mengine makubwa yalikuwa ni ya Idara ya Serikali na Taasisi za umma pia.

Kwa hiyo, nategemea baada ya muswada huu kupita Serikali iwe ni mfano wa kwanza kulipa ankra zake za bili watakazokuwa wakidaiwa na *TANESCO* bila ubishi badala ya kuwatisha kama ilivyokuwa siku za nyuma ili waendeleo ku-*survive*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watendaji wazuri walioondolewa *TANESCO* wafadhili hawa hawa waliotushauri tutele *NETGROUP* ndiyo wamewachukua baadhi ya wale wafanyakazi waliotoka katika *TANESCO* na kuwa washauri wao nafikiri mnajua Bwana Luhanga yupo wapi. *World Bank* ni mshauri wa masuala ya *energy*, tumepoteza wafanya kazi wazuri pasipo kutarajia.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la *TANESCO* kujizatiti katika kuboresha huduma zao, ni pale vifaa vya umeme katika nyumba za wananchi zinapoharibika, kuna usumbufu usioeleweka kabisa, ukienda kudai wanakuletea mlolongo wa hadithi wa kila aina ili kujiepusha kwamba wao siyo wenye dosari, dosari iko katika *wiring* ya umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba katika teknolojia ya kisasa nafikiri ni lazima kuna *guidance* ambazo zinaweza kutumika kama *detectors* za kutambua shoti za umeme huu kama ilitoka *before the main switch or after the main switch* ili kuweza kutenda haki ya malipo kwa wateja wale wanaostahili badala ya kuwasumbua sumbua na kuwakatalia.

Mheshimiwa Spika, hilo nilikuwa na-*summarize* katika kulipa fidia ingawa sifuiti vifungu lakini natengema wanasheria kwa vipengele mbalimbali watajua sehemu za *kuvi-fit* katika kanuni au sheria zitakazokuwa zimetungwa ili ziweze kuboresha muswada huu.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ninaloomba *TANESCO* katika kuboresha huduma ni kuzisogeza karibu ofisi za malipo ya bili karibu na makazi ya watumiaji ama wateja.

Upo usumbufu mkubwa katika maeneo mbalimbali nchini na naamini vijijini inaweza kuwa ni tatizo kubwa zaidi walitambue mapema kwamba ofisi zikiwa mbali zitawaletea usumbufu mkubwa sana wateja kuenda kulipa bili za umeme.

Mheshimiwa Spika, nina mfano hai, Mji mdogo wa Mikumi na mandhari yake kama unavyouona wateja pale wanaenda kulipa bili za umeme Kidatu kilomita 38 umbali

kutoka mikumi kwenda na kurudi kilomita 76 kwenda tu kulipia bili ya umeme pengine ni elfu 6 au elfu 7 na gharama ya nauli ni elfu 4 kwenda na kurudi.

Hivi kweli haiwezekani sehemu kama hizo hata kompyuta moja ikawekwa Mikumi ili ku-*process data* za watumiaji? Ntoa mfano huo ili isije kutokea tena katika maeneo ambayo hakuna umeme kabisa katika kuleta ufanisi katika utendaji wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho katika kuboresha huduma ni la kuji-*decentralize* kwa kiwango kikubwa zaidi madaraka ya Mameneja wa Mikoani, nimeshuhudia kama kweli *decentralisation* ikifanyika na ikatumika kwa *standard* na *speed* zako mafanikio ni makubwa ninayo mifano hai.

Miezi miwili iliyopita, nilimchukua Meneja wa Mkoa wa Morogoro, Ndugu Msofe na kumpeleka katika Kata zangu tatu; ambapo tayari kuna milingoti na nyaya zimekaa kwa miaka kumi, lakini hazijaunganishwa katika kijiji kimoja cha Kivungu. Zinahitajika mita 500 kutoka kwenye transfoma ingawa ni ndogo lakini kwa miaka kumi, imeshindikana. Tumekwenda naye Meneja huyo, tumepita kwa *DC* halafu tukaenda katika vijiji vilivyoko katika Kata hizo, hakuamini niliyokuwa nikiyasema, lakini alishikwa na butwaa kuona milingoti nadhifu, mizuri na nyaya safi, lakini zimekaa na nyumba mpaka nyingine zimeanguka, hakuna umeme uliunganishwa. Kwa madaraka aliyonayo, alitoa agizo pale pale kwa Meneja wake wa Wilaya na kutamka kwamba, lete fomu kesho na orodhesha wananchi wote katika maeneo haya, ambao wanaohitaji umeme na kufikia Julai lazima tufunge umeme. *Decentralization of* madaraka, ninategemea baada ya Muswada huu kupita na shughuli ya usambazaji wa umeme vijijini kufanyika, *TANESCO* na wawekezaji wengine wata-*decentralize operations* zao, kwa kiasi kikubwa ziwe kuleta ufanisi wa maamuzi ya haraka kufuatana na mazingira.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa linahusu uadilifu ambalo ni tete na nyeti. Tuna-*deal* na wawekezaji tunaowategemea kupitia *EWURA*, kupitia *negotiations* za Serikali na kadhalika; tumeona mifano kadhaa ya matukio yaliyojitokeza hivi karibuni, ambayo kwa kweli yanatutia wasiwasi. Muswada huu ninataka kusema, sio siri mara ya kwanza ulipoletwa ulikataliwa, kwa sababu tayari tunahisia za mizingira ambayo baadhi ya wenye nia mbaya walitaka kuanza kui-*sub trudge TANESCO*. La pili, kujipenyeza wao wenyewe kwa manufaa yao binafsi, *rather than* manufaa ya Taifa hili kupata miradi na kujinufaisha zaidi na zaidi. Tahadhari ndugu zangu Wabunge na Mawaziri tuwe waaminifu, tumsaidie Mheshimiwa Rais kutimiza dhamira yake ya kuleta maisha bora kwa Watanzania, kwa kutimiza yale ambayo anayategemea na yale ambayo sisi sote tunayategemea. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumesonga mbele na wananchi watajenga imani zaidi kwa Serikali yetu na tutaendelea bado kumudu kutawala nchi yetu kwa amani, utulivu, upendo na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niitumie nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kwenye Muswada huu wa Sheria ya Umeme, ambao kwa kifupi, unafungua milango kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa pale tulipewa dakika tatu kuchangia, kati ya watu ambao walikuwa hawautaki huu Muswada na mimi nilikuwa mmoja wao. Leo nimeona majedwali ya marekebicho yameletwa na Waziri, ninaona kidogo hali si mbaya sasa tutaweza kuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na Wakala wa Umeme Vijijini; mwaka 2005 Muswada huu ulizungumzwa ndani ya Bunge na Wakala ule ukawa Sheria Namba Nane ya 2005. Wakala ule uliunda *REA*, ukaunda Bodi ya Wakala, Mfuko wa Wakala na vilevile ukaunda Wakala wa Mfuko. Hii *structure* yenyewe tu ni gharama kubwa na tulikubali wakati ule ni gharama kubwa sana. Muswada ule wa Wakala wa Umeme Vijijini wa 2005 ulijadiliwa na zaidi ya Wabunge 48. Nilitaka nikumbushe tu kwamba, mwanzoni kwenye dibaji wale Wabunge 48 walisema nini; kila Mbunge aliyesimama alisema, Muswada umekuja kwa wakati muafaka, kila Mbunge alisema sheria inasubiriwa sana na wananchi na kila Mbunge alitoa pongezi kwa Waziri, kwa kuleta ule Muswada na waliozungumza wote waliunga mkono kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba sasa nisome jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri wa wakati ule, alivyohitimisha hoja ile ya kuundwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini. Ninaomba kunukuu anasema: “Muswada umechelewa, tunachoomba mturuhusu Muswada huu upite uwe Sheria na sisi tuko tayari kabisa kuanza mara moja, tukikutana mwezi Juni hapa labda tutakuwa na hadithi nyingine ya kusema.” Akaendelea kuhitimisha kwa kusema: “Tutaanza kuwa tunapokea miradi na kuona kwamba kazi hii inafanyika na umeme unafikishwa kule ambako unahitajika, kwa wananchi ambao wanaungojea kwa muda mrefu sana na tunasukuma maendeleo yetu kwa nishati hii ambayo tunaamini, itakuwa ya bei nafuu au bei ambayo wanaweza kulipa na ikawa ni kichocho cha maendeleo vijijini.” Alipigiwa makofi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tulipofika mwezi Juni, hakuna lililotokea, maana yeye alisema kwamba pengine hadithi itakuwa nyingine, hadithi haikuwa nyingine! Sasa mimi nauliza hivi; kama mtu ukimuuliza wale ng’ombe wangu umewaona, halafu yeye anajibu wale punda walikuwa weupe utaendelea kuuliza? Huwezi kuendelea kuuliza! Kwa hiyo, miaka minne imepita huu sasa ni wa nne; 2005, 2006, 2007, sasa 2008, wakala haujaweza hata kujitambulisha mahali popote. Mambo haya kidogo ni magumu na wakati ule yote haya ambayo tumeyasema leo hapa yalisemwa; ya *IPTL* yalisemwa; ya *SONGAS* yalisemwa; ya *Stigler’s Gorge* yalisemwa; ya *NetGroup Solution* yalisemwa; na ya *AGGREKO* yalisemwa. Kama ambavyo leo tumesema hapa, Muswada huu ulipojadiliwa yalisemwa haya na leo ni miaka minne wakala haujaanza kazi mahali popote, tunaambiwa tu umeanza mwaka jana lakini hatujaona jambo lolote na haujaweza hata kujitambulisha mahali popote!

Mheshimiwa Spika, Wakala huu tulisema utapata fedha zake kutoka kwenye Bajeti ya Serikali, ambayo ni shilingi bilioni kumi. Mwaka jana ninadhani tulikubali iwekwe kwenye bajeti, lakini hatujaona zimefanya nini? Hatuwezi kuelewa, sasa tungependa kufahamu. Tozo ya asilimia tano, sina hakika kama imefanyika. Kulikuwa na suala la misaada kutoka kwa wahisani gani, sina hakika kama kuna mhisani yeyote aliyetoa. Halafu vilevile kwenye chanzo cha fedha, tulizungumzia riba itakayotokana na wawekezaji, labda hii pengine ndiyo tunaisubiri sasa.

Mheshimiwa Spika, tunasema wawekezaji waliotutia hasara hatuwataki, hawa wanya tunaowataka watatoka wapi; maana tunao wengi na wote wametutia hasara? Ninadhani sawa tunakubali sasa tunafungua, tunaomba watakaokuja wasije na masharti yao, maana watakuja na masharti kwamba, nguzo zitoke Afrika Kusini, *wire* nunua kutoka Afrika Kusini, *socket breakers* nunua kutoka Afrika Kusini na *switch* nunua kutoka Afrika Kusini. Tukikubali masharti ya namna hii, tutakuwa tumeharibikiwa na ndiyo maana sasa *TANESCO* inanunua nguzo kutoka Afrika Kusini, maana shamba la nguzo wameliuza; sijui na Kenya wananunua kutoka wapi?

Mheshimiwa Spika, nilidhani sasa Miradi ya Umeme tuiweke kwenye Mpango wa Maendeleo, tuanze kueleza hapa mwishoni kwamba ni mpango wa namna gani. Lipo suala lingine la *EWURA*, sasa labda ipewe meno mengine kwa sababu *EWURA* iliyopo imeshindwa kudhibiti bei ya mafuta; *EWURA* ipi sasa ambayo itasaidia? *EWURA* sasa hivi inapata matatizo, hata bei ya maji wameanza kushindwa maana Mamlaka za Maji nchini kote zimeshaanza kuisukuma inakubali bei zinapandishwa katika maeneo fulani fulani.

*EWURA* hii haitakuwa na uwezo, labda ipewe uwezo wa kuangalia uendeshaji wa vyombo hivyo ukoje, kwa mfano, kama ni Mamlaka ya Maji labda waseme bodi ziondoke au nini kiondoke ili bei ipungue. Kwa mtindo wa sasa, unaipa *EWURA* tena kazi ya kuangalia bei ya umeme, ambapo wawekezaji sina hakika kama watakuwa na uwezo huo na siwezi kusema kwamba bei inaweza ikapungua. Ninadhani itaendelea kupanda tu, hakuna namna yoyote ile labda *EWURA* tuipe tena meno zaidi ili waweze kudhibiti mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa labda niseme kidogo juu ya *TANESCO*; *TANESCO* ni Shirika la Umma, ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 sasa. Liliundwa ili kutoa huduma, lilidekezwa sana na Serikali yenyewe na lazima tukubali hapa lilidekezwa na Serikali. Serikali yenyewe ndiyo ilikuwa hailipi madeni; Wizara nyingi sana zilikuwa hazilipi madeni na wakitaka kukata umeme wanashindwa kwa sababu yule ndiyo baba. Vilevile walidekezwa kwa sheria, maana ilikuwa hakuna mtu mwingine yeyote, ambaye angeweza kupeleka umeme mahali popote pengine isipokuwa *TANESCO* yenyewe.

Sasa baada ya kudekezwa nayo ikaanza kupuuza wateja na wengine walionekana kunyanyasika, hasa kwenye mambo ya ankra, kwenye mambo ya madeni na huduma mbalimbali, kama zilivyotajwa na wengine katika kuunganisha umeme na vilevile malipo ya awali (*deposit*). Hivi kuna sababu gani mtu alipie nguzo ili aweze kuunganishiwa

umeme wakati sio mali yake na nyaya atakazovuta sio mali yake? Ninadhani hakuna sababu, sasa ni muda wa kubadilika katika utaratibu wa ushindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na ukiritimba, ambao ulizaa mambo mengi; baadhi ya watendaji wakawa jeuri, wengine wazembe na wengine wameamua kufanya biashara zao. *TANESCO* inahitaji kurekebisha sana.

Mheshimiwa Spika, labda kwa sababu *TANESCO* ni Shirika la Umma, ambalo tunalimiki kwa asilimia 100, ningetoa ushauri ufuatao: Kwanza, gharama za uendeshaji za zipunguzwe kabisa, muundo wake uangaliwe upya.

Ushauri wa pili, Serikali ichukue madeni yote iisamehe *TANESCO*, Serikali yenyewe inasamehewa na nchi nyingine sasa iwe *TANESCO!* Serikali iisamehe *TANESCO* isilipe chochote, chukueni hayo madeni. Kwa kuwa *TANESCO* ina miundombinu hawa wawekezaji wanaokuja hawana miundombinu; *TANESCO* ndiyo inayoweza kupeleka umeme vijijini. Huu ndiyo ukweli, hata kama tunasema wawekezaji watakuja lakini bado umuhimu wa *TANESCO* ni mkubwa sana. Vilevile nilidhani Bajeti ya *TANESCO* ianzie chini kule, hatupati nafasi ya kujadili *activities* za *TANESCO* wapi zilipo. Maendeleo ya umeme nchini yangekuwa yanajadiliwa kwenye ngazi za Serikali za Vijiji, Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na *RCC*, hapo tungepata mahali ambapo wananchi wangeweza kupeleka matatizo yao, lakini hakuna muundo huo. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri amepewa nafasi ya kuleta taarifa hapa kwenye kifungu cha 37(2), basi ni vizuri taarifa za maendeleo ya Miradi ya *TANESCO* zijadiliwe kwenye ngazi nilizozitaja ili wananchi wajue, hata wakiwa na tatizo wajue pa kuelekea. Sasa hivi mtu akiwa na tatizo, inabidi amwone Mbunge au *DC* ili kuelezea matatizo ya *TANESCO*, kwa sababu hakuna vikao huko chini; tuwe na muundo ambao shughuli za *TANESCO* zitajadiliwa kuanzia huko chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba, matatizo ya umeme yapo kila mahali; Babati yapo na Mheshimiwa Waziri anajua, nilimpa muda mrefu orodha ya vijiji ambavyo vina matatizo, sina haja ya kuvitaja leo, lakini vilevile ninajua hata kwako Urambo, kuna matatizo ya umeme pia; Simanjiro yapo kabisa, kwa Legule yapo; kule Msalala yapo; kwa hiyo kila mahali mpaka kwa majirani zangu hapa, Mheshimiwa Lekule ndiyo kabisa sio kijiji tu hata wilaya haina umeme. Kwa hiyo, haya matatizo ni ya kweli, tunaomba *TANESCO* iwezeshe na Serikali ili ikisaidiana na wawekezaji, waweze kupeleka umeme kwenye vijiji mbalimbali, haiwezekani tukaachia kazi hii watu wengine, hatutaiendeleza nchi hii. Kitovu cha maendeleo ni pale kijijini, tuanzie pale kama ilivyo kwa Miradi ya Afya na Elimu, tumefanikiwa kwenye MEM na MES kwa sababu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitumie nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi na niseme ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata fursa hii. Kwa vile muda wangu siyo mwingi sana, nitatumia maneno ya Kiingereza *to go straight to the points*.



Nianze kwa ku-*declare interest*; mimi kwa taaluma kwa ujumla utaweza kuniita ni mwana mazingira, kwa lugha rahisi. Kwa hiyo, nitakayoyazungumzia mengi ni ya kimazingira, ambayo pengine Wabunge wengi hawayachangii hayo. Nitumie muda huu vilevile pengine kwa namna hiyo, kuwasemea Wabunge wenzangu ambao ni Maprofesa humu Bungeni; kuna maneno yamekuwa yakisemwa hata kwenye *press* eti kwa nini Maprofesa wanakwenda Bungeni; wanakwenda kutafuta nini? Nilidhani pengine nitathibitisha hiyo, kwa kwenda kwenye maeneo ya taaluma yangu, ambayo pengine wengine hawawezi kuyazungumzia vizuri.

Vilevile niseme wanaosema hivyo, pengine hawana nia ya kulibeba Bunge lionekane kana kwamba ni mahali ambapo wasomi wa ngazi za juu hawatakiwi kwenda, bali ni mahali pa watu wa kisomo cha chini. Ninadhani wanataka kusema hivyo na bila shaka hawataki kusema hivyo. Tunataka mchanganyiko mzuri kwenye Bunge; vijana, watu wa makamo na wenye elimu mbalimbali, ndio maana Bunge hili limekuwa na changamoto sana na limeamka kwa sababu ya mchanganyiko huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo sasa naanza na vifungu. Kifungu cha kwanza ni kwenye ukurasa wa 8 kifungu cha 4(h) kinazungumzia kwamba, haya ni majukumu ya Waziri (*To cause to be conducted inquiries*) nahoji neno *inquiries* inaleta maana ya kwamba ni kuwa *reactive* badala ya kuwa *pro-active*. Tuna-*react* kwenye *consequences* baada ya matatizo kutokea ndiyo tuna *react*. Utaratibu ni kwamba kama tungekuwa tumefanyia mchakato wa mazingira tukafanya *disaster assessment*, tukafanya *risk assessment* kabla mradi haujaruhusiwa tungeweza ku-*anticipate*, tungejua matatizo haya yatatokea na kuweka mkakati wa mapema tuta-*deal* nayo vipi. Sasa ukitumia *inquiries* inawezekana ni neno la kitalaam kwenye sheria mimi siyo mwanasheria lakini nilikuwa nahoji hilo neno pengine tusizungumzie ku-*inquire*, ku- *inquire* maana yake unahoji tu, lakini kitu kimeshafanyika. *We should have known in advance* kuwa hiki kitu kitatokea na tukajiweka sawa.

Kifungu cha pili ni kile cha 6(i) na (f), kinazungumzia *functions* za *authority*. Anasema, *to take into account the effects of the activities of the electricity supply industry on the environment*. Nilitaka kusema kuwa, *environment which is so broad* na watu wengi hawajui ni kitu gani, wanadhani kupanda miti ndiyo *environment*, kumbe ni *broad term* inayohusisha mambo ya *economics*, *social* na mambo ya baiolojia. Kwa hiyo ni vyema kuwa *more specific* na kusema, *supply industry on the social, economic and biological environment* kuliko ku-*beat around the bush*.

Kifungu kinachofuata ni cha 6(1)(h); kinazungumzia kuhusu ku-*promote the health and safety of persons in the working environment employed in the electricity supply industry*. Kinazungumzia kuwasaidia kuwaweka sawa, kuwatetea na kuwahifadhi wanaofanya kazi kwenye *authority* hiyo. Sote tunajua kwamba, nyanya za umeme na *transformer* zinawekwa hata vijijini kwenye mashamba ya watu. Je, hawa wanakuwa *protected* vipi; kwa nini hii *statement* ina-*protect* wale watu wa shirika (*authority*); *how*

*about other people* ambako nyanya zinapita na *transformer* zimekuwa *established*? Nilidhani kwamba, inahitaji kuwa *broadened* kuliko ilivyo.

Kifungu kingine ni cha 6(2)(a)(ii); “*The authority shall in the exercises of its functions, consults the Minister on matters of common concern including* kuna (a) na (b); sasa chini ya (b)(2) kifungu kinasema, *preservation of the environment.*” Huwezi ukazungumzia juu ya *preservation* ni kuacha vitu *untouched*; kila kitu kibaki *intact* kama kilivyokuwa, *that is preservation. Don’t do anything.* Hapa nadhani tunazungumzia *conservation and not preservation.* Ninadhani mtakubali hapo ni jukumu la Profesa pengine kutafsiri vifungu hivi. (Kicheko/Makofi)

Kifungu cha 38(2) kinazungumzia kuhusu *the Minister periodically evaluate the impact of the rural electrification program on economic and social development.* Ongeza pale *on economic, environmental and social development.* Usisahau *environment* pale. Halafu kifungu cha 39 sasa hiki ndiyo ninataka kutumia muda kukizungumzia kidogo; kinazungumzia kuhusu matumizi ya *natural resources.*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hata hapa nchini kumekuwa watu wameanza kilimo cha *bio-fuel* kama jatrofa kiholela; ninasikia Kisarawe, Kilwa na maeneo ya Mpanda wanalima, lakini hatujui *implication* za kilimo hiki. *Bio-fuels* ni kitu kilichoanzishwa na *Democrats* Marekani, zilianza kutumika kabla hata ya *World War I*, kwa sababu walidhani ni *cheaper.* Baada ya *World War II*, mahitaji ya *energy* yakawa makubwa, wakaanza kurudi kwenye *fossil fuels* ambayo ni *diesel* na *petrol.*

Miaka hii ya 2000, ndiyo tumeshuhudia sasa watu wameona umuhimu wa kuingia kwenye *bio-fuels*, lakini tunaingia kichwa kichwa. Nilitaka kwenye kifungu hicho, kifungu kidogo namba (5) na (6), tuzungumzie kwanza ni lazima tuwe na Sera ya *Bio-fuels in this country.* Ninaomba kuwe na mikakati ya kufuatilia na kutekeleza hiyo Sera. Endapo kutakuwa na utengaji wa maeneo ya kilimo, tuseme litalimwa kwa utaratibu upi kwa sababu kilimo hiki kinapingana sana na mambo ya *food security.* Sasa hivi ninasikia China ukiagiza mchele au unga, huwezi kupata kwa sababu wanajua kuna *shortage* ya chakula. Maeneo ambayo ni *prime land* kwa ajili ya kilimo cha mpunga, sisi tunataka kulima michikichi; ni watu wa ajabu sana! Hiki ndiyo tunataka kukifanya hapa nchini. (Makofi)

Vilevile inaingiliana na suala zima la *desertification*, kwa sababu ni lazima ufyeke misitu. Kule Brazil wanafyeka *tropical rain forest* kwa ajili ya kulima *bio-fuels.* *This is wrong*; sisi tusifanye hivyo. Misitu ni muhimu kwa ajili ya kujilinda na *climate change.* Sasa tunazungumzia mambo ya *climate change*, tutashughulikia vipi wakati tunakwenda kufyeka misitu na kupanda hizi *bio-fuels.* Inaingiliana na mambo ya *bio-diversity* na kuleta *poverty, malnutrition* na kupandisha bei za vyakula. Sasa hivi sote tunashuhudia bei ya mchele, hata mahindi ninasikia imefikia gunia *is about 30,000 to 35,000.* Kwa hiyo, nilitaka tuwe waangalifu, tusikiweke kienyeji kama kilivyowekwa kwenye kifungu kidogo cha 5 na 6, hebu tukizungumzie zaidi kifungu hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ambayo ni *technical*, kwa ruhusa yako, sasa nizungumzie kidogo masuala ya Ludewa .

Kwanza kabisa, nizungumzie habari ya Mchuchuma, kwa sababu watu wamekuwa wakilizungumzia suala hili. Kwenye kitabu hiki kidogo, Mwelekeo wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 24 wanasema, kati ya ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ni kuanzisha machimbo ya makaa ya mawe Mchuchuma yaliko katika Kata ya Mkomang'ombe Ludewa. Katika maendeleo ambayo ni kijitabu hiki cha Septemba, 2007, muhtasari wa takwimu za mafanikio unasema kwamba, Shirika la *NDC* linaendelea na mchakato wa kuwapata wawekezaji katika Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga basi. Sasa tumebakiza miaka miwili; hivi kweli kwa miradi mikubwa kama hii, mpaka leo hakuna kitu kinachoendelea; tutawajibu nini wana-Ludewa, pamoja na Wananchi wa Tanzania, tunasema tunaanzisha Mradi huu mkubwa wa Mchuchuma; mpaka leo tunazungumzia kutafuta wawekezaji?. Nilitaka Waziri, anieleze tumefikia wapi na kilichotukwamisha tusianze Mradi huu wa Mchuchuma mpaka leo ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi hata ndani ya Bunge, wamekuwa wakiniambia Profesa Mwalyosi usizungumzie mambo ya kuanza miradi midogo midogo ya Liganga na Mchuchuma, tungojee mpaka baadaye iwe miradi mikubwa, wapatikane wawekezaji wakubwa. Nikiwaambia jamani kama ni hivi, ili sisi tusiendeleo kulinda mali hizi kule Ludewa wakati wenzetu mnaendelea kupata umeme na sisi hatuna, basi mtupe fedha za kufanya maendeleo wakati tunaendelea kuwalindieni mali hizi; kwa nini sisi tuendeleo kubaki nyuma, tualinda mali wakati wenzetu mnaendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninasema tuelezwe kwamba, kama tunatakiwa tuendeleo kulinda zile mali; mtatusaidia vipi sisi kupata maendeleo kule Ludewa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *grid*, ninajua tuliahidiwa na ninadhani Mheshimiwa Waziri, atakumbuka kwamba, umeme wa gridi utakapokwenda Songea, utachepuka Madaba kwenda Ludewa, ninadhani ahadi hiyo bado ipo, tunasubiri *SIDA* watoe hizo fedha, tuanze na sisi kufaidika na umeme wa *grid*. Ninajua umeme wa *grid* hautafika kwenye vijiji vya ndani maporini huko, haiwezekani, utapita kwenye vijiji vikubwa vikubwa, kando kando zinakopita nyaya zile ndio watapata umeme, lakini kusema utaingia mpaka vijiji vya ndani ni uongo tusidanganyane. Sasa utaona umuhimu wa *mini hydros* kule kwetu; Mheshimiwa Spika, umewahi kufanya kazi kule Ludewa, unakujua ni nchi ya milima, mito kibao na *potential* ya kuzalisha umeme kutokana na maji ni kubwa sana, wamishenari wanajua na karibu vijiji vinne, vina umeme kwa ajili ya misheni, lakini haukwenda kwenye vijiji, isipokuwa kijiji kimoja. Sasa hivi ninavyozungumza, kuna Kata nzima wanataka ku-*electrify* kutumia *a mini hydro* lakini ni wamishenari; Serikali iko wapi? (*Makofi*)

Sisi tunajua zaidi jiografia ya nchi yetu, *where are we*, mpaka tunaacha wamishenari wanatoka nje, wanakuja kufanya hivi vitu! Nilidhani wenzetu hawa *REA*, mahali pa kuanzia, kama hawajaanza wakaanze Ludewa, *opportunities* za vitu kama *mini*

*hydro* Ludewa zipo. Waende wakatusaidie *mini hydros* kwa ajili ya vijiji vingi kule Ludewa, kwa sababu wenzenu bado tupo nyuma, hatuna umeme na mpaka leo hakuna mji wenye umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba Waziri atakapokuwa ana-*summarize*, atueleze mtachukua hatua gani; sisi kule Rudewa tuko pembezoni, maana yake tuliambiwa Sera ya Awamu hii ya Serikali iangalie maeneo ya pembezoni; je, kwenye suala la umeme mnalishughulikia hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu umeme wa dizeli Ludewa.

(*Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**SPIKA:** Aaah! Kengele ya pili hiyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalyosi, ninadhani Ludewa wamesikia pia. Sasa mzungumzaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa John Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho, nami pia nichangie kuhusu huu Muswada wa Umeme. Awali ya yote, nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa dhati kabisa, kuhusu hatua iliyochukua ya kusimamisha malipo ya *IPTL*. Nimesoma katika magazeti kwamba, kesi ya *IPTL* ilikuwa ikiendeshwa na kwamba, Serikali ilifikia uamuzi kuwa malipo haya yasimamishwe na kama inawezekana, hatua hii iwe *extended* kwa makampuni hayo mengine.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni vyema sana kama tutaokoa haya malipo ambayo yanaendelea kulipwa mpaka sasa, kwa sababu hatutaeleweka endapo malipo haya yanayolipwa kwa haya makampuni ambayo yapo *attached* kwa *TANESCO* ya shilingi bilioni mbili kila mwezi, yataendelea kulipwa. Tunaulizwa kwamba jamani malipo haya vipi? Sasa ninadhani ni changamoto kwa Waziri na Wizara kwa ujumla, kuhakikisha kwamba, mikataba hii ambayo inapigiwa kelele sana na wananchi, basi ionekane wananchi wanatendewa haki ili tuweze kuinusuru *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika ripoti yake ya *TANESCO* inasema hivi; “Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ya *TANESCO*, kinajitahidi sana kufanya kazi ya kufichua matatizo na mambo yanayoendeshwa kinyume cha sheria na taratibu zilizopo, lakini juhudi hizo zinagonga ukuta, kwa vile hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya wahusika.”

Mheshimiwa Spika, hizi juhudi zinagonga ukuta; ukuta gani huu maana lazima tuhoji? Ukiangalia sana, ndiyo maana tunasema kwamba, yawezekana tunapoilaumu *TANESCO* tunakosea, kwa sababu tumeshaelezana hapa kwamba, Serikali mara nyingi

iliingia jikoni na katika ripoti ya *Richmond*, tumegundua kwamba, matatizo yalikuwa ni hayo. *TANESCO* walijieleza wazi mapema kabisa kwamba bwana, hili suala la *Richmond*, tumeingiliwa vya kutosha, sasa walichoka. Ripoti ya Mkaguzi inasema hivyo kwamba, Wakaguzi ndani ya *TANESCO*, wanaeleza mambo bayana, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa!

Mheshimiwa Spika, ndiyo hapo ninaposema kwamba, tuna tatizo hapo na kwamba, Serikali ingelikuwa ni vizuri ingejitenga kuingilia mambo ya ndani ya Mashirika. *TANESCO* ni *replica* ya Mashirika yote ya Umma, kifo chake yanakwenda hivyo hivyo. Mimi ni mmojawapo niliyefanya kazi katika Mashirika ya Umma; ni kweli kabisa kwamba, mashirika mengi yaliingiliwa utendaji na hata pale yalipofanya vizuri yaliingiliwa. *TANESCO* ni mojawapo, kuna wakati lilifanya vizuri lakini likaja likaingiliwa na ripoti zilizoonyeshwa hivi karibuni zinaonyesha wazi wazi kwamba, kuna kuingilia ndani ya mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninawaasa viongozi wajirekebishe maana kadri kunavyokucha, orodha ya viongozi waadilifu inazidi kupungua. Ndiyo ukweli, kila kunapokucha, asubuhi tukiamka, orodha inazidi kupungua. Ninakuombeni ndugu zangu hii ni hatari kabisa.

Mheshimiwa Spika, bado tunao viongozi waadilifu katika Serikali yetu na katika nchi hii. Viongozi ambao wao wanaishi kwa mishahara yao na marupurupu ya Ofisi zao. Tunao mfano mzuri sana wa Dr. Ali Mohamed Shein, Kiongozi wetu; sijawahi kusikia anaandikwa mahali popote. *Ame-serve* katika Serikali ya Mheshimiwa Mkapa na Serikali ya Awamu ya Nne ameteuliwa. Huyu ni kiongozi mwadilifu kabisa na juzi tumepata bahati, tumempata Waziri Mkuu ambaye ni mwadilifu. Nikigusia viongozi waliostaafu; Mzee Rashid Mfaume Kawawa, anaishi kwa kuotesha uyoga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa viongozi wanaoingia mikataba hii sio maskini ni matajiris sasa utajiri huu wanataka waufanyie nini? Ninadhani bado tuna nafasi kabisa, kama kesho wewe unateuliwa na Rais kuwa Waziri, kama unajua una madudu ni afadhali umwambie Rais bwana tafadhali niache, lakini kama una madudu halafu unaficha na unakubali nafasi hiyo utaumbuka; hii ni dunia ya utandawazi hakuna siri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulipokubali hii Sera ya Soko Huria na masuala ya utandawazi, lazima mwelewe *implications* zake ni lazima uwazi utakuwepo na utaandikwa. Sasa tunapoandikwa, tunalalamika; unataka uandikwe mazuri tu; *that is the problem*. Mimi ningeliomba tuige, bado tunao viongozi waadilifu na nimewataja, tunaoweza kuiga kutoka kwao, tuweze kuinusuru nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningelikuomba utusaidie tuwaeleweshe wenzetu ili waweze kukaa chonjo. Kuhusu Muswada mimi ni Tomaso kabisa, ninaungana na ndugu yangu, Mheshimiwa Lekule Laizer, siku ya Ijumaa alichangia; ninakubaliana naye kabisa mambo ndiyo hivyo. Ninaunga mkono lakini hii ya kusema mia kwa mia hapana. Bwana mmoja wakati wa kuchangia, alifananisha *TANESCO* na mitamba, ninafikiri alisema hivyo. Halafu akasema kwamba, yule anayekuja mwekezaji ni madume;

tulikuwa na mashirika ambayo tumeyaunganisha mitamba na madume lakini hayazai na kama yanazaa ndama hatuwaoni. Sasa tuwe na uhakika pia katika Muswada huu, hayo madume yanayokuja hayo ya wawekezaji, tuhakikishe kweli ni madume yasije yakawa yamehasiwa hayawezi kuzaa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani hata kidogo ni lazima tuwe *sure* na dada yangu hapa Mrs. Malecela alizungumza hapa kwamba, hawa watu wawe *scrutinized* sawa sawa. Tuliambiwa hawa watu walikuja na mikoba hapa, sasa wajulikane hata wanakotoka, wengi ni ma-*reject* kule. Sasa wanasema, *let us try Africa* maana huku sasa ni kapu la takataka. Anasema bwana sasa ngoja niende Afrika, kwao kule ameshindwa, maisha yamemshinda, anasema *let me go and try in Africa may be I will succeed in life* na kweli anakuja hapa, akishafika anakuta viongozi wetu hawana uzalendo, basi wanapigana *ten percent*. Akishakusoma kwa hilo tu basi *there is nothing doing it is bussiness as usual*. Anaku-*sum up* kwamba, bwana huyu ni mtu wa kumjaza mifuko yake, basi nae anafanya vyovyote atakavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sijui ni adhabu gani tutafute, maana tukisema tukiambiwa hizi Kamati zetu zichungulie mikataba, wanaambiwa hapana tutaingia jikoni. Hili jiko; unapokaa unasikia harufu ya mboga mpaka mwisho inaungua unaambiwa hapana; mama ametoka sebuleni na hii mboga inaungua kwa sababu wewe huruhusiwi kufika jikoni, basi ikakamie yote! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Haroub, jana alipogusia hapa kwamba, labda kuna umuhimu wa kuwa na Kamati ya Bunge kuhusu masuala ya mafisadi. Nikirudi Manyoni kwa maana ya Itigi, tulipata umeme mwaka 2000, lakini uko *stunted* kwa sababu ambazo nimezizungumzia; *service line* ni shilingi laki tano. Vitu vinapokuwa pungufu, havipatikani kwa wakati na hakuna na ni adimu, watu walioorodheshwa ni 100 na wamelipia mita na vitu vingine, sijui vinakuja vingapi, sasa *definatly* kutakuwa na *corruption*; ampe nani amwache nani; atampa yule anayezungumza? Sasa vitu hivi tunavyo, tuna tatizo hilo, lakini ningeliomba tusikate tamaa, tuwape nafasi *TANESCO* tuone kama wanaweza wakatusaidia ili tutoe umeme hapo basi uende katika vijiji vyetu ambako ndiyo kwenye *bread basket* ya Mkoa wa Singida. *Bread basket* ya Mkoa wa Singida ni Mgandu.

Mheshimiwa Spika, hizi mbao zote ndugu zangu tunazonunua hapa Dodoma mjini kutengenezea vitanda na makochi ni mninga na zote zinatoka Mgandu. Asali, nta; watu wengi sana wanapenda asali lakini yote inatoka sehemu hiyo. Sasa mtazamo wetu wa kuweka mijini umeme badala ya sehemu zinazozalisha, *that is the problem*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa *motivated* zaidi na mambo ya siasa kusambaza umeme ndiyo maana hapa juzi tulikuwa tunashikana mashati; watu wa Kusini; watu wa wapi, ndio inategemea nani aliyekuwepo madarakani. Maana Kusini wamelalamika miaka mingi kwamba, hawapati umeme na ni kweli *disparities* hizo ndizo zinazotufanya tuweze ku-*complain*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeliomba umeme utoke Itigi hapa uende Mlongo G, ulanga, Itagata, Kayui, Mtakuja, Makale, Mitundu, Kiyombo, Kirumbi, Mwamagembe, Kimtanula mpaka Rungwa kule Kambikatoto, kwa ndugu yangu na sisi tuna nyumba za uhakika. Waziri mwenyewe ni shahidi, alifika kwenye Nane Nane alijionea mwenyewe. Hatuzungumzii umeme kuwekwa kwenye nyumba za nyasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka kupeleka maeneo ambayo kuna uzalishaji. Mwezi uliopita, nilipita sehemu za Bulyanhulu kule ulipo Mgodu wa Barrick, nje kidogo ya mgodi watu wako gizani. Maana ni afadhali nizingumze na maeneo mengine, msije mkasema mwamba, ngozi anavutia kwake, tuwe *fair* tu. Maeneo ya wazalishaji ndiyo tunasahau. Ninadhani Wizara italiona hili ili waweze kuwasaidia wale watu, nao wasilalamikie kuhusu Serikali yao bila sababu. Wakienda kule, wakashirikiana na Barrick, ninadhani wanaweza kuwasambazia umeme maeneo hayo, wakajisikia kwamba, wapo karibu na neema au wapo karibu na pepo.

Ukitoka Manyoni sasa kuja njia hii, lami inafika lakini watu wako gizani; nyumba siyo mbaya, unatoka Manyoni unaingia Muhalala, Solya, ukitoka pale Solya, unakuja Kilimatinde na Soja halafu unakuja Nunge, unashuka chini hapo halafu unakuja Chikuyu; sasa kweli gizani! Ningeliomba tuangalie haya, tuweze kusambaza haraka sehemu ambazo watu wamejipanga, kuweza kuleta maendeleo na si bora tu tunasambaza umeme, watu wengi wamechangia hapa kwamba, hii midume itakapofika, basi wahakikishe kabisa wanapangiwa maeneo na maeneo yaende kwa mtazamo wa kuleta maendeleo siyo masuala ya kisiasa, ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninakushukuru sana kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa John Paul Lwanji, wewe ni mtu muwazi na kwa hiyo, mchango wako umejaa ukweli na tunaomba uendelee hivyo hivyo. Waheshimiwa Wabunge, sasa tumemaliza wote waliotaka kuchangia katika Muswada huu; wenye historia ndefu; umepatiwa semina mbili nzito nzito; na umechangiwa na Wabunge zaidi ya 50. Kwa hiyo, sasa tumefika pazuri, ninafurahi sasa kumwita Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, unazo dakika zisizozidi 60, kwa hiyo, tulia nenda vizuri, jibu hoja safi kabisa. Una dakika hizo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati, kwa niaba ya wenzangu kutoka Wizara ya Nishati na Madini, vilevile kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye ana udhuru, hivi sasa anahudhuria mazishi ya Mtanzania mwenzetu, Marehemu Ditopile Mzuzuri, ambaye sote tunafahamu ametangulia mbele ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na kwa jinsi ambavyo wameujadili huu Muswada wa Sheria ya Umeme wa mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kurudia kutambua mchango mkubwa uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara na Kamati ya Nishati na Madini chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

Ushauri na mwongozo wa Kamati, kwa uhakika ulichangia katika kuboresha Muswada, hususan kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge, yaliyotolewa kwenye Semina zilizofanyika Dodoma na Dar es Salaam. Mimi na wenzangu katika Wizara ya Nishati na Madini, tumefarijika na ukweli ni kwamba, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kutofautiana katika baadhi ya maudhui ya Muswada, sote kwa pamoja tunatambua kwamba, Sekta ya Umeme ni nyeti na muhimu katika kushamirisha maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa utambuzi huo, michango ya Waheshimiwa Wabunge lililenga kuboresha Muswada ili uzingatie maslahi ya Taifa, pamoja na kuweka misingi imara ya kuendeleza Sekta ya Umeme kwa kushirikisha Sekta Binafsi.

Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa taratibu za Bunge, ndio yenye jukumu la kusimamia na kuongoza majadiliano ya kufanya marekebisho kwenye Muswada. Kwa muhtasari, maoni ya Kamati yaliyozingatiwa ni pamoja na yafuatayo: Elimu kwa wananchi inahitajika ili Sheria hii iweze kueleweka na kutekelezwa vizuri; Sheria mpya itumike kutekeleza Sera ya Nishati ya mwaka 2003; *EWURA* iimarishwe ili iweze kusimamia vizuri utoaji wa leseni na upangaji wa bei za umeme; *TANESCO* iimarishwe kwa kutekeleza mpango wa kuimarisha hali ya kifedha ya *TANESCO (Financial Recovery Plan)*; Serikali isimamie vizuri rasilimali za kuzalisha umeme nchini, Sheria ya Matumizi ya Rasilimali ya Gesi itungwe haraka; Mamlaka iweke Kanuni kwa ajili ya kuwabana wawekezaji; kutoa taarifa ya mwaka mmoja kabla ya kuondoa mitambo yao ya kuzalisha umeme; tozo kwa ajili ya wakala wa nishati vijijini iongezwe kutoka asilimia tano mpaka kumi kwa wenye leseni za kuzalisha umeme; wawekezaji katika Sekta ya Umeme watoe kipaumbele cha ajira kwa Watanzania na mikataba inayoingiwa na wawekezaji isiwe na kipengele cha kulipia gharama za *capacity charge*.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Umeme umezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, Programu za *Financial Recovery Plan*, kwa ajili ya *TANESCO* na ile ya *Power System Master Plan* zitatekelezwa kwa ukamilifu na kwa wakati, kwani ndiyo njia muafaka ya kuiimarisha *TANESCO* katika kipindi hiki cha mpito. Serikali bado ina imani na *TANESCO* na itaendelea kuchukua hatua za makusudi, zinazolenga kuiimarisha *TANESCO* ili iweze kuhimili ushindani wakati ukifika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, itashirikiana kwa karibu na *EWURA*, *REA*, *TANESCO* na taasisi nyingine husika, kuandaa utaratibu utakaohakikisha kuwa, wadau wa Sekta ya Umeme wanapata elimu stahiki kuhusiana na Muswada huu, kwani tunaamini malengo ya Sheria mpya ya Umeme, yatapokelewa kwa uelewa mkubwa na wananchi baada ya kupewa elimu hitajika.



Mheshimiwa Spika, kilio cha Waheshimiwa Wabunge wote ni kuharakisha upelekaji wa umeme vijijini. Serikali ilianzisha Wakala wa Nishati Vijijini kwa maana ya *Rural Energy Agency* na Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund*), kwa madhumuni ya kuweka mfumo wa kuharakisha kupeleka umeme vijijini. Maoni ya Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla ya kuongeza tozo na wigo wa mapato ya Mfuko wa Nishati Vijijini, yamepokelewa kwa moyo mkunjufu na ninaahidi nitashauriana na Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa ajili ya utekelezaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali ya gesi asilia. Mipango bora ya matumizi ya gesi ni muhimu ili kuhakikisha rasilimali hii inachangia ipasavyo katika uendelezaji wa Sekta ya Umeme na sekta nyingine za uchumi. Kwa kutambua hilo, Serikali ipo kwenye mchakato wa kutayarisha Muswada wa Sheria ya Gesi Asilia, ambao utawasilishwa Bungeni mapema iwezekanavyo.

Moja ya hoja kuu ya Waheshimiwa Wabunge ni kuondokana na malipo ya *capacity charge*. Kamati nayo imeshauri tufanye hivyo. Kama nilivyofafanua kwenye semina ya Wabunge, Vikao vya Kamati na hotuba ya kuwasilisha Muswada huu, *capacity charge* ni gharama za kufidia uwekezaji, ambazo zinajumuisha mtaji, mkopo, pamoja na gharama za uendeshaji. Moja ya malengo ya Muswada huu ni kuweka mazingira ambayo yatachochea uwekezaji kwenye Sekta ya Umeme, bila kuwepo na ulazima wa kuingia mikataba inayotambua malipo ya *capacity charge*. Kwa mfano, baada ya *TANESCO* kuimarika kifedha, itanza kuwekeza kwenye miradi ya kuzalisha umeme, ambayo mikataba yake haitakuwa na kipengele cha malipo ya *capacity charge*. (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa Muswada huu unalenga kuchochea Sekta Binafsi kuzalisha umeme na kuwauzia moja kwa moja wateja wakubwa, yaani *eligible customers*, uendelezaji wa miradi kwa mtindo huu, hautahitaji kuingia mikataba yenye kipengele cha malipo ya *capacity charge* kati ya waendelezaji wa miradi na *TANESCO*. Mwisho, baada ya soko la umeme kuimarika na kutawaliwa na nguvu za soko, yaani *wholesale competitive electricity trading model*, bei za umeme zitakuwa zinapangwa na nguvu za soko.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitambue mchango mzuri kutoka Kambi ya Upinzani, kupitia hotuba ya Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Jimbo la Mkanyageni na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani, imetoa michango na ushauri mzuri, ambao kwa uhakika, umesaidia kuuboresha Muswada huu. Michango ya Kambi ya Upinzani imejumuisha yafuatayo:-

Kwanza, jukumu la kutayarisha kanuni za kuuza na kununua umeme kutoka nje ya nchi, lisiwe la Waziri mwenye dhamana ya kusimamia shughuli za nishati na badala yake lichukuliwe na *EWURA*. Waziri atoe idhini ya mwongozo tu.

Pili, majukumu ya *Public Procurement Regulatory Authority*, kwa maana ya *PPRA*, yaainishwe kwenye Sheria ya Umeme.

Tatu, biashara ya kuuza umeme nje ya nchi ifanyike baada ya kutosheleza mahitaji ya ndani.

Nne, uhuishaji wa leseni usifanyike na ukifanyika ufanyike kwa uangalifu.

Tano, Watanzania wapewe kipaumbele cha kuajiriwa na kampuni zitakazoshiriki katika Sekta ya Umeme.

Sita, adhabu zilizoainishwa kwenye Muswada wa Sheria ya Umeme ni ndogo na hivyo ziongezwe.

Saba, kiwango cha uzalishaji umeme kinachostahili kupewa leseni kishuke kutoka megawati moja hadi walau kilowati 50 kwa maana ya megawati 0.05. *System Operator* apatikane kwa njia ya zabuni na asimamie utayarishaji wa *system expansion plan*.

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa ni biashara ya kununua na kuuza umeme nje ya nchi, idhibitiwe kwa kufunga mita makini kwa ajili ya kudhibiti mapato na matumizi ya umeme.

Uhamishaji wa leseni na majukumu kwa maana ya *transfer of licence and liabilities* usiruhusiwe na kama ukiruhusiwa, ufanyike kwa makini. Muswada hautoi mwongozo wa nini kifanyike iwapo mwekezaji ataamua kukatisha leseni. Haya yalikuwa ni maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe ufafanuzi kuhusu hoja za Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo: Kwanza, majukumu ya kutayarisha kanuni za kuuza na kununua umeme nje ya nchi ni suara la kisera na hivyo Waziri anawajibika kutayarisha mwongozo wa kusimamia uuzaji na ununuzi wa umeme nje ya nchi, kwa sababu kama nilivyosema ni jambo la kisera. Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani ilikuwa kwamba, jambo hili lishughulikiwe na *EWURA*, lakini *EWURA* ni chombo cha kiutendaji.

Maoni kuhusu majukumu ya *PPRA*, kiwango stahiki cha uuzaji wa umeme nje ya nchi, pamoja na udhibiti wa kuuza na kununua nje ya nchi. Mwongozo kuhusu ukatishaji wa leseni, pamoja na uhamishaji wa leseni yamezingatiwa kwenye Muswada huu.

Ajira kwa Watanzania itapewa kipaumbele kwa kuzingatia Sheria za Kazi, Uhamiaji na Sheria nyingine za nchi zinazotawala, ikiwemo taasisi yetu ya Uwekezaji kwa maana ya *Tanzania Investment Centre*. Wizara itashirikiana na taasisi husika, kuhakikisha kuwa, Watanzania wanapewa kipaumbele katika ajira za Miradi ya Umeme na ajira nyingine ambazo kwa stahiki, watakuwa wanapewa kipaumbele cha kwanza. Adhabu iliyoainishwa kwenye Muswada katika ibara ya 15, kifungu kidogo cha nane, inalingana na kosa lililokusudiwa kwenye ibara hiyo. Inapendekezwa kwamba, hii adhabu ni ndogo sana. Lengo la kutolazimika kupata leseni kwa ajili ya uzalishaji ambao hauzidi megawati moja ni kuhamasisha wawekezaji wadogo wadogo kuwekeza katika

Miradi ya Umeme Vijijini, pamoja na kuwapunguzia gharama zinazoambatana na taratibu za utoaji leseni.

Hata hivyo, wawekezaji hawa watasimamiwa na kanuni za udhibiti chini ya *EWURA*. Hoja ilikuwa kwamba, megawati moja ni kubwa na hawastahili kupata *exemptions*, lakini mantiki na malengo ya unafuu huo ni kwamba, tuhamasishe miradi mingi midogo midogo, ambayo haiko mijini, iko maeneo ya vijijini na tunaamini kwamba, hii ni mojawapo ya hatua ya kusonga mbele kuhakikisha kwamba, maeneo ya vijijini yanapata huduma stahiki ya umeme ambayo tulikuwa tukiililia kwa muda mrefu.

Kutokana na uzito na unyeti wa majukumu ya *system operator* ni muhimu kutumia utaratibu ulioainishwa katika Sheria hii inayopendekezwa, ambapo *EWURA* ina mamlaka ya ku-*designate* nani awe. Kuna mambo mengi ya kuzingatia katika hili. Mnafahamu wenzetu chini ya Mheshimiwa Mnyaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wangependa kuona jambo hili linahamia kwenye chombo chetu cha udhibiti kwa maana ya *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa mdomo na kwa maandishi. Nitaanza na wale waliochangia kwa mdomo. Nina wachangiaji 55, nitawasoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa kwanza alikuwa ni msemaji aliyetoa taarifa kwa niaba ya Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa O. Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Ahmed Ally Salim, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Dr. James P. Musalika, Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Manju S.O. Msambya, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o na Mheshimiwa Anne K. Malecela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi na Mheshimiwa John P. Lwanji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwatambue waliotoa michango yao kwa maandishi; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Severina S. Mwijage, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Joel N. Bendera na Mheshimiwa Yono S. Kevela.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohammed A. Chombo, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Said A. Arfi na Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Dr. Samsoni F. Mpanda, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwako, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Mohamed K. Missanga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma na Mheshimiwa James D. Lembeli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo ilikuwa orodha ya wachangiaji waliochangia kwa maandishi, jumla yao ni 89. Samahani, ninakumbushwa pia kuna Mheshimiwa Anastazia James Wambura, nilisahau nikamruka kwa bahati mbaya, ninaomba radhi. Alichangia kwa kuongea. Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, ninadhani pia nilimruka tu jina lake na Mheshimiwa Diana M. Chilolo, ambaye nimentaja.

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge, imejielekeza katika maeneo makuu yafuatayo: Kwanza, eneo linalohusu umeme vijijini. Sheria mpya ya Umeme, iongeze kasi ya kupeleka umeme vijijini, hiyo ni mojawapo ya hoja ambazo zimejitokeza katika hoja kuu hii kuhusu masuala ya umeme vijijini. Lingine lilikuwa ni Programu ya Kupeleka Umeme Vijijini, izingatie uwiano wa maendeleo ya nchi. Serikali iwajibike kutoa taarifa ya mendeleo ya upelekaji umeme vijijini, kama ilivyoainishwa kwenye Muswada huu. Vyanzo mbalimbali zaidi ya maji, viendelezwe kuchangia kuzalisha umeme unaokidhi mahitaji ya umeme nchini, kwa maana ya mijini na vijijini, lakini pia sehemu ambazo zipo gizani, zipewe kipaumbele cha kupelekewa nishati ya umeme. Hizi zilikuwa ni hoja ambazo zimejitokeza ndani ya hoja kuu, kuhusu hoja ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyochangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi ilikuwa ni kuhusu kuliimarisha Shirika la *TANESCO*. Katika hili, ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, ulikuwa ni kama ifuatavyo: *TANESCO* iache kubweteka, bali iongeze uwajibikaji kuhimili ushindani, *TANESCO* ifanyiwe marekebisho ya makusudi kwa nia ya kuchochea ufanisi na ushindani. Serikali ichukue hatua za makusudi za kuilinda *TANESCO* ili iweze kuwa imara na kuwa kampuni ya kibiashara badala ya kuwa kampuni ya kutoa huduma pekee. Serikali ibebe mzungu wa malipo ya *capacity charge*, iuze sehemu ya hisa zake ndani ya *TANESCO* kwa wananchi, ijenge gridi mpya kwa ajili ya Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Tabora na Rukwa. Mfumo wa usafirishaji wa umeme, yaani *transmission system*, ubaki mikononi mwa Serikali baada ya shughuli kuu za *TANESCO* kutenganishwa, kwa maana ya *vertical unbundling*. Mikataba mibovu iliyoingia *TANESCO* irekebishwe, kuipa *TANESCO* unafuu wa kifedha. Serikali iingie mkataba wa utendaji kwa maana ya *performance contract* na *TANESCO*. *TANESCO* iimarisha vituo vyake vyote vya kuzalisha umeme na itoe kipaumbele cha kuwekeza katika kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa umeme, hususan sehemu ya *North West Grid*. *TANESCO* itoe kipaumbele kukamilisha mradi wa kuunganisha Gridi za Zambia, Tanzania na Kenya ili kufanikisha kuanza biashara ya umeme kati ya nchi za *East African Community* na *SADC* na kuimarisha hali ya upatikanaji umeme nchini bila kutegemea mvua.

Ofisi za kulipia bili za umeme, ziwe karibu na vijiji kurahisisha malipo ya umeme na mita za luku zisamabazwe kwa wateja wengi kuimarisha mapato ya *TANESCO*. Mikataba ya Umeme wa Dharura iliyopo, isiongezwe muda baada ya kufikia ukomo wake. Aidha, kijengwe kituo Mwanza cha kuzalisha umeme wa *megawatt* 150 mpaka 200. Serikali itoe ruzuku kwa *TANESCO* kwa awamu mbili, yaani asilimia 50 mwaka ujao wa fedha 2008/2009 na asilimia 50 ya mwisho mwaka 2009/2010. Hoja nyingine iliyoongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa ni kuhusu Wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wake kwa maana ya *Rural Energy Fund*.

Katika hoja hii, ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni kuzingatia yafuatayo: Kwanza, wigo wa vyanzo vya mapato vya Wakala wa Nishati Vijijini upanuliwe na tozo ya asilimia tano kwa wenye leseni za kuzalisha umeme iongezwe hadi asilimia 20. Hapo kulikuwa na tofauti, wengine wanasema ifike asilimia kumi, wengine wanasema asilimia 20, lakini sisi tunaichukua ile ya juu ambayo ilipendekezwa. *REA* itoe kipaumbele kupeleka umeme maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa, kama vile Kigoma; Kasulu na Kibondo, pamoja na maeneo mengine ya Rukwa, lakini pia Mkoa wa Tabora. *REA* itengewe shilingi bilioni 100 katika bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja wa 2008/2009. Suala lingine ambalo liliongelewa lilikuwa ni kuimarisha utendaji wa *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, katika hili, ushauri na maoni ilikuwa ifuatavyo: *EWURA* iwe makini katika kutoa leseni. Msisitizo utolewe kwa leseni za kuzalisha na kusambaza umeme vijijini. Kanuni za kusimamia Sekta ya Umeme zitayarishwe na *EWURA*, badala ya Waziri. Kanuni za kudhibiti ubora wa vifaa vya umeme zisimamiwe na *EWURA*, uteuzi wa viongozi waandamizi wa *EWURA* ufanyike kwa makini. Aidha, *EWURA* itayarishe Programu ya Mafunzo kwa wafanyakazi wake katika maeneo ambayo wanahitaji mafunzo maalumu, yaani *specialized training*; *EWURA* isiwashinikize wawekezaji na ijihadhari na vitendo vya rushwa; *EWURA* ianzishe *tarrif stabilization tax* ili kuleta uwiano kwa gharama za umeme kati ya wateja wa *TANESCO* na wateja wa kampuni binafsi; *EWURA* isifanye kazi kama polisi na badala yake, ishirikiane na Serikali na *TANESCO* kupunguza bei za umeme, ilikuwa ni mojawapo ya mapendekezo na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge; *EWURA* ije na mkakati wa kuzuia wawekezaji binafsi kusitisha huduma zao na kuiweka Serikali rehani; *EWURA* iweke utaratibu mzuri wa malipo ya fidia kutokana na hitilafu za umeme; na mkataba kati ya *TANESCO* na mteja uheshimiwe kulinda maslahi ya mteja; *EWURA* kwa kushirikiana na *TANESCO* na Shirika la Umeme Zanzibar, *ZECO*, iandae semina kuhusu mipaka ya *EWURA* ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutengemaa kwa bei za umeme ilikuwa ni eneo lingine ambalo limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge. Katika hili, ushauri na mapendekezo ilikuwa kama ifuatavyo: Sheria mpya inayokusudiwa itoe msukumo wa kupunguza bei za umeme na kuziwezesha kutabirika. Mikataba iboreshwe na mikataba mipya iingiwe kwa uangalifu ili kuweka mazingira ya kupunguza bei za umeme. Bei ya gesi asilia izingatie bei kwenye soko la dunia. Gharama za kumuunganishia umeme mteja ni za juu mno na hivyo zipunguzwe au ziondolewe.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta Binafsi ilikuwa ni hoja iliyojitokeza kwa kuongelewa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Katika hili, maoni na maelekezo ilikuwa kama ifuatavyo: Mchango wa Sekta Binafsi ni muhimu katika kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini. Kampuni zitakazoshiriki katika uendelezaji wa Sekta ya Umeme zisiwe za kitapeli. Wawekezaji binafsi, wasiruhusiwe kushiriki katika eneo la *transmission*; Sekta Binafsi ishiriki kwa mtindo wa *public private partnership*; na Serikali iwe na hisa zisizopungua asilimia 25, kwa kila uwekezaji utakaotumia rasilimali ya nchi. Mikataba isijumuishie kipengele cha malipo ya *capacity*

*charge*, kodi ziondolewe kwenye vifaa vya kuzalisha umeme wa jua ili kuhamasisha matumizi ya nishati ya jua. Mradi wa *Stiegler's Gorge* uendelezwe na Serikali kwa mtindo wa *PPP*.

Kampuni ya *ARTUMAS* ni mkombozi wa Mikoja ya Mtwara na Lindi, hivyo basi, Wizara ya Nishati na Madini, iondoe urasimu katika kushughulikia programu ya kuendeleza gesi ya *Mnazi Bay*. Wawekezaji wasimilikishwe ardhi bali washirikiane na Serikali. Maeneo ya mpakani, yapatiwe umeme kwa kutumia vyanzo vya ndani badala ya kutegemea umeme kutoka nchi jirani. Kwa mfano, Wilaya ya Ileje, Mbozi na Rukwa, wanapata umeme usiotosheleza na usio bora. Miradi ya Ruhuji na Mpanga ipewe kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa sana lilikuwa ni kipengele cha ajira kwa Watanzania. Watanzania wapewe kipaumbele cha kuajiriwa na makampuni yatakayoshiriki katika uendelezaji wa Sekta ya Umeme. Utunzaji wa mazingira ilikuwa ni hoja nyingine na hili nimsifu sana Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, kwa jinsi ambavyo ametukumbusha katika mchango wake hivi karibuni. Nishati ya Umeme isambazwe vijijini ili kuzuwia ukataji wa miti usiwe endelevu. Nishati ya umeme unaozalishwa na gesi utumike vijijini kuzuwia uharibifu wa mazingira hususan kwa maeneo ambayo yako karibu na vyanzo vya kuzalisha gesi.

Mheshimiwa Spika, mchango ya Waheshimiwa Wabunge, imetumika ipasavyo kuboresha Muswada huu. Michango ambayo inagusa mambo ya kiseru, itapewa uzito unaostahili katika kutekeleza sera zetu. Michango inayohusu kuiimarisha *TANESCO*, itatumika kutekeleza kwa wakati mikakati iliyopo. Michango inayohusu kupanua wigo na kuongeza tozo kwa ajili ya mapato ya Wakala wa Nishati Vijijini, itajadiliwa kwa pamoja kati ya Waziri wa Nishati na Madini na Waziri wa Fedha na Uchumi, kubainisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Sheria mpya ya Umeme inayokusudiwa, yatahitaji usimamizi mzuri wa *EWURA*. Michango ya Waheshimiwa Wabunge, kuhusu uimarishaji wa utendaji wa *EWURA* itazingatiwa, kwani Serikali inaamini kwamba, *EWURA* yenye nguvu itakuwa na faida katika kulinda maslahi ya Serikali, Wananchi na washiriki wote kwenye Sekta ya Umeme.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta Binafsi haukupukiki na Serikali itazingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge, katika kuchuja wawekezaji wasiokuwa na sifa au kwa maneno mengine, wawekezaji matapeli. Serikali itakuwa makini kuhakikisha Sekta Binafsi inashiriki kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na ikibidi, mtindo wa *PPP* utapewa kipaumbele hususan kwa miradi mikubwa, ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa kama vile Mpango wa Uwekezaji wa *TANESCO*, utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, kwa gharama ya shilingi trilion moja nukta sita, katika miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutambua kilio cha Waheshimiwa Wabunge, kuhusu upelekaji wa umeme katika majimbo yao ya uchaguzi. Sheria ya Umeme

inayokusudiwa, imeainisha vizuri, azma ya Serikali ya kuharakisha kupeleka umeme vijijini kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Sera ya Taifa ya Nishati zinavyoelezea. Miradi yote iliyoainishwa na Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kujadili Muswada na hata ile ambayo haikusemewa hapa imeorosdheshwa. Sisi na Wizara ya Nishati na Madini, tunayo orodha kwa lengo la kuitafutia fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, sitaitaja miradi ambayo Waheshimiwa Wabunge, wameiainisha lakini ninaahidi Wizara ya Nishati, itatayarisha majibu kwa kila Mbunge, ambayo yatakuwa yanaeleza hatua na mikakati itakayochukuliwa na Serikali katika ketekeleza miradi tajwa. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge, wawe na subira, hasa katika kipindi hiki ambacho tunaendelea kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, ninapenda kutoa shukrani za dhiti kwako, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi mlivyoliongoza Bunge hili Tukufu katika kipindi chote cha kujadili Muswada huu. Ninapenda kutumia nafasi hii, kumshukuru pia Mheshimiwa William Shellukindo na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa michango na ushauri wao ambao ulichangia katika kuuboresha Muswada huu. Ninamtambua Mheshimiwa William Shellukindo, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Ninapenda pia kushukuru Kambi ya Upinzani, kupitia Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kwa michango yao. Mwisho, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, kwa mdomo na kwa maandishi, michango yao imekuwa chachu katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakidhi mahitaji ya kuendeleza Sekta ya Nishati ya kisasa, kwa misingi iliyo endelevu. Juu ya yote, Muswada wa Sheria ya Umeme, umelenga kuweka mazingira mazuri ya ushindani kwenye soko la umeme, kwa faida ya mteja na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Azma ya Serikali ya kuilinda na kuiimarisha *TANESCO*, iko pale pale sambamba na kuweka mazingira bora ya kuishirikisha Sekta Binafsi. Baada ya kusema hayo, sasa ninaomba kupitia kwa ufupi, kulingana na muda utakavyoruhusu, kwa wachangiaji ambao walichangia lakini pia kwa kuzingatia yale ambayo nimetolea ufafanuzi, kama hoja mahususi ambazo zilijitokeza kupitia michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzungumza ama kwa kuandika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mchangiaji wa kwanza alikuwa ni msoma taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa. Katika hili, kulikuwa na hoja nyingi ambazo zilijitokeza lakini niseme machache tu; kulikuwa na hoja ya kutaka elimu kwa wadau ili sheria iweze kueleweka na kutekelezwa vizuri. Tunasema, tutazingatia ni jambo la msingi, mipango ipo kuhakikisha kwamba, sheria hii ikishapita sasa, tuwaelimishe wananchi ili wajue zaidi. Sheria mpya itumike kutekeleza Sera ya Nishati ya mwaka 2002, ndio dhamira. Kimsingi pamoja na sababu nyingine, mojawapo ilikuwa ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Taifa, kuleta Muswada huu mbele ya Bunge hili Tukufu, *EWURA* isimamie vizuri upangaji wa bei za umeme. Jukumu hili limeainishwa katika Ibara ya 6(1)(b) na (c) ya Muswada huu. Kwa hiyo, mambo haya yamezingatiwa.



Mheshimiwa Spika, *TANESCO* iimarishwe kwa kutekeleza Mpango wa *Financial Recovery Plan*, pamoja na *Power System Master Plan*. Kama tulivyosema, Serikali imeazimia kuhakikisha utekelezaji wa Programu za *FRP* na *PSMP* unafanikiwa kwa wakati. Serikali isimamie vizuri rasilimali za kuzalisha umeme kama gesi asilia, makaa ya mawe, maji, nishati taka, nishati ya mimea na kadhalika. Ushauri huu tunauzingatia, Serikali kupitia sekta husika, itahakikisha kuwa rasilimali zote za kuzalisha umeme zinatumika ipasavyo na kwa tija. Sheria ya Matumizi ya Rasilimali itungwe haraka, kama nilivyokwisha kusema, tumekuwa katika mchakato wa kutayarisha sheria, ambayo itahusu masuala ya nishati. Mamlaka iandae kanuni kwa ajili ya kuwabana wahusika wote katika soko; tunatoa ufafanuzi kwamba jambo hili tutalizingatia.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kama nilivyosema, ilikuwa ni kuongeza wigo wa tozo ambao Sheria sasa hivi inaelekezwa kwamba, Wizara ya Nishati na Madini, inaweza kutoza mpaka asilimia tano kwa watumiaji wa umeme. Kama nilivyosema kwamba, tutawasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi, kuona ni jinsi gani tutaweza kuongeza kwa sababu ina *implications* zake katika masuala ya kodi. Niseme tu kwamba ni mawazo mazuri na sisi tuko tayari kwenda kulitekeleza hili.

Wawekezaji watoe kipaumbele cha ajira kwa Watanzania, kama nilivyosema tutazingatia kwa kushirikiana na taasisi nyingine.

Mikataba inyoingiwa na wawekezaji isilazimishe kulipia gharama za *capacity charge*; jambo hili tumeshaliongelea sana, ninarudia kusema kwamba, tutaendelea kuwa makini kwa sababu ambazo tumezisema.

Mheshimiwa Spika, hoja za Upinzani kama nilivyozielezea, kulikuwepo na hoja ya ongezeko la neno *low voltage* na *high voltage*, kwenye tafsiri ya ibara ya tatu ya Muswada. Ushauri huu tumeshauzingatia na tutauziangatia hasa baada ya kukamilisha taratibu za zoezi zima, kwa sababu hatua inayofuata sasa, waandishi wetu wa sheria watakuwa wameyazingatia mabadiliko madogo ambayo tumeyawasilisha, hasa kwa kuzingatia jedwali la kwanza na la pili. Yote kimsingi yamewasilishwa, yakizingatia hoja mbalimbali ambazo zimetolewa. Ibara ya 4(1)(g), jukumu la kutayarisha kanuni za kuuza na kununua umeme kutoka nje ya nchi, lisiwe la Waziri mwenye dhamana ya kusimamia shughuli za nishati, badala yake lichukuliwe na *EWURA*. Kama nilivyosema, jambo hili ni la sera linabaki kwa mwenye dhamana, kwa maana ya sera, Waziri ndio atahusika nazo lakini *EWURA* wana mamlaka ya kutayarisha kanuni nyingine ndogo (*rules*), kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya *PPRA* yaainishwe kwenye Sheria ya Umeme. Ushauri huu tumeupokea, ibara husika itafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia hilo. Niseme tu kwamba, hata kama tusingetaja kwenye sheria hii, katika hili kwa kweli hakuna ombwe (*vacuum*), kwa sababu sheria hii haifanyi kazi kama ilivyo peke yake. Ndio utaratibu wa kawaida, inazingatia pia sheria nyingine ambazo zinatumika katika jamii husika. Kwa hiyo, hata kama tusingetaja kifungu hiki, bado sheria inayotawala kuhusu masuala ya manunuzi inabaki kuwa ni ile sheria na mamlaka husika (*PPRA*).

Ibara ya 8(1)(f), biashara ya kuuza umeme nje ya nchi, ifanyike baada ya kutosheleza mahitaji ya ndani. Ushauri huu umepokelewa na utazingatiwa katika mwongozo utakaotayarishwa na Waziri wakati wa kurekebisha Soko la Umeme. Tumesema baada ya shughuli nzima ya kupitisha hii sheria, kuna mwaka mmoja wa kujiandaa lakini ndipo hapo ambapo Waziri mwenye dhamana, atakuwa anaangalia wakati utakapofika ni maeneo gani, *segment* gani ifunguliwe kwa ajili ya kuruhusu soko huria. Uhuishaji wa leseni usifanyike na ukifanyika ufanyike kwa uangalifu; umakini utazingatiwa wakati wa uhuishaji wa leseni. Hili tunalichukua; ni jambo la heri na ni miongoni mwa hoja za Wabunge wengi sana. Ibara ya 14(5)(c), Watanzania wapewe kipaumbele cha ajira, kama nilivyosema, hii ndio dhamira, Serikali haijawahi kubadilisha msimamo na tutaongeza zaidi usimamiaji wa utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 15(8), adhabu isomeke *should not be less than 4,000,000* badala ya *not exceeding 4,000,000 million*. Adhabu iliyoainishwa inalingana na kosa lililokusudiwa kwenye kifungu hicho, kutokana na mambo ya Mheshimiwa Mnyaa na Kambi ya Upinzani kwa ujumla. Tukubaliane kwamba, kwa kuanzia, tunaamini kwamba, inatosha lakini tutakapojulishwa kwamba, pengine adhabu hii haitoshi, muda utakuwepo wa kurekebisha, lakini kwa sasa tulikuwa tunadhani kwamba tuliache kama lilivyo. Ibara ya 18(4), kiwango cha uzalishaji umeme kinachostahili kupewa leseni, kishuke kutoka *megawatt* moja hadi *kilowatt 50*; kama nilivyokwisha kusema, sababu kubwa ya kutoa walau nafuu katika hiyo miradi ambayo inaweza kuzalisha *megawatt* moja ni kuhamasisha wawekezaji wakawekeze katika maeneo ya vijijini, ambako takriban asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kule. Tunaamini kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaongeza juhudi ya kuwafikishia umeme.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 20 ibara ndogo ya 1. *System operator* apatikane kwa njia ya zabuni na asisimamie utayarishaji wa *system expansion plan*. kutokana na uzito wa unyeti na majukumu ya *system operator* ni muhimu kutumia utaratibu ulioainishwa katika sheria hiyo kama ambavyo inajitokeza kwenye ibara ya 20 ibara ndogo ya 6. Tunawashauri wenzetu kwamba waamini. Serikali hili imelifanyia kazi imezingatia na tunajua ni kwanini Serikali inasema ni jambo ambalo ni bora likabaki chini ya mamlaka ya *EWURA* kwasababu kuna mambo mengi ya kuzingatia. Ibara ya 22 ibara ndogo ya 1, buiashara ya kununua na kuuza umeme nje ya nchi idhibitiwe kwa kufunga mita makini ili kudhibiti mapato ya matumizi ya umeme. Ushauri huu utazingatiwa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 19 haisemi ni nini kinafanyika iwapo muwekezaji ataamua kukatisha leseni yake. Ushauri huu tunauzingatia na tuseme tu kwamba, tuna nia ya kuweka taratibu nzuri kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, siku ya kuwasilisha. Tunatarajia kwamba, kutakuwa na utaratibu mzuri, mmojawapo ikiwa ni kuhakikisha kwamba, kunakuwa na taarifa ya mwaka mmoja kama ataamua vinginevyo, kama muwekezaji atakuwa na makusudio ya kutoendelea na biashara katika mazingira ya nchi yetu. Uhamishaji wa leseni na majukumu, kwa maana ya *transfer of licence and liabilities* na kama upo unafanywa mara ngapi. Masuala ya utaratibu wa uhamishaji wa leseni za muda, pamoja na majukumu mengine, utawekewa utaratibu na *EWURA* kabla

ya kuruhusu uhamishaji wa leseni kama ilivyoainishwa katika ibara ya 14 ya kifungu cha Muswada huu, ambao utakapokuwa sheria, itakuwa ni kifungu. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, jambo hili tumelizingatia. Kuna mambo mengi, sheria inatoa ile *general frame work*, lakini mambo ya kiutekelezaji, yatajitokeza kwenye zile kanuni zitakazotungwa na Waziri lakini pia zitakazotungwa na *EWURA*, kwa maana ya zile *rules*, kwa hiyo tunaamini kwamba, jambo hili litakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja mahususi imejitokeza, kama nilivyosema, suala la umeme vijijini. Hoja hii imechangiwa na wachangiaji wengi. Katika hili tuna Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Juma H. Kilimbah, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Mohamed A. Aziz, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Severina S. Mwijage, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Captain John D. Komba, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati na Mheshimiwa Benito W. Malangalila. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la umeme vijijini limeongelewa sana, lakini niseme tu kwamba, tunazingatia yote ambayo yamesemwa. Lakini katika hili, hoja zilikuwa sheria mpya ya umeme iongeze kasi ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninataka nifafanue kwamba, ibara ya 37 mpaka 39, zinaelezea masuala ya kupeleka umeme vijijini. Ukisoma ibara ya 39(4) na jedwali la pili vinaelezea vizuri. Marekebisho yaliyoko kwenye jedwali la kwanza, tunasema kabisa hii ni kwa ajili ya ku-*promote*, kuhamasisha uwekezaji na kuwezesha uwekezaji katika maeneo ya vijijini. Tofauti na mazingira tuliyonayo sasa, tunasema muwekezaji atakapokuwa na *plan*, kwa mfano, kama ataamua kujenga *transmission line* yake, kila eneo atakalopita likawa na watu ambao wana vigezo vya kuhudumia umeme, baada ya taratibu na vigezo vyote ambavyo vinatumika, basi iwe ni sehemu ya *package* yake ya *investment*. Hili jambo tunadhani kwamba, litaongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini, kuliko ilivyo sasa kusema tu kwamba, mashirika yaliyopo au Shirika letu la *TANESCO* mpaka lipate fedha. Tunataka tuanze na ukurasa mpya kwamba, hawa wanaokuja wajue jukumu lao linaanzia mwanzo wanapoanza ku-*invest*. Watakapokuwa wanafanya *feasibility study* ni pamoja na maeneo ambayo njia zao zitapita, kwa sababu haya maeneo yana sifa hawatayaruka. Ndio maana tunasema kwamba, ibara hii inatupa hakika zaidi ya kasi ya kufanikisha zoezi la kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme vijijini, uzingatie uwiano wa maendeleo wa nchi nzima. Tunapokea ushauri huu, lakini pia nibainishe kwamba, katika Sheria ya Wakala wa Nishati Vijijini ya mwaka 2005, ukisoma pale kifungu cha 6(2)(c) imeelezwa na hasa unapoisoma pamoja na lile jedwali lake, inaelezea majukumu, misingi na vigezo vinavyozingatiwa wakati wa kubainisha miradi ya kutekelezwa katika kupitia huu Mfuko wa huu Wakala wa Nishati Vijijini. Maeneo ambayo yanaanza kuzingatiwa ni yale ambayo hayajapewa hii huduma kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, ushauri tunauzingatia lakini msisitizo ni kwamba, sheria pia inatambua hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwajibike kutoa taarifa ya maendeleo ya upelekaji umeme vijijini, kama ilivyoainishwa kwenye Muswada huu. Suala hili litazingatiwa na limeainishwa kwenye sheria inayopendekezwa, kwa maana ya ibara ya 37(2). Vyanzo mablimali vya maji viendelezwe ili kuchangia kuzalisha umeme wa kutosha vijijini. Kwa kweli hii ndio dhamira ya Serikali, suala hili litazingatiwa, vilevile Sera ya Taifa ya Nishati, inaelekeza uendelezaji wa vyanzo mbalimbali ili kuharakisha usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, *REA* imefanya nini tangu ilipoanzishwa? Hili jambo limeongelewa sana, ninadhani tumekuwa tukitoa taarifa, kwa namna ambayo pengine si muafaka sana. Shilingi bilioni kumi ambayo tuliipata kwenye mwaka wa fedha huu ambao tunaendelea nao sasa, imeshaanza kutumika na hapa nina miradi ambayo ningependa kuisoma, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, wametaka kujua na nikizingatia hasa angalizo la Mheshimiwa Omar Kwaangw', hivi karibuni alikuwa anahoji na kutaka kujua hiyo miradi imefanya nini na iko wapi.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa hiyo shilingi bilioni kumi imetumika kama ifuatavyo: Tunapeleka umeme Jimbo la Kilolo kwa Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, kwa gharama ya shilingi bilioni moja nukta sita; tunapeleka Wilaya ya Kilindi kwa gharama ya shilingi bilioni moja nukta sita; tunapeleka umeme Uyui kwa gharama ya shilingi bilioni moja nukta tano; tunapeleka Wilaya ya Bahi kwa gharama ya shilingi bilioni moja nukta saba; tunapeleka Nkinga kwa gharama ya shilingi milioni 88.8; tunapeleka huduma hii ya umeme kwenye eneo la Matema Beach kule Mkoani Mbeya, Wilaya ya Kyela kwa shilingi milioni 712; tunapeleka umeme kwenye jimbo la Mheshimiwa Mkono kule *Chief Oswald secondary School*, kule Mang'ombe kwa gharama ya shilingi 198 milioni; tunapeleka umeme maeneo ya Mto wa Mbu kwa gharama ya shilingi 324 milioni na pia tumeshatoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa ndugu zetu wa Kibiti na Wilaya ya Rufiji kule, ambao ile njia ya umeme kuelekea Mikoa ya Kusini hasa ule umeme wa *SONGAS* unapopita, kulikuwa na matatizo pale ya fidia (*compensation*), kwa muda mrefu lakini tumekubaliana, tumetenga shilingi milioni 250 na zimeshakwenda.

Kwa hiyo, ninapenda kutumia nafasi hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, fedha hii inatumika, tumebakisha fedha kidogo kwa ajili ya uendeshaji, lakini tunasema kama ambavyo imejitokeza kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge, tunaamini kwenye bajeti inayokuja, Bunge litaridhia kutupitishia kasma ya kutosha ili tukawekeze kwenye miradi mingi zaidi hasa ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kuwa vigezo vizingatie maeneo ambayo yako gizani kwa muda mrefu, kama nilivyosema vigezo vinaeleweka kwenye Sheria ya REA. Hoja nyingine mahususi ilikuwa kuimarisha TANESCO, ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge karibu wote, lakini pengine niwataje, orodha ni ndefu inakaribia majina 100, nivumilie niache. Katika hili ilikuwa ni yale maangalizo kwamba, TANESCO isibweteke, ushauri tumezingatia. TANESCO ifanyiwe marekebisho ya makusudi, kwa nia ya kuongeza ufanisi, pamoja na kuhimili ushindani. Suala la kuongeza ufanisi ni la msingi, ushauri huu umezingatiwa. TANESCO ilindwe na Serikali, hii ndiyo dhamira ya Serikali; ukisoma pale kama nilivyosema, jedwali la kwanza lile la marekebisho, utaona ibara ya 41(6), tumeweka mahususi kwa ajili ya kulilinda Shirika la TANESCO.

Pamoja na juhudi nyingine, lakini tunasema pia kwamba, ijionyeshe dhahiri kwenye sheria hii. Tunasema kwamba, tupe ile *right to first refusal* kwamba, kwenye miradi yote mikubwa na hapa hatutaki kujifunga pengine na migodi; tuseme watumiaji wakubwa kwa maana ya kwamba, leo unaweza kutaja migodi, kesho ikaja miradi mingine mikubwa, ambayo inatumia umeme mwingi. Tunadhani kwamba, TANESCO iwe ni namna mojawapo ya kulinda, tuwape kwanza hawa kipaumbele wawe na haki ya kuwafanya hawa wawekezaji wawe wateja wao, lakini vinginevyo inawapa fursa pia ya kushirikiana na wawekezaji wengine, kwa jinsi ambavyo wanaona wao. Tunasema kipaumbele ni TANESCO kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia *financial recovery plan*, ndiyo tunavyosema kwamba ni mojawapo ya mipango ambayo tunaendelea kuhakikisha kwamba. TANESCO inaendelea kuwepo. TANESCO ifutiwe madeni na Serikali; niseme tu kama ambavyo tumetoa taarifa wakati ninasoma hotuba yangu ya kuwasilisha Muswada huu, mpaka sasa hivi Serikali ilishabadilisha kiasi cha shilingi 1.3 trilioni kuwa mtaji ndani ya TANESCO. Juhudi kubwa zimefanyika na tunaendelea kuhakikisha kwamba, TANESCO inaendelea kuwepo.

Serikali ibebe mzigo wa malipo ya *capacity charge*; Serikali inabeba nusu ya *capacity charge* ya IPTL, pamoja na *capacity charge* zote kwa mitambo ya kukodi kwa mkataba wa AGGREKO, ALSTOM pamoja na Dowans. Serikali iuze sehemu ya hisa zake katika TANESCO kwa wananchi; ushauri huu ni mzuri tunauchukua, lakini niseme tu kwamba, kwa sheria zetu zilivyo sasa hivi na hasa kwenye zile taratibu za kuandikisha kampuni kwenye lile soko la mitaji, tunafahamu kuna mchakato unaendelea, kubadilisha kanuni zao. Wanasema kwa sasa hivi ili kampuni iweze kuwa na sifa ya kuandishwa pale, lazima iwe na *track record* ya miaka mitatu mfululizo. Sasa kwa TANESCO, ndiyo kwanza tunaanza, kwa hiyo, hatujafikia hatua, lakini ushauri ni mzuri tunauzingatia.

Hoja kwamba ijengwe Gridi mpya kwa Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Tabora na Rukwa; ufafanuzi wetu ni kwamba, mkakati ni kuimarisha na kupanua Gridi ya Taifa ili iweze kufika mikoa yote ya Tanzania na hatimaye kuunganisha na Gridi za nchi za jirani na za kikanda. Mfumo wa usafirishaji umeme (*transmission system*), zibaki mikononi mwa Serikali baada ya TANESCO kutenganishwa shughuli zake kuu, kwa maana *vertical unbundling*. Mwelekeo mpya wa Sekta ya

Umeme, umeelekeza kuwa, mfumo wa usafirishaji wa umeme utakuwa chini ya Serikali. Mikataba mibovu iliyoingia *TANESCO* irekebishwe kuipa unafuu wa kifedha; Serikali inapitia upya mikataba kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alishatoa ufafanuzi na zoezi linaendelea. Tunaamini kwamba, katika hilo baada ya hapo kuna mambo ambayo yatakuwa yamerekebishwa. Niseme pia kwamba, juhudi zinaendelea kwa mfano, kuweza kuinunua mitambo ya *IPTL*, hii yote itakuwa inaipunguzia *TANESCO* mzigo.

Halafu Serikali iingie mkataba wa utendaji kwa maana ya *performance contract* na *TANESCO*; tayari Serikali imeanza kutengeneza utaratibu wa kuingia mkataba wa utendaji wa *TANESCO*, jambo hili linatekelezeka. *TANESCO* isambaze umeme vijijini, kwa kutumia mwongozo wa *power system master plan*; usambazaji umeme vijijini hauko chini ya *PSMP*, sheria inayopendekezwa inaainisha uwepo wa *rural electrification plan* na *strategies* ambayo iko chini ya *REA*. Kwa hiyo, hapa tulikuwa tunataka tufafanua kwamba, ile ni dira inaonyesha lakini utekelezaji wake utapitia kwenye Sheria ya Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini.

*TANESCO* imeajiri wafanyakazi wengi kuliko mahitaji yake, ajira ya sasa ya *TANESCO* imeendana na muundo wake, shirika ambalo muundo wake unazingatia mahitaji ya kiutendaji wa sasa na mwelekeo wa baadaye. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, changamoto tunaichukua. Haya ni mambo ya kiutendaji, kama mnavyofahamu, yapo masuala katika kugawana majukumu ya shughuli kama hizi. Lile ni shirika letu ambalo tumelipa sifa kujiendesha kibiashara, lina Bodi yake ya Wakurugenzi na *Management*. Kimsingi, tunaipeleka changamoto na tutakwenda kukaa nao, kwa sababu ndiyo sisi Wizara ambao taasisi iko chini yetu, tutaona jinsi gani ambavyo wanaweza kuikabili changamoto.

*TANESCO* ipambane na vishoka; ushauri utazingatiwa. *TANESCO* irudishe kiwanda cha nguzo ili kupunguza gharama za kusambaza umeme; ushauri tunaupokea, tutaufikisha kama nilivyosema kwa wenzetu, tutaendelea kujadiliana nao, tuone jinsi gani ambavyo wanaweza kurudi, kwa sababu ndiyo mojawapo ya misingi ya kujiimarisha katika kukabiliana na soko huria.

*TANESCO* iboreshe makusanyo ya mapato kutoka kwa wateja; ushauri umezingatiwa. *TANESCO* iimarisha vituo vyake vyote vya kuzalisha umeme na itoe kipaumbele kuwekeza katika kuimarisha mfumo wa usafirishaji; ushauri huu tumeupokea. Niseme tu kwamba, nilipokuwa ninawasilisha Muswada siku ile ya kwanza, kwa maana ya Ijumaa wiki iliyopita, *program* ya uwekezaji ilikuwa ni mambo ambayo niliongea katika taarifa yangu; ile *program* ya miaka mitano na imezingatia mambo haya kuhakikisha kwamba, *TANESCO* ina mizani yake ya vitabu, inabadilika na inakuwa bora zaidi.

Pia *TANESCO* itoe kipaumbele kukamilisha Mradi wa Kuunganisha Gridi za Zambia, Tanzania na Kenya ili kufanikisha biashara ya umeme kati ya nchi za Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Afrika. Juhudi za kutafuta fedha za kukamilisha mradi huo zinaendelea; ni miradi mikubwa. Serikali ipongezwe kwa kusitisha malipo ya *capacity charge* ya *IPTL*; je, baada ya hapo bei za umeme zitashuka? Ufafanuzi wetu ni

kwamba, Serikali haijasitisha malipo ya *capacity charge* ya *IPTL*, malipo yanaendelea kufanyika kwa mujibu wa mkataba ni mambo ambayo tunaongelea. Serikali ina jukumu la kuwaambia wananchi kupitia Bunge hili Tukufu ukweli na uhalisia wa mambo. Ninachotaka kusema ni kwamba ni mojawapo ya changamoto zinazotukabili katika Wizara ya Nishati na Madini, kwa niaba ya Serikali nzima, lakini tunayashughulikia.

Halafu ofisi za kulipia bili ziwe karibu na vijiji, ushauri huu tumesema utazingatiwa; yako mambo mengi ambayo yamesemwa lakini niseme kulikuwa na hoja ambayo ilitolewa kwamba, ruzuku kwa *TANESCO* ifanyike kwa awamu mbili; asilimia 50 mwaka unaokuja wa fedha na baadaye mwaka 2009/2010 ili kutayarisha *TANESCO* kuhimili ushindani. Ushauri ni mzuri lakini kama unakumbuka kwamba, mwaka jana Serikali hapa hapa Bungeni, tulitoa taarifa na tukaridhia kwamba si vyema kuendelea kutoa ruzuku kwa Shirika letu la *TANESCO*, kwa sababu tumeamua kulipa *mandate* ya kufanya kazi lijiendeshe kibiashara. Niseme tu kwamba, zile hatua ambazo tumezichukua hasa ile ya *financial recovery plan*, pamoja na mipango mingine inayoendelea, tuendeleo kuimarisha ili lizidi kuwa imara. Kurudi kwenye mzunguko ninadhani haitakuwa vyema, maana ni suala la kisera, sina hakika kama ni wakati muafaka wa kurudisha. Tunauzingatia ni ushauri mzuri, zipo namna nyingine kwa sababu ni shirika ambalo linajiendesha kibiashara na kuliboresha zaidi.

Je, *ARTUMAS* inapewa ruzuku kiasi gani na Serikali, hamna sababu ya kuwa na *double standards*; Serikali inaandaa utaratibu wa kuweka Mfuko Maalum (*Tariff Equalization Fund*), kwa nia ya kupunguza bei ya umeme kwa mlaji katika maeneo ya Mradi wa *ARTUMAS* ili kuhakikisha kuwa, bei hazitofautiani na maeneo mengine.

Hoja nyingine mahususi iliyojitokeza katika mjadala wa Bunge, ilikuwa ni kuimarisha *REA*, pamoja na Mfuko wake. Katika hili ni muhimu kupanua vyanzo vya mapato vya Wakala wa Nishati Vijijini, ndiyo hoja ambayo ilikuwa inajengwa. Tutazingatia ushauri huu, kwa kushirikiana na wadau wengine katika utekelezaji wake. Niseme tu kwamba, sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi, kuhakikisha kwamba, ile tozo ambayo tunapewa kwa mujibu wa Sheria ya *REA* ya mwaka 2005 ile ya asilimia tano kwa watumiaji umeme, basi tuanze kuitoa na pia tutazingatia kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameshauri, tuongeze hicho kiwango na baadaye tunaamini kwamba, tutakapokuja kwenye bajeti, mambo haya Bunge lako Tukufu litaridhia.

*REA* itoe kipaumbele sehemu zilizo mbali na gridi; hili tumeshalisemea. Miradi ya Umeme Vijijini ipewe ruzuku, jambo hili lipo wazi ndiyo utaratibu unaendelea. Maeneo ya Kigoma, Kasulu na Kibondo, wapewe kipaumbele na *REA*; Sheria ile inatoa kipaumbele kwa maeneo ambayo hakuna umeme kabisa kwa muda mrefu.

Hoja nyingine ilikuwa ni ya jumla kwamba, utendaji wa *EWURA* uimarishwe. Tunakubali kuchukua changamoto hii, ndiyo dhamira ya Serikali na tunaamini kwamba, tukizingatia haya, mambo yetu yatakuwa mazuri kwa maana ya wenzetu wa *EWURA*, tutakuwa karibu nao. Tunaamini pia kwamba, Bunge lako Tukufu, litazidi kutushauri kila ambapo mambo yatakuwa hayaendi sawa sawa.

Utengemavu wa bei za umeme, ilikuwa ni mojawapo ya hoja ambayo iliongelewa sana na Wabunge. Niseme tu kwamba, haya mambo tunayazingatia na faida mojawapo ya kulifungua soko, ukifuata ile misingi ya ushindani kwa ujumla na hasa ukizingatia kwamba hii sekta ni ndogo, bado inasimamiwa na mdhibiti ambaye ni *EWURA*. Tunaamini kwamba, hawatakuwa na fursa ya kupanga bei zao kwa jinsi wanavyotaka, kwa sababu kuna vigezo Sheria ya *EWURA* inaelezea wakati wa kupanga bei ni mambo gani yazingatiwe. Hakuna mwekezaji ama shirika katika soko hili, atakayekuja kwa jinsi anavyoona halafu akatupangia bei, jambo hili halitawezekana. Pia ni nia ya Serikali kuona kwamba, uwekezaji huu unakuwa ni wa gharama nafuu. *Over investment* ambayo baadaye itaji-*translate* kwenda kwa mtumiaji, jambo hili tutalidhibiti vizuri na kwa kutumia sheria zilizopo na taratibu zimekaa vizuri na sheria zilizvyo, tunahakikisha kwamba, jambo hili tunaweza kulidhibiti.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine mahususi ilikuwa ni kuhusu mchango wa Sekta Binafsi. Katika hili, Waheshimiwa Wabunge walijielekeze kwenye yafuatayo; mchango wa Sekta Binafsi unahitaji hususan katika kuongeza kasi ya kuongeza umeme vijijini kama nilivyosema ibara ya 39(4) ya Muswada, tunalizingatia tukiwa tumeweka mahususi kwenye ule wajibu/jukumu kwa huyu mwekezaji atakayekuja, hasa kama ataamua kuzalisha, kusafirisha na kusambaza, basi kila anapopita kama hatatumia njia ya *TANESCO* kwa maana ya mifumo hii ya Gridi ya Taifa, basi ahakikishe kwamba, kila anapopita penye watu wenye sifa za kuhudumia awahudumie.

Tunampa kama sehemu ya wajibu na hii inajitokeza zaidi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa wanasema, hii *corporate social responsibility* katika hawa wawekezaji iko wapi; sisi tumeamua kuijumuisha hapa katika wajibu iwe ni sehemu ya jukumu na itakuwa rahisi zaidi kwa sababu katika misingi ya kawaida; ukiongelea *corporate social responsibility*, unaongelea habari ya kujadili kwamba, wewe unapata faida ndani ya jamii ambayo inakuzunguka; huoni kama ni hekima na busara utupe kiasi Fulani? Sisi tunasema twende zaidi ya hapo, tuiseme kwamba tukaombe, tunasema iwe ni sehemu ya jukumu lake ni kwamba ni jambo la heri hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mambo ya kuhusu *capacity charge*, kama ambavyo nimesema, mikataba ya *TANESCO* ambayo ipo na hawa wazalishaji binafsi, Serikali imekuwa ikiendelea kulipa. Nusu ya *capacity charge* ya *IPTL* tunaendelea kuishughulikia.

Kulikuwa na hoja ya kwamba, Mradi wa *Stiegler's Gorge* uendelezwe na Serikali badala ya Sekta Binafsi au kwa mtindo wa *public private partnership*. Kwa kweli hii ndiyo dhamira ya Serikali na niseme tu kwamba, ukiongelea habari ya *Stiegler's Gorge*, unaongelea rasilimali ambayo iko chini ya mikono ya Watanzania.

Sisi tunaomba kusema kwamba, kwa ujumla tunapokuwa tunaongelea haya masuala ya uwekezaji binafsi, hatumaanisha lazima wawe wa kutoka nje lengo letu sisi, kwa mfano, kama kuna Watanzania wanaoweza ku-*invest* na kwa sababu tunafahamu



uwekezaji haategemei kuwa na fedha yako mkononi ni suala la kwenda kuchukua mikopo benki. Tunaamini wapo Watanzania wenye uwezo wa kufanya hivyo; ni dhamira ya Serikali kuona kwamba, Watanzania watakuwa ni wa kwanza, kutumia fursa hii kuwekeza ili mradi rasilimali iko chini ya *RUBADA*. Tunaamini kwamba, *RUBADA* inaweza kushirikiana na Watanzania wengine, wakazalisha umeme ambao unakaribia kuwa *megawatt* 2000, itatusaidia sana kuondokana na matatizo ya umeme. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, kwa kufanya vizuri itatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipewa changamoto hapa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, wakati anachangia akaniomba akasema kimsingi ni yeye tu na Mheshimiwa Cheyo, kaka yangu, ninadhani tulishakubaliana. Mheshimiwa Arfi, aliniambia iwapo nitamweleza kwamba, *TANESCO* ipo katika nafasi gain; ni kampuni ya kibiashara au ni kampuni ya huduma, ndipo ambapo yeye atakubali kuunga mkono Muswada. Ufafanuzi ni kwamba, *TANESCO* ni shirika la kibiashara, linalotoa huduma ya umeme. Biashara zipo za aina mbalimbali, lakini *TANESCO* inatoa huduma ya umeme. Ninamwomba Mheshimiwa Arfi, mwisho wa yote, aunge mkono Muswada kwa sababu ni maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira lilikuwa ni eneo mojawapo lililoongelewa na Waheshimiwa Wabunge; vipo vifungu kadhaa ambavyo vinajitokeza vikielekeza hilo; kwa mfano, ukisoma ibara 9(2)(d) na ibara ya 9(3), inaelezea umuhimu wa kuzingatia mojawapo ya vigezo ambapo mwekezaji atakapokuwa anakuja, anataka kupata leseni kutoka *EWURA*, mambo ya kuzingatia ni pamoja na hilo. Sisi tunaamini, pamoja na changamoto ambazo Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ametupa, tunazichukua na tunaahidi kwamba, tutakwenda kuzifanyia kazi, kwa sababu tunaamini ni kwa ajili ya faida na maslahi ya Taifa. Ninaahidi kwamba, mambo mengi yameongelewa kama ambavyo tumesambaza jedwali la kwanza na la pili, kwa marekebisho yale ambayo ni ya kiuandishi kama ambavyo limejitokeza lakini niombe radhi kwa machache ambayo hatujaona. Ninaamini kwamba, kwa ujumla wake, Muswada huu unazingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuzungumzia suala la *TANESCO*, tumeulizwa sana kwamba, huu mpango huu wa miaka mitano wa kuirusha *TANESCO* ukoje; nimeshasema kwamba, Serikali imeshaandaa. *TANESCO* ndiyo ilibuni ule mpango wa *financial recovery plan*, ilikuwa yule ni mtoto wa *TANESCO* na tunaamini kwamba, kwa sababu tumeipa mamlaka ya kujiendesha kibiashara na kwa sababu tunataka kutekeleza ile dhana ya kutowaingilia, kwa sababu ni shirika la kibiashara, tunaamini kwamba, mpango waliokuja nao na hasa kwa sababu Serikali mwaka jana iliuridhia, utatekelezeka vizuri. Ninafahamu suala la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela la kutaka kumhakikishia kwamba, *TANESCO* inalindwaje; moja ya namna ya kuilinda *TANESCO* ni kama nilivyosema; ni huu mpango wa kuihuisha ambayo vyanzo vyake vimeshabainishwa.

Tunapongea hivi, tayari vyanzo vimeshabainishwa, ule mpango wa 1.6 trioni si maneno ya kusema kwa ajili ya kuwafurahisha wananchi, mwisho wa yote *TANESCO* ni ya kwetu, upo hapa tunao, tungekuwa na muda ningeweza kusoma takwimu zipo hapa na vyanzo tumeshavibainisha; pesa za ndani, wafadhili na wahisani mbalimbali, pamoja na

mapato ambayo yanatokana na *TANESCO*. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tuamini kwamba, tunachokisema sio maneno ya kufurahisha, ninawaambieni kwa dhati kwamba, tuna nia ya dhati kuhakikisha kwamba, *TANESCO* inaendelea kuwa hai na tunawapa *mandate* yote inayowezekana, pamoja na changamoto ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi lakini kama nilivyosema kwamba, tutarudi kuja kujibu hoja kwa maana Mbunge mmoja baada ya mwingine, lakini niseme kwamba, ninaomba radhi sikuweza kupata nafasi ya kuweza kuwatambua kila aliyechangia. Tumeyakusanya majina kwa jumla, kwa kuzingatia mliyoongea, mniwie radhi. Miradi yote ndiyo hiyo tunasema kwamba, tatizo letu ni upungufu wa fedha lakini vinginevyo, tunaweza kuitekeleza. Tunatambua sana michango yenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

### **Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 (*The Electricity Bill, 2007*)**

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 3

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 4

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *submission* yangu ya maandishi na katika kuzungumza, niliezea kifungu cha 4(1)(h), kuhusu lile neno *enquires* na kwamba, kuna haja ya kuangalia hapa kwa sababu inaelekea Muswada una-*react* badala ya kuangalia namna ya kuzuia mambo yasitokee. Kwa hiyo, nilidhania suala la ku-*enquire* pengine ndiyo nzuri sana hapa.

**MWENYEKITI:** Nilidhani pengine unapenda la ziada, lakini hatuwezi kuzuia *enquires* katika utekelezaji wa sera hizi. Uchunguzi uwe haufanyiki, sasa kama kuna hatua nyingine ambayo inatakiwa, ulitakiwa unilettee Mezani kama badiliko.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5  
Ibara ya 6  
Ibara ya 7  
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, kifungu kipi cha kumi na moja?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani umeenda kidogo kwa haraka; kifungu cha 10(2) kinazungumzia *the authority may change terms and conditions of any licence issued under this act provided (a), (b), (c), (d)*. Sasa nilichouliza wakati ninazungumzia juu ya Muswada, inaonekana kwamba ni njia nyingine ambapo unatoa mwanya kwa mwekezaji kudai katika mikataba, pawepo na *physical stability*, kwa sababu mtu hawezi kuja kuwekeza huku akijua kwamba, Waziri anaweza ku-change au hisa inaweza kugeuza *conditions* za uwekezaji na tunajua *physical stability* za uwekezaji na *physical stability* za *contracts* nyingi zimetupa matatizo; sasa nilikuwa ninataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na hayo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninakumbuka kama nilivyosema, tunaheshimu michango ya Mheshimiwa Cheyo, lakini niseme tu kwamba, leseni kimsingi kwa utaratibu wa kawaida ni sheria lakini hilo la *physical stability*, haliwezi kufikia hapo, kwa sababu utaratibu wa kutunga sheria ni kwamba, sheria ndogo haiwezi ku-*contradict* na *parent law*. Katika hili, mamlaka ya EWURA kutunga sheria, tunafahamu hiyo nayo ni sehemu ya huu mkataba, lakini una nguvu ya kisheria hauwezi ku-*contradict* kama sheria haijasema kwamba, kuna fursa hiyo ya EWURA kuweza kumpa. Kwa mfano, masuala ya unafuu fulani ambayo yanagusa masuala ya kodi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ungependa kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kumhakikishia kwamba, jambo hili haliwezi kutokea kwa utaratibu wa kawaida. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Lakini mimi sio mwanasheria lakini Mheshimiwa Waziri ni Mwanasheria anajua sheria isiposema ndiyo kusema hilo jambo linaweza

likafanyika kwa sababu sheria haijakataza? Unayotueleza wewe leo sawa kesho ndugu yangu labda uko *Prime Minister* anayekuja pale ni mtu mwingine na yeye anachofuata ni sheria tu hapa haijasema mahali popote kwamba mwekezaji yoyote hataruhisiwa kudai mkataba ambao unam-*guarantee a physical stability* ambayo una-*contradict section* hii maana yake *physical stability* ambao una-*contradict section* hii maana yake *physical stability* ndiyo kusema kwamba hakuna kugeuza geuza ulivyoikuta ndivyo u livyoikuta?

**MWENYEKITI:** Ninadhani Mheshimiwa Cheyo, ungesoma mpaka mwisho, utaona kwenye (b) iko *proviso*, hubadili tu *the modification; is in the public interest where the benefit to the publics significantly exceed any disadvantage to the licence*. Kwa hiyo, hatuwezi kuweka *private interest* ikawa juu ya *public interest*. Hilo ndilo jibu lenyewe; *that is how it should work*. Waziri mwenye dhamana hii anapokuta kwamba, *it is in the public interest*, mathalani kuna *wind fool profits; this is one of the thing, most of our registration does not deal with wind fool profits*, zinabebwa moja kwa moja na hao hao wakubwa, akiamua kuibadili hiyo, mbona ni vizuri Wabunge tushangilie tu. (Makofi)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 11

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kuna mambo mbalimbali ambayo Kambi yetu inependekeza. Nilitaka kujua juu ya *transfer of licence*; kwa sababu imejitokeza hapa, tuna uzoefu kwamba, kuna makampuni ambayo yali-*transfer* kutoka moja kwenda nyingine; kwa mfano, *RICHMOND* kwenda *DOWANS*, sasa ningependa ufafanuzi kuhusu hili.

Je Muswada huu unazungumza vipi, yaani tumeona hapa kuwa ikiachiwa hivi inaweza kujitokeza watu kama hawa kuendeleza *process* hii ya *transparent*?

La pili, nilitaka kuelewa kuhusu *transfer of liabilities* ikoje; hili alikuzungumzwa vizuri katika Muswada; utaratibu gani ambao unaweza kutumika?

**MWENYEKITI:** Kwa hili la pili, halihusiani na kifungu hiki, labda tutalifikia huko mbele ila Waziri utoe ufafanuzi kwa hilo la kwanza.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema mojawapo ya mambo tuliyoyazingatia kutoka kwa wenzetu Kambi ya Upinzani ni hivyo, kwamba walikuwa wametutahadharisha tuwe makini sana. Mapendekezo yao kidogo yalikwenda mbele zaidi, maana yake walikwenda kwenye *extent* ya kusema ikiwezekana kusitokee *transfer* kwa hao wawekezaji watakaokuja. Sisi tunasema, ukiongelea habari ya biashara katika hali ya kawaida, mojawapo ya ukweli katika biashara na hasa unapofanya biashara kupitia taasisi mojawapo ya sifa za taasisi, ikaitwa *corporate entity* ni *transferability*.

Sasa hatudhani kama sisi tunataka kuja na kitu ambacho kimsingi na hili ninalisema tu, kwa sababu ni jambo la kawaida *conventionally* kwamba, ndivyo inavyofanyika. Pengine si nia ya wenzetu kushauri hivyo, kwa sababu tu ya hofu, zipo namna nyingi za ku-*plug* hizo *loop holes*. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwambahuo ni ukweli mmoja lakini tupo makini. *Transfer* ile haitoki mpaka kuwe na idhini ya kimaandishi kutoka kwa mdhibiti, EWURA. Sasa EWURA yule kuna vigezo vingi ambavyo atavizingatia ili kujiridhisha kama kuruhusu ama kutoruhusu. Kwa hiyo, nilikuwa ninamwomba kaka yangu, kama utapenda tukubaliane kwamba, twende pamoja. Ahsante sana. (Makofi)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 12  
Ibara ya 13

(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 14

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili, tulizungumzia juu ya umuhimu wa *transmission* kuwa katika msingi wa Serikali. Alipokuwa anajibu hoja, Mheshimiwa Waziri alisema kwa haraka haraka kwamba, *transmission* itakuwa katika msingi wa Serikali. Sasa Ibara ya 14(b), ambayo inazungumzia leseni ninanukuu: “*To provide access to its transmission or distribution access on an open and discriminatory basis.*” Sasa hii ndiyo inatupa shida, kwa sababu *transmission* hii *is really* ipo *open*, imefunguliwa kwa mtu yeyote yule ambaye anataka kuwekeza na hili nilifikiri umezingatia ushauri wetu, kwa sababu huu ndiyo mshipa wa usafirishaji na kwamba, ushiriki wa Serikali hapa ni muhimu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yawezekana niliongea haraka haraka sana, kwa sababu nilikuwa ninakimbizana na muda, ninaomba radhi kwa hilo. Nilisema kwamba, jambo hili tutalizingatia na nikasema endapo Sheria hii itapita, ikishapita kuna mwaka mmoja wa maandalizi. Katika ufafanuzi wangu nilisema kwamba, yapo mambo mengi ya kuzingatiwa, kwa sababu wakati tunaandaa mwongozo tunaangalia. Waziri kapewa Mamlaka kwenye huu Muswada, utakapokuwa Sheria, tutaangalia ni wapi tufungue, kwa sababu tunasema *segments* zote hazifunguliwi kwa pamoja na si lazima zifunguliwe kwa pamoja katika Sheria hii. Ndiyo maana ninasema, ukisoma kile Kifungu cha 40 na 41, kinaelezea tukifika kule tutaona, tutakapofika Waziri ataangalia ni wapi tuanze kufungua sasa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Cheyo twende na huu ukweli ndani ya Sheria kwamba, limezingatiwa na tutakuwa makini, lakini ninakushukuru sana kwa kutukumbusha.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge)

*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate ufafanuzi kuhusu Ibara ya 23 na hasa ile sehemu inayohusu gharama ya kuunganisha umeme na *deposit* ama malipo ya awali. Katika michango ...

**MWENYEKITI:** Itamke basi iko wapi?

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Ukurasa wa 23.

**MWENYEKITI:** Hapana siyo ukurasa wa 23 ni ukurasa wa 21.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Ibara ya 23(1)(c) halafu na ...

**MWENYEKITI:** Hebu anza na hiyo kwanza.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba, katika mchango wangu, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, tulitoa kilio cha wananchi kuhusu gharama kubwa ya kuunganisha umeme. Sasa Waziri amejaribu

kutaja taja, lakini majibu sijasikia kwamba, atachukua hatua gani ili kuweza kusaidia hasa wananchi wa vijijini ambao hawana uwezo na ilionekana kwamba, gharama ni kati ya Sh. 400,000 mpaka Sh. 500,000. Je, kwa sheria hii, atasaidia vipi hiyo gharama ipungue ili wanakijiji wengi au wananchi wengi zaidi, waweze kuunganisha umeme katika nyumba zao, baadhi yao hivi sasa wanao umeme lakini wanashindwa kwa sababu ya gharama hii kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni ibara ndogo ya (5) kuhusu *deposit* ni kwamba, kuna gharama nyingine tena inabuniwa kwamba, kabla ya kuunganisha umeme lazima ulipe malipo ya awali, ama juu ya hicho kifungu cha kuunganisha umeme na inaonekana kwamba, hii gharama itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya kwanza, kwa sababu zilizoelezwa katika Muswada huu. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, tutakwamisha wananchi wetu kuunganishiwa umeme kwa gharama hizi ambazo zitakaribia kufika Sh. 1,000,000 kabla hujaunganisha umeme; ninaomba maelezo tu kwamba, itakuwaje ama atachukua hatua gani kupunguza gharama hizi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Degera, wakati unaendelea, ninaomba niwakumbushe Kanuni ya 28(5), ambayo inasomeka kama ifuatavyo: “Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa moja na dakika arobaini na tano, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi, ndiyo sasa hivyo, kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao na Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini bila kuhoji Bunge au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki.” Kwa hiyo, ninatumia Mamlaka yangu chini ya Kanuni hii, kuongeza muda usiozidi dakika thelathini ili tuweze kukamilisha kazi iliyo mbele yetu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi hapo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifafanue hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Degera kama ifuatavyo:-

Kuhusu hii ibara ya 23(1)(c), kwenye gharama, ninafahamu Mheshimiwa Mbunge anaongelea gharama za sasa zilivyo lakini niseme tu, tunafahamu kwamba wananchi wetu vipato ni vidogo, havitoshi lakini pia kuna ukweli huo tena kwamba, ukiongelea mazingira ya leo ya *TANESCO*, tunataka lijiendeshe kibiashara kwa namna yoyote ile, lazima lifidie gharama zake za uzalishaji au uendeshaji. Kwa hiyo, kama ambavyo tumekuwa tukifafanua sana hapa, hasa wakati tunajibu maswali mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, gharama zinazotozwa sasa ni za juu, lakini pia ndiyo gharama halisi ambazo zinaonyesha gharama halisi kwa ajili ya kufikisha huduma katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hii ni changamoto kwetu sote, lakini kwa mazingira ya Muswada huu itakapokuwa sheria, mojawapo ya faida ambayo hutokana na biashara ya ushindani ni kwamba, washindani wanajitahidi kadri itakavyowezekana kupunguza gharama, kwa sababu wanawagombea wateja na katika mazingira fulani wateja ni wale wale. Katika hili watu wanaongeza ufanisi, teknolojia na kutumia muda

wa kujituma zaidi. Hii ni mojawapo ya faida zinazoweza kupatikana katika mazingira ya ushindani, sisemi kwamba, itakuwa hivyo lakini ukichukua ule utaratibu na ndiyo misingi na ukweli wa ushindani, mojawapo ya faida ni hiyo.

Kwa hiyo, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Degera kwamba, kwa hili kwa sababu zile bei lazima ziridhiwe na mdhibiti *EWURA*, hakuna namna ambayo gharama zinaweza kuwa hazionyeshi gharama ya uendeshaji. Kwa hiyo, ninamthibitishia kwamba, zitakuwa zinazingatia maslahi ya pande zote mbili kwa mtoa huduma lakini pia kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *deposit*, lengo hapa ni kwa wale wauzaji wakubwa kuweka *deposit* kidogo kwa hii ibara ndogo ya (5), wale watoa huduma wakubwa kwa wateja wakubwa ambao ndiyo wanaombewa *deposit*. Niseme kwamba, bado kuna fursa ya *regulations* kwa upande wa Waziri, bado kuna fursa kwa kanuni ndogo (*rules*), kwa upande wa *EWURA*, lakini pia bado tunakwenda kutengeneza *standard mode* kwa ajili ya leseni. Kwa hiyo, ninapenda kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazingatia ni jinsi gani ibara hii inaweza kutekelezeka kwa mazingira yaliyo bora, badala ya kukwaza wanaopewa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hiyo hiyo ya 23(3)(a), (b) na (c). Kwa maoni yangu ...

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa 22?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Ukurasa wa 22 ndiyo. Nilikuwa ninafikiri tungeiboresha ibara hii kwa kuongeza (d), ambayo ingezungumzia *salary increase*.

**MWENYEKITI:** Samahani, Mheshimiwa Kaboyonga, katika hatua hii sasa ungekuwa umeleta hayo unayopendekeza chini ya Kanuni ya 86. Kwa hiyo, ni wazo zuri, lakini ninaona kama umechelewa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26



**MWENYEKITI:** Ngoja niwakumbushe maana yake wasisononeke tu; Waheshimiwa ukurasa wa 57 wa Kanuni zetu, Kanuni ya 86(9) inasema: “Mbunge yeyote au Waziri anaweza wakati wa mjadala huo, kumshauri mtoa hoja afanye mabadiliko katika Muswada ama mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja Mbunge na wakati wa Kamati ...” Nilikuwa ninakitafuta kile cha wakati wa Kamati, namba (11); Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima, yaani sasa hivi. Kwa mfano, Mheshimiwa Kaboyonga hapa, ninamhurumia lakini sasa siwezi kupindisha, pamoja na kuwa ni Mbunge mwenzangu kutoka Mkoa wa Tabora na tunamheshimu sana, lakini amesahau hii ya (11) inaruhusu hivi sasa tunapoutazama Muswada huu, kama unalo badiliko ukiliwahisha hapa Mezani, basi litasomwa. Ahsanteni sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

Ibara ya 31

Ibara ya 32

Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

Ibara ya 35

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba maelezo na pia nilikuwa nataka kutoa *amendments*.

**MWENYEKITI:** Upande gani sasa?.

**MHE. JOHN M. CHEYO :** Ibara ya 36.

**MWENYEKITI:** Ibara ya 36 ndiyo tulikuwa tunakwenda hivyo. Nilifikiri 35 nilitaka kusema hapana.

Ibara ya 36

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 36(1) mpaka (3), inazungumzia juu ya kuchukua ardhi ya mtu kwa lazima (*compulsory acquisition of land*). Sasa katika dunia ya leo, ambapo tumesema ardhi ina thamani, huyu anayefanya shughuli kwenye ardhi ambayo inachukuliwa anafanya biashara na ile *land acquisition* yake iliyotungwa wakati wa babu zetu ilikuwa ni kwa sababu ya kuchukua ardhi kwa ajili ya shughuli za umma na pia kuna *judgment* au uamuzi wa Mahakama, ambao tayari umeshatolewa.

Pale Ubalozi wa Amerika ulivyochukuliwa kwa matumizi ya umma na Mahakama imeamua kumpa Mwamerika kujenga Ubalozi pale siyo matumizi ya umma na Serikali imeamuliwa kulipa fedha nyingi sana kwa yule mtu aliyekuwa anakaa pale. Kwa hiyo, kwa nini mtu yeyote yule anayetaka ardhi asitumie tu Sheria ya Ardhi ya 1999, Namba (4) na Namba (5) badala ya kwenda kwa *compulsory acquisition*, ambayo kwa ajili ya shughuli ya mtu binafsi ambaye anataka kupitisha umeme ili atengeneze biashara. Kwa hiyo, ninaona kifungu hiki kwanza, kinaweza kuondolewa kwa sababu tayari kuna Mahakama ambayo imekwishatoa uamuzi juu ya ku-*apply* kifungu hiki kwa watu ambao ni binafsi na pili ni uonevu ambao kwa sasa hivi tumeshauona katika Sekta ya Madini, jinsi watu wengi walivyohangaishwa kwa kunyang'anywa ardhi yao na wengi bila kulipwa hata fedha ambayo inakidhi kuweza kuhama pale walipo. Kwa hiyo, ninaomba hiki kifungu chote kifutwe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, *with due respect*, hebu soma kifungu kidogo cha tatu na pengine ukisome kwa sauti ili wewe mwenyewe uone jinsi ambavyo umetaka kutupeleka kwingine kabisa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** “*The Minister responsible of Land shall if is satisfied that the land or interest in land is required for the purpose of providing or maintaining electricity supply services to the public pursue the acquisition of the land on behalf of the licensee in accordance with the Land Act and the Land Acquisition Act.*” Hii ndiyo mbaya zaidi.

**MWENYEKITI:** Unaona raha yake enhee?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Aaa, hii haina raha hata kidogo, kwa sababu hii ndiyo mbaya zaidi. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Hebu jieleze sasa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwa sababu hapa *the public* inayozungumzwa ni *customers, you see*, inaondokana na ile dhana ya umma; *public* ndiyo *customers* na wale *customers* wanalipa na huyu mtu anatengeneza fedha; sasa kwa nini mimi aninyang'anye mihogo yangu na ardhi yangu ili yeye atengeneze fedha na kwa lazima; si afadhali tu kama ni hivyo, tukae tuzungumze kama kuna chochote kile mimi nipate na yeye apate,

lakini ku-*apply* hii sheria, ndiyo njia nyingine ya kuonea wanyonge? Hilo ndilo tatizo langu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, *you are simply reading this upside down.* Hii inaanza hiyo hiyo *process* unayoisema. Ukiisoma hiyo sheria ata-*pursue the acquisition of the land on behalf of the licensee in accordance with the law* ile ile uliyoitaja. Sasa ile ndani yake ina fidia na *compensation; fair and equitable compensation.* Kwa hiyo, huwezi kuzuia mathalan hao wanaofikiwa *public* wapo upande wa pili, wewe ukazuia kabisa hapa. Hicho ndiyo kinazungumzwa, mimi ninaona hapa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama angeweza tu kusimama *with the Land Act* ingetosha. Ugomvi wangu ni pale anaposema *and the Land Acquisition Act*, maana yake akishafika kwa *Land Acquisition Act, the Land Act* ina-*provide process ya proper compensation.* Bahati mbaya tu Mheshimiwa Magufuli, hayupo hapa lakini kitu ambacho watu wengi sasa wamekielewa ni kwamba, hata kama Serikali inajenga *school* au zahanati ni lazima itoe fidia. Kwa *Land Act* sina matatizo nayo, lakini unaposema *The Land Acquisition Act*, hiyo ni tofauti, maana yake *The Land Acquisition Act* wanasema tunachukua kitu ambacho kwa hali ya sasa hakifai na tena hiyo *Land Acquisition Act* ingefutwa katika *Statutes* za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, anatikisa kichwa, *actually process;* basi endelea Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu ni kwamba, kama unataka ku-*acquire land*, Sheria inayotumika ni *Land Acquisition Act*, ndiyo inayoweka utaratibu wote wa ku-*acquire land in the public interest.* Kwa hiyo, huwezi kufuta hiyo *Land Acquisition Act*, kwa sababu ukiifuta tu *then* utakuwa huna utaratibu wa ku-*acquire* hiyo *land* ya mtu mwingine. Kwa hiyo, utaratibu mzima wa ku-*acquire land* unakuwa *provided for under the Land Acquisition Act* na *compensation* unayolipwa ni kwa sababu siku hizi kama alivyosema Mheshimiwa Cheyo ni kwamba, *land* ina thamani; kwa hiyo utalipwa thamani ile ya ardhi yako kama itaonekana ni muhimu ku-*acquire* hiyo *land.* Kwa hiyo, ninadhani kifungu hiki kilivyo hapa kwenye hii sheria, kinafaa kuwa *maintained, otherwise* ukiondoa vyote *then* huyu mtu utachukua *land* yake kwa kutumia sheria ipi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninadhani Mheshimiwa Cheyo, Bunge lipo na linazidi kuimarishwa, unadhani mambo haya yatakuwa yanatokea tu siku za usoni ovyo ovyo? (*Makofi*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye marekebisho ile *Clause* ya 39(5), inazungumzia *where electrical generation is done by using natural resources.*”

Nilitaka kupata ufafanuzi; je, kama unatumia *cultivated resources* kama vile mazao haya ya *bio-fuels* ambayo unaweza kuzalisha dizeli ukatumia kuzalisha umeme; ninaona Muswada upo kimya kuhusiana na *resources* hizo za kuweza kuzalisha umeme, *even* kwenye *rural area or on a large scale*; sasa sijui kama *regulations* zitakazotungwa kwenye Kifungu (6) zitahusisha vilevile *sources* za umeme zinazotokana na *cultivated resources*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hii yote ipo kwenye *schedule of amendment*, huwezi kuiona kwenye *Act* ile; (4) na (5) zinaendelea kwenye *schedule of amendment*. Kwa ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ni kwamba, *details* nyingi pia na mambo hasa ya utekelezaji yatazingatia Kanuni ndogo ndogo, ambazo tunakwenda kuzitayarisha, lakini pia tutazingatia Sheria nyingine kwa mfano, kama nilivyokuwa ninasema, Sheria nyingine ya vyanzo vingine vya nishati, ndiyo hiyo ambayo ipo kwenye mchakato na tutahakikisha kwamba, itazingatia mambo haya. Kwa sasa hivi niseme tu kwamba, Kanuni ndogo zitazingatia jambo hili. Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme mimi si Mwanasheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu, alijibu akisahau kwamba, sisi wengine ni Walimu na hatujui sheria kabisa na amekwenda haraka sana. Mimi bado ningependa kwa sababu swali langu ni dogo sana, sina uhakika kama lipo kwenye ibara ya 40 au 41, nitaomba niambiwe nika. Ningependa kupata *clarification* kidogo tu ya 1.6 trilioni; ninauliza kwamba, awamu ya kwanza ya *approximately* 300bn wameshapewa kama mkopo kupitia benki wakiongozwa na *Stanbic*; nikauliza hivi hiyo 1.6 trilioni katika kufufua *TANESCO*, ndiyo mtiririko huo watakuwa wanapewa kwa mkopo walipe pamoja na riba au kuna taratibu gani? Ningependa hili tueleze vizuri, kwa sababu baadaye litakuja kutuletea matatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, ninadhani hapo hapo linafaa tu kwa sababu ni ku-*restructure*, ku-*foster competition*, kwa hiyo, kuna *capital movement* inatakiwa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme kwamba, wakati ninaelezea pengine nilikwenda kasi lakini pia nilikuwa ninazingatia muda na ni bahati mbaya sana na nilisema kwamba, jambo hili kwa kweli linahitaji maelezo marefu kidogo, lakini jambo moja la msingi nililosema kwa niaba ya Serikali ni kwamba, tayari hata vyanzo vimeshaainishwa; tuna vyanzo mbalimbali na pengine ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, imletee nakala ya vyanzo vile, kwa sababu tunavyo. Kwa mfano, tuna vyanzo kutoka *MMC*, tuna *TEDAP* hii ni kutoka *World Bank*, tuna miradi mingine kupitia Shirika la Uholanzi, kuna msaada tunapata kutoka *SIDA*, *JICA* ya Wajapan na *TANESCO* yenyewe. Kama nilivyosema wakati ninatoa majumuisho, kwenye vyanzo vyao pia kuna *NORAD Funds* na pia mchango wa Serikali na vyanzo vingine mbalimbali.

Kwa hiyo, tunavyo na hii 1.6 trilioni siyo tu kwamba ipo na kwa sababu ule mchakato mzima wa uanzishaji wa hii *plan* ulianzishwa na *TANESCO*, halafu Serikali ikaja kuridhia na tuna vyanzo na mazungumzo yameshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii 300bn/= iliyotoka, ninasema hili ni shirika la kibiashara na mojawapo ya vyanzo vingi tu katika shughuli za biashara zinazofanywa na taasisi kubwa kama hizi ni mikopo. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni mojawapo ya uwezesaji, lakini ikumbukwe kwamba, katika hili Serikali ilitoa *guarantee* na tunafahamu katika tafsiri ya kawaida, *guarantee* inapokuwa imetolewa na mtu yule (*guarantor*), ndiyo hatma ya yote kama atashindwa yule aliyekopa yeye ndiye mwenye jukumu. Kwa hiyo, katika hili Serikali ndiyo ina jukumu la 300bn/= na endapo itajitokeza kwamba, *TANESCO* itashindwa kulipa kwa wakati, nilikuwa ninaomba kumhakikishia mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba, tunayo maelezo ya kutosha lakini pia ninakuahidi kwamba, nitakupa ufafanuzi kwa jinsi ambavyo vyanzo vimeainishwa. Bahati nzuri wale tuliokuwa nao kwenye Kamati wameviona, si kitu ambacho ni siri, kipo wazi, ninaahidi kumpa nakala ya maelezo haya Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru. Nimekubali kwamba, nitahitaji kupata hiyo nakala lakini angenijibu ndiyo au hapana, hii 300bn/= ambayo ni awamu ya kwanza ipo katika 1.6 trilioni. Jawabu hapa ni ndiyo au hapana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Jibu ni ndiyo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasubiri ibara ya 41.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wangapi sasa; Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Anthony Diallo. Haya tunaanza Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ibara ya 41 na zaidi ningemshauri Mheshimiwa Waziri, ajikite kwenye marekebisho ya T(6) *first refusal*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo endelea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimechelewa ku-*widen* kitu kimoja, sijui nitafanyaje sasa; kabla sijasema ninaweza nikapeleka hayo *ahead?* (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, hebu eleza kwanza nitakusaidia tu, *we want to make good laws*.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru sana kama hiyo inawezakana. Sasa hapa amezungumza kitu ambacho ni kizuri. *First refusal* inakwenda *TANESCO; to all intensive electrical energy consumers*. Wakati nilipokuwa ninachangia nilisema kwamba, Mwenyezi Mungu ametupa vyanzo vya umeme; kuna maji, makaa ya mawe, *geothermal energy* na kuna vitu vingi tu na Mungu huenda akatupa pia *uranium*. Sasa kama tumeweza kuona umuhimu wa *consumer* wakubwa kupata *priority* na hili nilimweleza Mheshimiwa Waziri; kwa nini hatujaweza kuona umuhimu wa kuweka *priority* hiyo hiyo kwa *sources?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Malagarasi pale kuna *hydro power, first refusal* to *TANESCO* kama wamo au kipande cha *TANESCO* au kwa Serikali kuliko kutoa tu kwa *anybody*. Sasa nilikuwa ninataka kusema hapo, kama ingeongezwa *energy consumers and sources of electrical power*, hiyo ndiyo nilitaka kuongeza pale ili *refusal* ya kwanza iende kwa Shirika la Umma; *for public participation* kama ni *TANESCO A or TANESCO B* ya baadaye. Sheria *i-recognize* kwamba, wenye mali ndiyo sisi siyo mtu aliye na fedha; mtu unaweza kuwa na hela kama huna *source* huwezi ukatengeneza umeme. Sasa sisi mtaji wetu mkubwa ni makaa, mtaji wetu mkubwa ni *hydro; you know facilities* tulizonazo, mtaji wetu mkubwa ni gesi. Sasa kwa nini hatupatiwi *first refusal*, kama vile tumeona *first refusal* kwa *consumers?* Hilo ndilo tatizo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unaweza kunisaidia kwa *speed* sikuweza kukupelekea ile, iongeze na ile *and sources of electricity power*, nitakuwa *happy* na *I am sure* na Watanzania wengine pia watakuwa *happy*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, inaleta tabu gani hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hoja hii tumeiongelea na Mheshimiwa John Cheyo, tangu kwenye Kamati maana yake tulikuwa naye. Niseme tu kwamba, kwa mazingira haya tunayoongelea, tukumbushane tu kwamba, unajua ukiongelea *TANESCO* kama ni tofauti na Serikali, unaweza kupata hiyo picha ambayo Mheshimiwa Mbunge anaiongelea. Tunapoongelea *TANESCO*, ndiyo Tanzania yenyewe ya leo na ndiyo sisi ambao kimsingi, rasilimali fedha hazitoshi kuweza kuendeleza vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna jambo moja hapa la kuona kwamba, *TANESCO* ndiyo Tanzania na ndiyo Serikali na kwamba, tunazo fedha za kuwekeza?. Hata sera hii leo tunayosema tuitekeleze kwa kufunga milango, inazingatia kwamba sisi kama Taifa, hatuna huo uwezo ingawa tuna vyanzo vingi. Nimekuwa nikisema tuna vyanzo ambavyo vinaweza kutuzalishia umeme megawati zaidi ya 4,700, lakini bajeti yetu ndiyo hii, leo tunasema tunahitaji fedha kiasi cha shilingi trilion 1.2 kupeleka Miradi ya Umeme vijijiniwala huendelezi vyanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kwamba, ninaelewa anachokisema, lakini tutazingatia rasilimali hii ni ya Tanzania kwa ujumla na ni rasilimali yetu, hatutarajii kwamba, tukiliambia Shirika la *TANESCO* liwe na *the right first refusal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kwamba, ilivyosimama hivyo, haitupunguzii umiliki wa rasilimali hizi ni zetu Watanzania. Wenzetu wanakuja ku-*team-up* kutuongezea nguvu ili tuweze kuzi-*harmonise* kwa haraka kidogo, kuliko ambavyo tungesubiria mpaka tufikie wakati fulani ambapo tumeiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikumbushe lingine, wakati tunapoongelea habari ya *capacity charge*, nilisema na ulikuwa ni ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, itakapofikia wakati ambapo *TANESCO* itakuwa na uwezo, itawekeza kwenye vyanzo hivi ili hatimaye iondokane na haya mambo ya *capacity charge*, kwa sababu itakuwa ina *own*, ku-*transmit* na ku-*supply* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba, jambo hili ni la kwetu sisi kama Taifa, lakini pia linaweza changamoto mbele yetu kwamba, tuna uwezo kama Taifa, kwa sababu *TANESCO* ndiyo Taifa la Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ninadhani kama Mheshimiwa Waziri ameondoa hofu ile, hebu kaa kwanza. Ulichokuwa unakisema ni ile hofu kwamba, wawekezaji binafsi watavamia ile minofu, watachukua *Stiegler's Gorge* na *uranium*. Sasa hiyo inawezekana

mahali ambapo hakuna *regulation* kabisa, lakini *elsewhere* katika namna ya kuwapa hiyo miradi, ninadhani Serikali inasimamia *and that is the better safeguard* kuliko hata kusema tuwe tunauliza tu kwanza *TANESCO* wakisema *they can not do it* ndiyo mtu anapewa. Kuna *restrictions* zilizomo ndani za ku-grant *project licences*, siyo kila mtu atakuja kuchukua *uranium* bure, unachukua *Stiegler's Gorge* bure. Ninadhani ukipata *assurance* hiyo inatosha kabisa. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, simpingi mdogo wangu, ninaona ana roho nzuri ya Tanzania. Tatizo tunatunga Sheria ambayo ni *impersonal*; haina mtu, yeye leo yupo sawa, ulisema hivi *fine; tomorrow* kuna jamaa mwingine ambaye kazi yake ni *ten percent* tu; *what do we do?* Hapa asinishike kwa *TANESCO*. Dhana kubwa ninayotaka kuileta hapa kwanza ni *the fact* kwamba, tuna *uranium* itakuwa *streamed dangerous* kwa Serikali kuwaachia iende kwa mtu binafsi tu. Mwamerika anaifuata *uranium* mpaka Iran kuhakikisha kwamba Iran haitumii hiyo *uranium* inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalau wangetafuta njia na yeye nilimwambia mapema, atafuate njia ambapo Serikali ina-*participate* katika *areas* ambazo ni kubwa na kwa majibu yake amezungumzia juu ya *PPP*. *There is no where in the law*, ambayo inatoa hiyo fursa. Akiniambia kwamba, ataweka kwenye *regulations*, lazima *in any merger investment* patakuwa na *free carried shares*, hiyo ninaweza nika-*concede* kwamba, *okay* ni afadhali. Hakuna tatizo la kuiweka hapo kwamba, katika miradi mikubwa Serikali itapata *first refusal; something like that* kui-*safeguard* hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, hayo unayoyasema siyo mahali pake hapa. Hii ndiyo njia ya moja ya kushughulikia haya, lakini lingine ni zile Sheria nyingine ambazo zinasimamia utaratibu mzima wa kupewa leseni ya mradi ambayo Waziri huyu siyo yeye kama Mheshimiwa William Ngeleja, Wizara lazima izifuate na izirudishe hapa Bungeni. *Nobody can give huge sources* hivi hivi *in the present circumstances*, bila kufuata Sheria *proper* za *licencing* ya hizo *projects* ambazo ni *multi-sectoral*, zinapita katika sehemu nyingi. Hivyo, ndivyo ninavyoona anachosimamia kama Serikali. Kuiweka kwenye *TANESCO* peke yake, haitusaidii sana. Ninadhani tuendelee.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hapana! Malumbano na Spika hayaruhusiwi. Nitakwenda kwenye Kanuni na itakuwa shida bure. Ninakuheshimu sana. Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwishayafikisha Mezani mapendekezo yangu; ibara ya 41(7), pamoja na marekebisho yake; pale penye marekebisho mstari wa mwisho, panasema kwamba, wale ambao sasa hivi wana Mkataba na Serikali na *TANESCO*, hawatalazimika kupata *licence* mpaka baada ya miaka mitano. Mimi nimependekeza kwamba, hao nao wawe *subject of the licence under this Act*.



**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, hebu malizia basi sababu zake nini sasa?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zake ni kwamba, imekwishajitokeza wazi kwamba, Mikataba iliyopo mingi ni mibovu. Sasa kwa nini tuchukue Mikataba mibovu tunakwenda nayo mbele, yaani leo tuhalalishe kwamba ile Mikataba mibovu twende nayo tu mbele kwa miaka mitano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninadhani ungependa kutoa ufafanuzi; ninadhani kuna *process* nyingine inaendelea Kiserikali kuhusu Mikataba mibovu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa kwa suala ambalo ameuliza Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, linahusu wale ambao wapo hapa na kama ambavyo tumeweka marekebisho kwenye hiyo Ibara ya 41(7); kwanza, sina uhakika kama Mheshimiwa Kaboyonga amesoma majedwali yote mawili ya rekebisho la pili lile? Niseme tu kwa ujumla kwamba, tunaendelea na zoezi la kupitia hiyo Mikataba, ipo Mikataba mingine haitafika hiyo miaka, kwa sababu hata kwa jinsi inavyosimama haifiki. Kwa sababu walengwa wakuu hapa zilikuwa ni hizi *rental powers*. Sasa hakuna hata mmoja kati ya hao, ambaye ana Mikataba unaoweza kutufikisha miaka mitano mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi tunasema lengo la ibara hii ni kwamba, baada ya Mikataba yao, sasa ukisema miaka 20 itakapopita hapa kwa kipindi cha miaka mitano, wasishiriki huku kwa sababu ya sababu ambazo tumezisema na madhumuni yake ni kwamba, yapo manufaa ambayo wamekwishayapata; tayari ukiwaachia itakuwa wana *undue advantage* dhidi ya wale wengine ambao wanakuja *fresh*, tumesema kwamba pengine hao wasubiri kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo hasa lengo letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Muda hauruhusu, tunaingia kipindi ambacho kinafanana na *guillotine* sasa. Kwa hiyo, hatuwezi kuvunja Kanuni hata hiyo nusu saa sasa imepita na Muswada huu umeshughulikiwa miezi mitatu, sasa inakuwa ngumu kidogo. Ninadhani tutaendelea kuuboresha tu Muswada huu. inaaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunakwenda kwa sehemu siyo ibara. Katibu nenda Sehemu ya Nane.

Sehemu ya 9

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, iliyokuwa Sehemu ya Nane imekuwa Sehemu ya Tisa?

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bung  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 10

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007  
(The Electricity Bill, 2007)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria, ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 (*The Electricity Act, 2007*), kama ulivyorekebisha katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara  
ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutangaza kwamba, Muswada wa Umeme (*The Electricity Bill, 2007*), sasa umepitishwa rasmi na Bunge na sasa Muswada huo utashughulikiwa kwa taratibu za kawaida ili kuweza kuwa Sheria. Ninawapongeza wote kwa sababu mmekuwa na kazi ngumu, lakini hatimaye tumeweza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaona nichukue nafasi hii, nitoe matangazo, siku zijazo hizi tatu, mfahamu tutakuwa na Shughuli gani ili muweze kujipanga.

Waheshimiwa Wabunge, kesho Siku ya Jumatano baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu, tutakuwa na Uchaguzi wa Wajumbe katika Bodi ya Chuo cha Ufundi

Arusha na Mbunge mmoja wa Bunge la Afrika, kuchukua nafasi ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, hiyo itakuwa mpaka saa 5.00. Kuanzia saa 5.00 hadi 7.00 mchana, halafu saa 11.00 hadi 1.45, tutapokea na kujadili Taarifa za Kamati za PAC na LAAC; Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa, siku itakuwa imekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, Siku ya Alhamisi saa tatu kamili, tutakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu na kuanzia saa 3.30 hadi 4.30 kitakuwa ni kipindi cha maswali ya kawaida. Saa 4.30 hadi saa 7.00 mchana na saa 11.00 hadi 1.45 tutakuwa na hoja binafsi zifuatazo: Moja, hoja ya Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji. Pili, hoja ya Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro kuhusu Uuzwaji wa Nyumba za Serikali. Tatu, hoja ya Mheshimiwa Said Amour Arfi kuhusu Utendaji Kazi wa Kampuni ya Reli (TLA), baada ya Ubinafsishwaji. Nne, hoja ya Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi kuhusu Utendaji Kazi wa *Tanzania Internal Container Terminal Services (TICTS)*. Hizo ni hoja nne kwa siku nzima ya Alhamisi.

Waheshimiwa Wabunge, Siku ya Ijumaa ni siku ya hitimisho la Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge tarehe 25 Aprili, 2008, saa 3.00 hadi 4.30 kipindi cha maswali na majibu. Saa 4.30 hadi 5.00 ni kusomwa kwa Mara ya Kwanza Miswada sita ambayo siwezi kupoteza wakati kuitaja, mnaifahamu na imekwishagawiwa. Saa 5.00 hadi 6.00 mchana Maazimio mawili. Kwanza, Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2006 na pili, Azimio la Bunge Kuridhia Uanzishwaji wa Bunge la SADC. Saa 6.00 nitamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu ili atoe Hoja ya Kuliahirisha Bunge. Hizo ndizo Shughuli zilizopangwa, tutawagawia mtazipata ili muweze kujipanga kuona ushiriki wenu.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa Kuahirisha Bunge umepita na sasa ninaliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.13 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,  
Tarehe 23 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*